# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Agosti 6, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579989

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



ST.JOSEPH UNIVERSITY
In Tanzania
"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019, "Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz

For more information contact:
+255 676 504 147
+255 745 281 505

215359802




## Kesi ya kina Mbowe siku tano mfululizo

UKURASA 3

# Mwandishi kortini tuhuma makosa yasiyodhaminika

UKURASA 2



Rais John Magufuli akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alipotembelea banda la benki hiyo lilipo katika mkutano mkuu wa SADC unaofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo, Tully Mwambapa. Benki ya CRDB ni mmoja wa wadhamini wakuu wa mkutano huo 2019. **PICHA: IKULU**

# Nyundo 6 za JPM viwanda SADC

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**SPIKA NDUGAI ATAKA UZAZI WA KIUCHUMI**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka Watanzania kuzaa idadi ya watoto kulingana na uchumi...

**UKURASA WA 4**

**JK ATOA NENO KWA WAKULIMA, WAFUGAJI**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete, amewataka wakulima na wafugaji kuendelea kusikiliza...

**UKURASA WA 10**

**VYOMBO VYA USAFIRI ZIWA VICTORIA VYAKOSA MABOYA**

VYOMBO vya usafiri majini katika Ziwa Victoria vinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na maboya...


## Polisi waonya wenye ving'ora

UKURASA 3


**MICHEZO** NDAYIRAGIJE AFUNGUKA UDHAIFU TAIFA STARS UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Mwandishi kortini tuhuma makosa yasiyodhaminika

**Na Hellen Mwango**

VILIO na simanzi vilitawala jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisitu, jijini Dar es Salaam, baada ya mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera (39), kufikishwa mahakamani hapo kwa ajili ya kusomewa mashtaka yanayomkabili.

Vilio hivyo vilitoka kwa watu wanaodaiwa kuwa ndugu na marafiki wa Kabendera, akiwamo Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe.

Kabendera alifikishwa mahakamani hapo saa 6:30 mchana akiwa kwenye gari la Jeshi la Polisi aina ya Toyota Land Cruiser chini ya ulinzi wa askari kanzu.

Baada ya kufikishwa katika eneo la mahakama, alipandishwa ukumbi namba mbili wa mahakama hiyo.

Mwanahabari huyo ambaye pia ni mfanyabiashara, alisomewa mashtaka matatu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, likiwamo la kujihusisha na magenge ya uhalifu, kukwepa kodi na kutakatisha fedha Sh. milioni 173.2.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Paul Kadushi, Faraja Nchimbi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, ulimsomea mshtakiwa huyo mashtaka yake.

Kadushi alidai kuwa kati ya Januari 2015 na Julai 2019, Kabendera akiwa na wenzake ambao hawajafikishwa mahakamani, walitoa msaada katika genge la uhalifu kwa kujipatia maslahi binafsi.

Nchimbi alidai katika shtaka la pili kuwa, kati ya Januari 2015 na Julai 2019, mahali tofauti bila sababu za msingi mshtakiwa alishindwa kulipa kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Sh. 173,247,047.02.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu, mshtakiwa anadaiwa kuwa kati ya Januari 2015 na Julai 2019, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 173.2, huku akijua ni mazalia ya kutakatisha fedha zilizotokana na kukwepa kodi.

Hata hivyo, kesi hiyo ya uhujumu uchumi iliyopewa usajili namba 75 ya mwaka huu, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote.

Hakimu alisema mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo mpaka pale itakapopewa kibali na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika kuhamishiwa Mahakama

INAENDELEA UK 8



Mshtakiwa Erick Kabendera, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam na kusomewa makosa mbalimbali ikiwamo utakatishaji fedha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waziri ataka mazingira bora uwekezaji SADC

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ametoa wito kwa nchi zote za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kutilia mkazo uboreshaji wa mazingira wezeshi na wadau mbalimbali kujitokeza kuwekeza katika viwanda.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya nne ya Wiki ya Viwanda ya SADC jijini Dar es Salaam, akiungwa mkono na Katibu Mtendaji wa jumuiya hiyo, Dk. Stergomena Tax na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Salum Shamte.

Watatu hao pia walimpongeza Rais John Magufuli kwa jitihada kubwa za kujenga mazingira wezeshi ya ujenzi wa viwanda nchini.

Bashungwa alisema Tanzania imekuwa ikifanya vizuri katika biashara ndani ya SADC katika mauzo. Alibainisha kuwa mauzo ya Tanzania kwenda nchi za SADC kwa mwaka 2018 yalikuwa Dola za Marekani milioni 999 ikilinganishwa na Dola milioni 875 mwaka 2017.

Alisemu takwimu hizo zinaonyesha ongezeko la asilimia 12.16 na uingizaji wa bidhaa Tanzania kutoka SADC uliongezeka kutoka Dola milioni 600.64 mwaka 2017 hadi kufikia Dola milioni 604.32 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.61.

Alitaja bidhaa muhimu ambazo Tanzania inauza SADC kuwa ni pamoja na madini mbalimbali kama vile tanzanite na dhahabu, bidhaa za kilimo kama vile chai

INAENDELEA UK 8

# Nyundo 6 za JPM viwanda SADC

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefungua Maonyesho ya nne ya Wiki ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kuhimiza nchi wanachama kutilia mkazo mambo sita, ili kutekeleza mkakati wa SADC wa Maendeleo ya Viwanda 2015 - 2063.

Ufunguzi huo ulifanyika jana katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri, makatibu wakuu, mabalozi, wabunge na Sekretarieti ya SADC.

Rais Magufuli ambaye aliongozana na mkewe, Mama Janeth Magufuli, alisema pamoja na kuwapo kwa Mkakati wa SADC wa Maendeleo ya Viwanda, bado kasi ya ukuaji wa viwanda ni ndogo na hivyo kusababisha viwanda kuendelea kutoa mchango mdogo katika maendeleo ya kiuchumi kwa nchi za SADC.

Alisema nchi za jumuiya hiyo zinapaswa kuweka kipaumbele kwenye uhaulishaji wa teknolojia ya viwanda ndani ya jumuiya na Afrika kwa ujumla kabla ya kwenda mbali.

Alisema suala hilo linapaswa kwenda sambamba na uanzishaji na uimarishaji wa viwanda vidogo ambavyo hukua na kuwa vikubwa baadaye.

Alisema jambo lingine muhimu ni kuuziana malighafi na bidhaa nyingine ili kukuza mtaji na kuendeleza viwanda ndani ya jumuiya.

"Kama ni magari yanahitajika kununuliwa kutoka Afrika Kusini kuja Tanzania yanunuliwe na kama sukari inatoka Maurius kuja Tanzania inunuliwe huko badala ya kununulia kwingine ili kujenga soko la watu milioni 350 ndani ya SADC, tutajenga uchumi ndani ya jumuiya," alisema.

Rais Magufuli pia alisisitiza kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza sekta ya viwanda kwa kuwa na nishati ya umeme wa bei nafuu na miundombinu ya usafiri na usafirishaji, akieleza kuwa ndiyo sababu Tanzania inatekeleza mradi wa umeme wa maji, kujenga reli ya kisasa na barabara.

Alisema jambo la nne ni kushughulikia vikwanzo vinavyochelewesha maendeleo ndani ya SADC na Afrika, akivitaja kuwa ni pamoja na kuwekeana vikwazo visivyo vya maana kwenye biashara.

Alivitaja kuwa ni utitiri wa taasisi za udhibiti, kodi, tozo, urasimu wa taratibu za uwekezaji na vikwazo vya mpakani.

Rais Magufuli pia alishauri kuhimiza sekta binafsi kwenye nchi husika kuwekeza kwenye sekta ya viwanda kwa kuwa ndiyo wahusika wakuu katika kujenga viwanda.

"Changamkieni fursa zilizopo. Sekta binafsi za SADC ziache kulalamika, ziendelee na changamoto na kuzitatua, hakuna vitu vinavyokuja bure bure, ujumbe umefika," alisema.

Rais Magufuli pia alishauri nchi za SADC kutumia fursa ya kuwa na malighafi nyingi, kuwekeza kwenye viwanda kwa kuwa kila nchi ina utajiri wa madini, mafuta, gesi, kilimo, uvuvi, ufugaji na soko ni kubwa.

Alisema Afrika imechelewa sana kwenye maendeleo na sasa inapaswa kukimbia badala ya kutembea.

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka (katikati), akimtambulisha Mkurugenzi wa Uendeshaji Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Anselim Peter (kushoto), kwa Meneja Msaidizi Idara ya Uhusiano na Itifaki Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Vicky Msina, wakati mkuu wa mkoa huyo alipoongozana na viongozi wa baadhi ya taasisi zinazoshiriki maonyesho ya Nanenane kutembelea banda la WCF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya kina Mbowe siku tano mfululizo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepanga kusikiliza siku tano mfululizo kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe na wenzake wanane ushahidi wa upande wa Jamhuri.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa jana na leo, lakini upande wa utetezi uliwasilisha barua ya kuwaombea ruhusa mshtakiwa wa kwanza Mbowe na John Heche, kwa kuwa wamefiwa na kaka zao.

Hata hivyo, mshtakiwa Mbowe alifika katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba kwa ajili ya kusikiliza kesi yake.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Peter Kibatala, ulidai kuwa mapema mahakamani hapo aliwasilisha barua ya kuwaombea ruhusa washtakiwa hao wawili baada ya kila mmoja kufiwa na kaka yake.

Alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza amefika mahakamani kwa kuwa amemaliza shughuli za msiba wa kaka yake, lakini mshtakiwa Heche bado hajamaliza mazishi hivyo aliomba kesi hiyo kupangwa tarehe nyingine ya kusikilizwa.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Salim Msemo, ulidai kuwa kutokana na mazingira hayo hauna pingamizi.

Hata hivyo, Nchimbi alidai kuwa mahakama izingatie mambo mawili, kwanza kesi zilizokaa muda mrefu zinatakiwa kusikilizwa haraka na kutolewa maamuzi, pili, shahidi wa sita ameshikiliwa muda mrefu na kwamba anatarajiwa kwenda kwenye mafunzo ya kijeshi Nairobi, nchini Kenya.

Hakimu alisema kesi hiyo itasikilizwa mfululizo siku tano, Agosti 15, 16, 20, 21 na 22.

Alisema dhamana za washtakiwa zinaendelea.

Mapema mahakamani hapo, shahidi wa sita Koplo Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi, alidai kuwa alikimbilia kwenye gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Vile vile, alidai mihemko hiyo ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya serikali.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuripoti mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video, ilipofika saa 10 alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani, nilimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali," alidai na kuongeza:

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuliposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Mbali ya Mbowe na Heche washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Iringa Mjini, Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka huu Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16, mwaka huu Barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Wilaya ya Kinondoni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na

INAENDELEA UK 8

# Polisi watangaza msako magari yenye ving'ora

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema kuanzia leo, litakuwa na msako wa magari binafsi, bajaji na pikipiki zilizoweka taa zenye mwanga mkali (spot light) na ving'ora.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa alitangaza msako huo jana jijini alipozungumza na waandishi wa habari walivyojipanga kuimarisha ulinzi wakati wa mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Kuanzia kesho (leo) tutaanza kukamata magari binafsi, pikipiki na bajaji walioweka taa za vimulimuli au rangi, taa zenye mwanga mkali na ving'ora," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema yeyote atakayekamatwa, atawekwa ndani na gari lake litabadilishwa taa hizo likiwa polisi.

"Magari yanayoruhusiwa kwa mujibu wa sheria kuwekwa 'spot light' au ving'ora ni yanayotoa huduma za dharura tu na ya kampuni binafsi za ulinzi. Wapo watu wanaoweka kwa sababu ving'ora na taa vinauzwa madukani, wanakwenda kununua na kufunga kwenye magari yao. Tutawakamata wote, msako huu siyo kwa sababu ya mkutano wa SADC, utakuwa endelevu," alisema.

Mambosasa alisema wanaofanya hivyo wamekuwa wakileta usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara, hasa nyakati za usiku ambao hudhani ni msafara wa kiongozi hivyo hukaa pembeni kupisha.

Akizungumza kuhusu pikipiki, Kamanda Mambosasa alisema kuanzia leo hadi mkutano wa SADC utakapoisha, waendesha bodaboda hawataruhusiwa kuingia na pikipiki zao katikati ya jiji.

"Ni marufuku kuanzia hadi Agosti 18 bodaboda kuingia katikati ya jiji. Tumepiga marufuku kwa sababu baadhi yao hujihusisha na vitendo vya uhalifu, tunawataka watii kwa sababu kinyume cha hapo utakamatwa," alisema.

Mambosasa pia alionya bodaboda wenye tabia ya kuingilia misafara na wasiovaa kofia ngumu.

# Spika Ndugai ataka uzazi wa kiuchumi

**Na Mary Geofrey**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka Watanzania kuzaa idadi ya watoto kulingana na uchumi wa familia.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa siku mbili wa wabunge wa nchi za Afrika na Asia, waliokutana kujadili ukuaji wa maendeleo na idadi ya watu.

Alisema taifa linapaswa kuwa na idadi ya watu endelevu ambao watanaishi maisha marefu na wenye uchumi mzuri.

"Jambo la muhimu hapa na ujumbe wangu ni idadi ya watoto ilingane na uchumi wa familia au kaya na taifa. Kuhusu idadi ya watoto mtu azae wangapi, inategemea na uchumi wa familia husika," alisema.

Alisema suala la uchumi haliwezi kuangaliwa kitaifa, bali linatakiwa kuliangalia katika ngazi ya familia ndipo matokeo ya kitaifa yataonekana.

Alisema Bunge litaendelea na

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
**06/08/2019**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **07/08/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEARS CONSTRUCTION & INVESTMENT** itapita bila mzigo kutoka KABANGA kuelekea SUMBAWANGA gari hilo lenye namba za usajili: **T349 BNT/T 646 BCJ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 20.0
   Upana –mita 3.0
   Kimo – mita 2.90

3. Njia itakayotumika **KABANGA hadi SUMBAWANGA** kupitia **MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## Malezi ya yatima 100 kugharamiwa

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo' ameahidi kugharamia malezi ya watoto yatima 100 katika kituo cha kutunza watoto yatima cha Makao Makuu ya Watoto Kurasini jijini Dar es Salaam.

Vilevile, Mo, mmoja wa mabilionea vijana barani Afrika, ametoa msaada wa Sh. milioni 10 zitazotumika kununua mashine za kutotoresha mayai kwa ajili ya kituo hicho.

Dewji alitoa ahadi hiyo alipotembelea kituo hicho mwishoni mwa wiki, akieleza kuwa utekelezaji wa ahadi hiyo utafanyika chini ya taasisi yake ya Mo Dewji.

Akizungumza na viongozi, watoto wanaoishi kwenye kituo hicho, Dewji alisema anatambua watoto hao wanapitia katika kipindi kigumu na anaamini msaada huo utasaidia kuboresha maisha yao.

Alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais John Magufuli za kuboresha maisha ya Watanzania.

Alisema yeye ni mfanyabiashara ambaye anaunga mkono juhudi za serikali na anaamini ana wajibu wa kusaidia jamii inayomzunguka, hasa watu wenye uhitaji wakiwapo watoto yatima.

"Mimi najua hata Mheshimiwa Rais atapenda jambo hili - mimi nitagharamia mwenyewe huduma zao hapa na hela zao zote za matumizi nitatoa mimi. Na pia najua wanahitaji kupata sehemu ya malazi, mtakaa mkubaliane, sisi tutakuja kujenga majengo kwa ajili ya hao watoto 100 wakae.

"Taasisi ya Mo Dewji itawagharamia. La pili, tutajenga miundombinu ili watoto waishi kwenye mazingira mazuri na la tatu, nitatoa Sh. 10 milioni ili zitumike kufanya biashara ili watoto waishi kwenye mazingira mazuri na bora zaidi," Dewji aliahidi.

Akitoa taarifa kuhusu kituo hicho, Ofisa Mfawidhi wa Makao Makuu ya Watoto Kurasini, Beatrice Laurance, alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinakwamisha mipango yao ya kuwa na biashara ambazo wanaamini zitawawezesha kujiendesha.

"Tunashukuru sana kwa msaada ambao umetupatia, ambao utasaidia kuboresha maisha ya watoto tunaoishi nao hapa kituoni. Ni wazi sasa kwamba maisha ya watoto hawa yatabadilika," alisema.

Kituo hicho kilianzishwa mwaka 1975 na kwa sasa kinatunza watoto 72 ambao wengi wao ni wadogo na wengine wanasoma shule za msingi na wachache wako sekondari na vyuo vikuu.

# JK aeleza umuhimu wa wataalamu kilimo, ufugaji

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete, amewataka wakulima na wafugaji kuendelea kusikiliza ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema kwa kufanya hivyo wataongeza tija katika uzalishaji, na kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

Aidha, Kikwete amewakata wataalamu kutoa ushauri na mawazo mapya kulingana na hali halisi ya mazingira ili kusaidia makundi hayo kuongeza tija, kuboresha mazao, kuongeza kipato na kumudu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayojitokeza.

Kikwete alisema hayo baada ya kutembelea viwanja vya maonesho ya kilimo na mifugo vya Kanda ya Mashariki vya Mwalimu J.K Nyerere, vinavyojumuisha waoneshaji kutoka mikoa ya Morogoro, Tanga, Dar es Salaam na Pwani.

Aliwataka wataalamu kusambaza utafiti mbalimbali wanaoufanya kwa wananchi badala ya kuhifadhi makabatini ili uwasaidie wakulima, wafugaji na wavuvi kwa maendeleo yao.

Akiwa katika banda la Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani, Kikwete alishangazwa kuona bata waliopo hawana maji, hivyo akawataka waonyeshaji kupeleka elimu kwa uhalisia ili wananchi wajifunze kwa vitendo kwani anachojua kwenye bata, huwa wanahitaji maji mengi, na wanaokwenda katika eneo hilo wajifunze kuwa bata hahitaji maji katika ufugaji wake.

Hata hivyo, alieleza kuridhishwa na mambo mengi mapya katika maonyesho ya mwaka huu kwa Kanda ya Mashariki, zikiwamo teknolojia mpya na vipando, hali inayoonyesha kupigwa hatua za kimaendeleo.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema wizara yake itaanza rasmi kuutumia ipasavyo utafiti unaofanywa na wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili katika vyuo vikuu nchini kwa kuwa umeonekana kuwa na manufaa makubwa kwa serikali na wananchi licha ya kutotiliwa maanani kwa kinachoainishwa katika matokeo yake.

Waziri Mpina alisema hayo kwenye maonyesho hayo, baada ya kutembelea mabanda kadhaa likiwamo la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Kaimu Naibu Makamu wa chuo hicho, Dk. Samuel Kabote, alibaini changamoto ya kutotumika serikalini kwa matokeo ya utafiti mbalimbali, hali inayokwamisha matokeo mengi ya utafiti kushindwa kuwafikia vyema wananchi.



Wachoraji wa sanaa za mikono kutoka soko la Tinga Tinga jijini Dar es Salaam wakiandaa michoro ya rangi zenye kung'aa, katuni, mapambo na vidoti kwa ajili ya maonyesho ya nne ya bidhaa kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) yaliyofunguliwa na Rais John Magufuli jijini humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Pinda atoa ushauri kuipanga Dodoma

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameushauri uongozi wa Jiji la Dodoma kwenda China kujifunza namna ya kuupanga mji huo ili uendane na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Pinda alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuonyesha vyakula vyenye asili ya China ambayo iliandaliwa na Ubalozi wa Watu wa China.

"Nilipokuwa katika jimbo moja la China, nilipata bahati ya kwenda katika maonyesho ambayo dhamira yake ilikuwa ni kutaka watu wajue wamepiga hatua katika mipango miji.

"Na ni kweli wamepiga hatua kubwa sana na miji yao ni mikubwa na imepangwa vizuri na maeneo mengine ukiambiwa ni makao makuu ya mkoa huamini.

"Ndiyo maana nimemwomba sana Balozi wa China nchini, atusaidie kutuunganisha katika miji iliyojengeka vizuri nchini kwake ili kile tulichokiona kule cha mipango miji na sisi tupeleke vijana wetu kwenda kuona na kujifunza na wakirudi wanakuwa wamepanuka vizuri uelewa juu ya mipangomiji.

Pinda pia aliwashauri Watanzania kuanza kutengeneza vyakula vya asili ya China katika hoteli wanakofikia watalii kutoka nchi hiyo.

"Dhamira kubwa ni kwamba wameona Tanzania ina mwelekeo wa mvuto kwa watalii kutoka China. Kwa hiyo, wanaona ni vema wanapokuja kufanya utalii, wanapata kabisa na vyakula vya kwao.

"Hata mazao yetu tunayolima wenyewe wamesema wanaweza kuyatumia hayo katika kupika chakula cha kichina," Pinda alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema tayari wamekamilisha mapitio ya mpango kabambe wa makao makuu ya nchi ambao utaendana na mabadiliko yaliyofanyika ya ujenzi wa mji huo.

"Tangu mji (wa Dodoma) umejengwa ni zaidi ya miaka 40, kwa hiyo hatuwezi kwenda na mpango uleule, mpango huo utatoa taswira ya Dodoma katika miaka 20 ijayo.

"Waziri Mkuu mstaafu yuko sahihi na sisi tunalifanyia kazi na tunaamini miaka kadhaa ijayo litakuwa jiji la mfano kwa sababu linajengwa katika karne ya 21 na teknolijia mpya,"alisema.

Balozi wa China nchini, Wange Ke, alisema kama ambavyo wamekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania, watahakikisha wanawaunga mkono katika ujenzi wa jiji hilo hususani kwa kuwapekeka wataalamu kwenda kujifunza nchini mwao.

"TTB (Bodi ya Utalii Tanzania) kwa sasa inafanya kazi kubwa ya kutangaza utalii Tanzania na kwa sasa inapata watalii wengi wakiwamo wanaotoka China.

"Kutokana na hali hiyo, ni vizuri pia watumie fursa hiyo kuhakikisha hoteli wanazokuwa wanafikia watalii, zinakuwa na vyakula vya aina mbalimbali vikiwamo vya China na hii itavutia zaidi," alisema.




BONITE BOTTLERS LIMITED

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**DEREVA WA MAGARI MAKUBWA.**
**(TRUCK & TRAILER)**

**SIFA ZA MUOMBAJI.**

1. AWE NA ELIMU YA DARASA LA SABA NA KUENDELEA.
2. AWE NA UMRI KATI YA MIAKA 25 NA 45.
3. AWE NA UZOEFU WA KUENDESHA MAGARI MAKUBWA KWA MUDA USIOPUNGUA MIAKA MITANO NA KUENDELEA.
4. AWE NA LESENI MPYA
5. AWE NA BARUA YA UTAMBULISHO KUTOKA KWA MWAJIRI WAKE ALIPOKWISHA FANYA KAZI AU CHETI CHA UTUMISHI.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI.**

Barua zote ziambatanishwe na vivuli vya vyeti vya taaluma, barua za utumishi (Certificate of service), leseni ya udereva, namba za simu n.k. Barua za maombi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Bonite Bottlers Limited kwa anuani hapo chini.

MKURUGENZI MTENDAJI,
BONITE BOTTLERS LTD,
P.O.BOX 1352,
MOSHI.

Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe 16/08/2019



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sensa ya kilimo, uvuvi, ufugaji ina umuhimu

TAARIFA kwamba Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inakusudia kufanya sensa ya kilimo, uvuvi na ufugaji nchini ili kupata matokeo ya mchango wa sekta hiyo kwenye pato la Taifa na kupanga mikakati mingine mipya, zina mantiki.

Ofisi hiyo imesema kuanzia timu ya wataalamu wa NBS ipo mkoani Morogoro kwa ajili ya kufanya zoezi la majaribio katika mikoa sita ya Bara na miwili Zanzibar na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha ili kusaidia kupatikana kwa takwimu hizo.

Akizungumza katika Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane yanayoendelea mkoani Simiyu. Mtakwimu Mwandamizi kutoka ofisi hiyo, Samwel Kawa, alisema kupatikana kwa takwimu hizo zitawezesha kupanga, kupima na kufuatilia Tathmini ya Programu ya Pili ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP II) .

Alisema pia kupatikana kwa takwimu hizo kutasaidia kufikia uchumi wa kati wa Tanzania ya viwanda pamoja na malengo ya maendeleo endelevu na mpango wa pili wa Taifa wa maendeleo na usalama wa chakula pamoja na vita dhidi ya umaskini.

Kawa alisema sensa ya kilimo ya mwisho ilifanyika mwaka 2007/2008, hivyo kufanyika kwa sensa mpya kutatoa takwimu mpya kuhusu uzalishaji wa mazao, idadi sahihi ya mifugo pamoja na mazao yatokanayo na mifugo.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba Tanzania kwa sasa inaelekea katika safari ya uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda. Ikumbukwe kwamba viwanda vinahitaji malighafi zitokanazo na kilimo, uvuvi na mifugo.

Kwa maana hiyo haiwezekani tena kuendesha na kusimamia sekta hizo nyeti bila kuwa na takwimu sahihi, halisi na zinazokwenda na wakati.

Tunaona kwamba uamuzi wa kufanya sensa ya kilimo, mifugo, uvuvi kwa sasa ni wa mantiki kwa sasabu upo uwezekano kwamba takwimu nyingi za sasa hazina uhalisia kwa sababu umepita muda mrefu bila sensa hiyo kufanyika.

Taarifa kuwa sensa ya mwisho ilifanyika mwaka 2007/2008, zinatoa picha kuwa tamwimu zinazotumika kuhusiana na masuala ya sekta hizo zina mapungufu makubwa yasioendana na hali halisi, hivyo upo uwezekano makubwa wa kutoa takwimu zisizo za uhakika.

Kwa hali hiyo unaweza kupotosha takwimu kuhusu uzalishaji wa mazao, idadi sahihi ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo pamoja na idadi ya samaki walioko nchini.

Kwa hiyo takwimu halisi za sekta hizo zitaiwezesha serikali, wananchi, wadau pamoja na wawekezaji kuwa na uelewa mpana ili pale wanapotaka kufanya shughuli zao wafanye kwa kuzingatia takwimu.

Kwa mfano, serikali itapanga mipango yake ya kuzisaidia na kuziwezesha sekta hizo kwa kuzingatia mahitaji halisi.

NBS pia inasema sensa hiyo itakusanya taarifa kuhusu takwimu na hali ya takwimu nchini.

Kwamba kupitia takwimu hizo, itasaidia serikali kujua mchango wa sekta katika pato la taifa, kupima mikakati yake ya kufikia Tanzania ya viwanda na inatoa fursa kwa wadau wengine kujua fursa na changamoto ya sekta hiyo.

Tunaunga mkono hatua hiyo, huku tukiishauri serikali kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu endelevu wa kufanya sensa ya sekta hizo kwa wakati mwafaka ili kuwa na takwimu za kisasa, hivyo kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzitafutia ufumbuzi haraka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Serikali iwezeshe vyama ushirika kununua mazao ya wakulima

**NILITAKA** nisiendeleze ajenda ya kusuasua kwa ununuzi wa pamba ya wakulima wiki hii, nikiwa na imani kwamba suluhisho lake lingemalizwa kesho kutwa, siku ya Nanenane na Rais John Magufuli mkoani Simiyu.

Rais Magufuli anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha Maonyesho na Maadhimisho ya Nanenane mwaka huu, yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyakabindi, wilayani Bariadi mkoani Simiyu, moja ya mikoa inayolima kwa wingi zao la pamba.

Nilitaka nisizungumzie lolote juu ya kadhia hiyo kwa wiki hii ili nikiwa na imani kwamba kuna ambacho atasema juu ya kero hii ambayo bado ni adha kwa wakulima ambao hawajalipwa fedha baada ya kuuza pamba yao.

Lakini si kwa hao tu ambao tayari wameshauza pamba yao ambayo bado imehifadhiwa kwenye maghala ya Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), pia kwa wakulima ambao bado hawajaiuza kabisa.

Kuna wakulima wengi wenye pamba majumbani, wakisubiri iliyo tayari kwenye maghala ya AMCOS isafirishwe, ili nafasi ipatikane ya kuhifadhi pamba nyingine na fedha za kutosha zipelekwe.

Hata hivyo, Muungwana amelazimika aendeleze ajenda hii ya kusuasua ununuzi wa zao hili, akichagizwa na hatua ya serikali kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ya kuendelea kulishughulikia kwa dhati suala hili.

Ikumbukwe kuwa tangu msimu wa uuzaji wa zao hili ulipoanza Mei 2, mwaka huu, serikali imekuwa ikichukua kila jitihada za kuhakikisha wakulima wanauza pamba yao, tena kwa bei yenye tija.

Ilichukua hatua ya kusimamia bila ya 'kupepesa macho' bei elekezi ya Sh. 1,200 kwa kilo kinyume na zilizokuwa zinatolewa na wanunuzi binafsi za kati ya Sh. 500 hadi Sh. 800 kwa kilo.

Lakini ikatoa pia dhamana kwenye benki mbalimbali kuwezesha kampuni za ununuzi kukopa fedha ili zinunue pamba ya wakulima.

Hatua hiyo ilifuatia madai ya kampuni za ununuzi kwamba benki zinasita kutoa mikopo kwao kwa madai kuwa bei ya pamba kwenye soko la dunia imeshuka na hivyo kukosekana uhakika wa mikopo kurejeshwa.

Aidha, serikali ikatoa maelekezo ili kufikia Julai 30, pamba yote iwe imenunuliwa kutoka kwa wakulima, ingawaje elekezo hili halikutekelezwa ipasavyo. Katika kuhakikisha suluhu ya changamoto hii inapatikana, wiki iliyopita Agosti 2, Waziri Mkuu alikutana kwa mara nyingine na wanunuzi wa pamba, wamiliki wa benki na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Vilevile Agosti 3, akazungumza na Wakuu wa Mikoa minane inayolima pamba ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera, Mara, Tabora na Singida, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB.

Katika mikutano hiyo, Majaliwa ameagiza benki zilizoko katika maeneo yanayolima pamba zihakikishe taratibu zimekamilika ili kampuni za ununuzi zipate mikopo na ununuzi uwe umeanza kwa nguvu kuanzia jana Jumatatu.

Ni bahati nzuri kwamba mikutano hiyo ya Majaliwa ilihudhuriwa pia na mwenyekiti wa wanunuzi wa zao hilo Christopher Gachuma, ambaye aliagizwa kuweka utaratibu madhubuti wa ufuatiliaji ili kujua kiasi cha pamba iliyonunuliwa, kutoka kwa nani na wapi.

Muungwana ana imani kwamba kwa agizo hili la sasa la serikali pamba yote ya wakulima itanunuliwa na hivyo kuondoa kero hiyo kwao.

Pamoja na juhudi hizo zote za serikali, Muungwana anaona wakati umefika sasa kwa serikali kuwezesha vyama vya ushirika vya mikoa kushiriki kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima ili kuepusha adha kama hizi zinazoendelea kwenye zao la pamba.

Anasema hivyo kutokana na somo lililopatikana kwenye kadhia ya zao la korosho na sasa pamba.

Kwamba hata kama wanunuzi binafsi wataendelea kuwapo, lakini hatua hiyo itatoa uhakika wa mazao ya wakulima kununuliwa kwa hali yoyote zikiwamo za wanunuzi binafsi kusuasua kama ilivyo sasa.

# Hii kero Mikese hadi lini?

***Ndugu Mhariri***

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je, kwa majibu haya kuna amani hapa?*


*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*

*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

***Ahsante ni sisi wanakitongoji, Ukomanga-Fulwe, Mikese***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Elimu hii ni msaada kwa watoto wa kike

**Na Sabato Kasika**

SUALA la mzunguko wa siku za hedhi kwa wanawake, ni jambo ambalo inasemekana huwa halizungumzwi hadharani katika jamii nyingi barani Afrika kutokana na imani za kidini na kitamaduni.

Katika mazingira hayo, inaelezwa kuwa hata ushiriki wa wanaume katika suala la hedhi kwa msichana nchini lina pande mbili, huku wakiwapo wanaounga mkono na wengine kupingana nayo na kuona ni jambo la siri.

Wakati wa maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama mwaka 2018, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ulikaririwa na vyombo vya habari ukisema, wasichana wanakosa masomo 50 kati ya 194 na vipindi 400 kati ya 1,552 kwa mwaka.

Sababu kubwa iliyotajwa ni suala la hedhi ambalo limekuwa likipigiwa kelele kwa muda mrefu na wadau mbalimbali wa elimu ambao baadhi yao wamefikia kampeni za kuchangisha fedha ili kununua taulo za kike.

Wakati kukiwa na kampeni za kuchangisha na kununua taulo hizo, wapo wadau wengine ambao sasa wanafundisha wanafunzi wa kike kutengeneza taulo za asili ili waweze kujihifadhi wawapo shuleni.

HakiElimu ndio wanaofundisha utengenezaji wa taulo hizo za asili kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na walianzia wilayani Masasi mkoani Mtwara tangu mwaka jana.

Hivyo ndivyo Ofisa Programu wa HakiElimu Alinanuswe Kasyele, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kwamba wamedhamiria kumsaidia mtoto wa kike kupunguza utoro shuleni wakati wa hedhi.

Wakati huo HakiElimu ilitarajia kufika katika halmashauri 22 na kwenye kila halmashauri ilichagua shule mbili za sekondari na msingi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kutengeneza taulo hizo.

Ingawa HakiElimu haikufafanua zaidi jinsi ya kutengeneza taulo hizo, lakini mjadala unaona elimu hiyo ni ya muhimu na inatakiwa kuenezwa nchi nzima ili kumwondolea usumbufu mtoto wa kike.

Ikumbukwe kuwa wazazi wengi vijijini hawana uwezo wa kununua taulo za kike, hivyo elimu ya kutengeneza taulo za asili ikienezwa nchini itakuwa umewapunguzia gharama hata wale wasio nacho.

Hatua hiyo inaweza kusaidia pia kuwashirikisha wazazi na walezi ili kuwasaidia watoto wa kike ambao wamekuwa hawahudhurii shule kwa baadhi ya siku kutokana na hedhi.

Ingawa inasemekana bado kuna watoto wa kike wanaokwama kwenda shule kwa sababu ya hedhi, wadau wasikate tamaa, waendelee na kampeni na harakati za kumsaidia mtoto wa kike.

Kuendeshwa kwa mafunzo ya kutengeneza taulo za asili kuwe chachu ya kuongeza kasi ya kampeni kama ambavyo East Africa Television imekuwa ikifanya kupitia kampeni yake ya 'Namthamini'.

Suala la hedhi ni la kawaida kwa watoto wa kike (wasichana), ambalo huwatokea kila mwezi kutokana na mfumo wa uzazi, ambao wakati mwingine baadhi yao hushindwa kwenda shule kwa kukosa taulo za kujihifadhi.

Mjadala huu unatambua kampeni zinazofanywa wadau mbalimbali wa elimu za kuchangisha fedha au kununua taulo hizo na kuzigawa kwa wanafunzi, katika shule mbalimbali nchini.

Unatambua kuwa lengo kubwa ni kutaka kuwasaidia watoto wa kike waweze kuhudhuria shule kama kawaida hata wakati wakiwa katika hedhi kwa vile wanakuwa tayari na taulo za kuwahifadhi vizuri.

Kwa maana hiyo bado juhudi kubwa ziendelee kufanyika kwa kushirikisha wadau wa elimu wakiwamo wazazi na walezi ili kuwasaidia watoto wote wa kike nchini waondokane na adha hiyo, ambayo hukumbana nayo.

Kimsingi, watoto wa kike wanapokuwa katika hali kama hiyo hudharirika na kufadhaika, wanakosa namna bora, yenye heshima na staha katika kujistiri na wakati mwingine wanashindwa hata kusaidia kazi nyumbani.

Wataalamu wa masuala ya afya, wanakumbusha kuwa matumizi ya taulo kiafya ni muhimu kwa vile humpa mwanamke fursa ya kutawala vizuri mazingira yanayomzunguka.

Vilevile hata kazi anazofanya na uwajibikaji mwingine wowote unaohitaji kuushughulisha mwili wake, hivyo suala la taulo za kike ni la muhimu kwa kila mwanamke wakiwamo wanafunzi.

Kwamba hedhi huwanyima fursa wasichana kuhudhuria vipindi muhimu darasani na hivyo kuwa na athari kwa namna moja au nyingine na mafanikio yao ya kielimu.

Tatizo kubwa zaidi kuhusiana na taulo hizo lipo vijijini ambako ndiko waliko Watanzania wengi wenye kipato cha chini, hivyo bado kuna haja kubwa ya elimu ya mafunzo ya kutengeneza taulo za asili kufikishwa huko.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



HABARI KITAIFA

# Mwandishi kortini tuhuma makosa yasiyodhaminika

INATOKA UK 2

Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi maarufu kama 'Mahakama ya Mafisadi'.

Kadushi alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kwamba upande wa Jamhuri uliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Jopo la utetezi likiongozwa na mawakili, Jebra Kambole, Reginald Martin, John Mallya na Benedict Ishabakaki, lilidai halina pingamizi kwa kuwa kesi hiyo haina dhamana waliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Mshtakiwa alitakiwa kupelekwa mahabusu mpaka Agosti 19, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.

Zitto alionekana akibubujikwa na machozi huku baadhi ya ndugu nao wakiangua kilio kwa uchungu baada ya mahakama kuamuru apelekwe mahabusu kwa kuwa mashtaka yanayomkabili hayana dhamana.

Wakati huohuo, jopo la Mawakili wa Utetezi liliiomba mahakama hiyo kuyaondoa maombi ya dhamana yaliyofunguliwa wiki iliyopita dhidi ya DPP.

Kambole alidai kuwa kwa kuwa maombi hayo yalikuwa yanahusu mshtakiwa kuachiwa kwa dhamana au kufikishwa mahakamani kwa sasa hayana nguvu, aliomba kuyaondoa.

"Mheshimiwa kwa kuwa mshtakiwa amefikishwa mahakamani na mashtaka yanayomkabili hayana dhamana tunaomba kuyaondoa maombi ya dhamana," alidai Kambole.

Kadushi alidai kuwa upande wa Jamhuri hauna pingamizi na kuondolewa kwa maombi hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, Majura Kasika (kulia), akishiriki katika uvunaji wa pamba shambani kwake wilayani humo juzi, huku akisaidiwa mkazi wa kijiji cha Mchangani, Meshack Majebere. Msimu wa zao hilo kwa mwaka huu umeanza. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waziri ataka mazingira bora uwekezaji SADC

INATOKA UK 2

na kahawa, bidhaa za viwandani kama vile plastiki, tumbaku, saruji, marumaru, dawa na vifaa tiba.

Alisema bidhaa ambazo Tanzania inanunua kwa wingi kutoka nchi za SADC zinahusisha magari, mbegu za mahindi, gesi, mabati, vilainishi, bia na sukari.

Alisema bidhaa hizo zaidi zinatoka katika nchi za Afrika Kusini, Zambia, Mauritius na Malawi.

Alisema Tanzania pia inanufaika na miradi mbalimbali ya ushirikiano inayotekelezwa katika nchi za SADC hususan miradi inayounganisha nchi jirani.

Aliitaja kuwa ni pamoja na mradi wa vituo vya pamoja vya forodha vya mpakani kati ya Tanzania na Zambia (Tunduma) na kati ya Tanzania na Malawi (Nakonde) na mradi wa maendeleo ya maji na uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe.

Waziri wa Viwanda na Biashara Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Amina Ally, alisema serikali ya awamu ya tano imekuwa ikifanya kazi kubwa kuwaletea maendeleo wananchi, hasa katika kuimarisha miundombinu.

"Tunakupongeza Rais Magufuli kwa uthubutu wa kuendeleza kile kilichoanzishwa na Mwalimu Nyerere kwa kuendeleza bwawa la kufua umeme kwa manufaa ya Watanzania na nje ya Tanzania," alisema.

Katibu Mtendaji wa SADC (Dk. Taxe) alisema uendelezaji wa viwanda unahitaji mambo mengi ikiwamo umeme wa uhakika na wa gharama nafuu.

"Huwezi kuwa na viwanda kama huna umeme unaozalisha kwa urahisi na unafuu, kuwa na umeme unaotakiwa ni kitu cha muhimu sana, pongezi kwa Rais Magufuli na Serikali ya Tanzania kwa kuona umuhimu wa umeme na kuendelea na mradi wa Mto Rufiji," alisema.

Kiongozi huyo wa SADC aliwataka Watanzania kutumia fursa zilizoko kwenye soko la SADC linalojumuisha nchi 16, zenye watu wapatao milioni 344.

Mwenyekiti wa Baraza la Biashara wa SADC, Charity Mwiya kutoka Namibia, alisema wanawake wanapaswa kujengewa mazingira wezeshi ili kupata fursa ikiwamo kufanya biashara.

"Nimeangalia katika orodha ya watoa mada wengi ni wanaume, ila natambua kwamba wengi wao wapo huko kwenye mabanda wakionyesha bidhaa mbalimbali, mimi ni mwanamke wa kwanza kuwa mwenyekiti wa kamati hii, naelewa hali ilivyo," alisema.

# Nyundo 6 za JPM viwanda SADC

INATOKA UK 2

"Sekta ya viwanda ni muhimili muhimu kwa maendeleo ya taifa lolote, ni muhimu kukuza uchumi, kupambana na umaskini na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira, ndivyo vilivyochochea ukuaji wa uchumi na kuyaletea maendeleo ya mataifa makubwa," alisema.

Alisema miaka ya hivi karibuni nchi za Asia ambazo kwa miaka ya 60 na 70 zilikuwa na viwango vinavyoshabihiana kimaendeleo na Afrika, lakini zimepiga hatua kubwa kimaendeleo kupitia viwanda.

Rais Magufuli alisema Afrika inasafirisha malighafi badala ya bidhaa kamili ikilinganishwa na mabara mengine na kwamba wanunuzi wa bidhaa ghafi ndiyo waamuzi wa bei kwa kuwa wasiponunua Afrika hakuna pa kuzipeleka.

"Mwenendo huu umewadidimiza wakulima kutokana na kutotabirika kwa bei, nchi za Afrika zinaongoza kuagiza bidhaa za viwandani kutoka nje ambazo zinatokana na malighafi zetu, huuzwa bei kubwa na waamuzi wa bei ndiyo wanunuzi wa malighafi, sisi hatuna nguvu ya kupanga bei ya mazao ghafi yetu wala bei ya bidhaa tunayoagiza kutoka nje," alisema.

"Urari wa biashara kati ya Afrika na mataifa mengine umekuwa siyo mzuri, kati ya Afrika na Umoja wa Ulaya ilikuwa Euro bilioni 280, lakini tulinunua bidhaa za Euro bilioni 149 na tukawauza bidhaa zenye thamani ya Euro 131, asilimia 60 ya bidhaa zilikuwa ghafi ambazo thamani yake ni ndogo," alisema.

# Kesi ya kina Mbowe siku tano mfululizo

INATOKA UK 3

kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi, kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano wa hadhara mshtakiwa Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano...watu wanapotea... watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome...," alinukuliwa na kudaiwa kuwa maneno yaliyoelekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.



# Spika Ndugai ataka uzazi wa kiuchumi

INATOKA UK 3

jukumu lake la kuishauri serikali kuhusu sera mbalimbali zitakazowezesha watu kuishi miaka mingi na kuwa nchi yenye uchumi imara.

Mwenyekiti wa Chama cha Kibunge Kinachoshughulikia na Idadi ya Watu na Maendeleo, Jamal Kassim, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu na kukabiliana na changamoto za idadi ya watu na uchumi.

Alisema kupitia mkutano huo, wabunge watabadilishana uzoefu na kueleza juhudi za serikali katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini.

Mbunge wa Viti Maalum, Suzan Lyimo (Chadema), alisema inafahamika duniani kote kuwa idadi ya watu ikiwa kubwa, eneo la ardhi nalo linakuwa dogo, hivyo kufifisha uchumi.

Alisema lengo la serikali na mpango huo ni kutaka kuona idadi ya watu inaenda sambamba na rasilimali za taifa zilizopo ili kuwa na uchumi imara.

## HABARI KITAIFA

# Hospitali zote rufani kujengewa majengo ya dharura, mahututi

**Na Dege Masoli,** TANGA

HOSPITALI 28 za serikali za rufani nchini zitajengwa majengo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma za dharura na mahututi ili kukabiliana na changamoto ya vifo vinavyotokana na kutokuwapo kwa huduma hiyo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Wazee na Watoto, Ummy Mwaimu, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua jengo la huduma za dharura (EMD) na mahututi (ICU) la Hospitali ya Rufani ya Bombo Mkoa wa Tanga.

Ummy alieleza kuwa lengo la serikali ni kupunguza vifo kwa asilimia 40 vinavyotokana na kukosekana kwa huduma hiyo kwa watu wanaohitaji katika hospitali hizo, na kwamba serikali imeona umuhimu wa kujenga vitengo hivyo maalumu kwa ajili ya dharura na wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu.

Alisema mpango huo umeanza, na kwamba Hospitali ya Bombo imebahatika kuwa ya kwanza kufikiwa na mkakati huo.

**Mpango wa serikali ni kujenga majengo manne ya huduma za dharura na mahututi kwa kila mwaka kuanzia mwakani ili kuifikisha haraka huduma hiyo kwa wananchi.**

Hata hivyo, alibainisha kuwa huduma hiyo itawekwa kwenye hospitali zote za rufani zilizopo katika mikoa yote nchini.

Alieleza kuwa utafiti uliyofanywa wa kitaalamu umeonyesha kuwa huduma hiyo imepunguza vifo vya watu wanaohitaji kuipata kwa asilimia 40, na kwamba lengo ni kuendelea kupunguza kama siyo kumaliza kabisa tatizo hilo.

"Mpango wa serikali ni kujenga majengo manne ya huduma za dharura na mahututi kwa kila mwaka kuanzia mwakani ili kuifikisha haraka huduma hiyo kwa wananchi," alieleza Waziri Ummy na kuongeza kuwa:

"Bombo sasa ina uwezo wa kuwahudumia wagonjwa 12 wenye uhitaji wa huduma ya ICU kwa wakati mmoja."

Ummy alieleza kipaumbele cha serikali katika kufanikisha mpango huo kuwa ni kuhakikisha utekelezwaji wa kuwapo madaktari bingwa wa vitengo vya kuhudumia magonjwa mbalimbali katika hospitali hizo.

Ummy alimshukuru Makamu wa Rais wa Shirika la Abbot Fund Tanzania, Addy Wilson, kutokana na shirika hilo linavyojitolea kusaidia changamoto mbalimbali za kijamii, na kwamba kufanya hivyo ni kuunga mkono serikali.

Awali akisoma taarifa fupi kwa waziri huyo, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Bombo, Dk. Jumanne Karia, alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana, lakini alimweleza pia changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo ikiwamo uhaba wa watumishi na uchakavu wa miundombinu ya majengo.

Dk. Karia alitaja changamoto nyingine ni uhaba wa vitanda ambapo alisema vilivyopo ni 445 wakati uhitaji ni 600, uhaba wa vifaa kwa ajili ya kufanyia uchunguzi na kushukuru serikali kwa kutoa kibali cha kuajiri watumishi 62, na kwamba hilo litapunguza upungufu huo.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (mwenye kofia), akiangalia namna msikiti wa kale wa Songomnara, uliyojengwa uliopo katika orodha ya urithi wa utamaduni, wakati alipotembelea eneo hilo, katika Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi jana, kwa ajili ya kuangalia namna ya kuboresha miundombinu ili watalii waweze kutembelea. **PICHA: WMU**

# Wakulima wapewa siri dawa ya tembo waharibifu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAKULIMA waishio katika maeneo ambayo yamekuwa yakivamiwa na tembo wameshauri kutumia nyuki kudhibiti wanyama hao.

Aidha, wakulima hao wameshauriwa kutumia nyuki ili wanufaike na biashara ya asali.

Ofisa Uhifadhi wa Taasisi ya Friedkin Conservation Fund (FCF), Julius Robinson, ndiye aliyewapa siri hiyo wakulima jana wakati akizungumza nao katika banda la taasisi hiyo, katika maonesho ya Nanenane kitaifa kwenye viwanja vya Vyakabindi wilayani Bariadi Mkoa wa Simiyu.

Robinson alisema nyuki wana faida kubwa kama wakitumiwa vizuri na wafugaji, hasa katika udhibiti wa tembo na kupata asali kwa takriban mwaka mzima.

"Kutokana na umuhimu wa nyuki, FCF tumekuwa na mradi wa kuwapa mizinga ya kibiashara wananchi wanaoishi wilayani Meatu, ambapo taasisi hii imewekeza katika shughuli za utalii wa picha na uwindaji kupitia kampuni ya Mwiba Holding na nyingine," alisema.

Alisema hadi sasa mizinga zaidi ya 100 imetolewa kwa vikundi vya ufugaji nyuki, wilayani Meatu mkoa wa Simiyu na sasa vinapata asali, na kwamba mazao yao hayavamiwi tena na tembo.

Ofisa nyuki wa wilaya ya Serengeti mkoani Mara, Fares Mwacha, alisema mizinga ambayo inatolewa na FCF ni rafiki kwa ufugaji wa nyuki na mfugaji anaweza kuvuna asali mwaka mzima bila nyuki kuhama katika eneo lake.

"Hii mizinga ni ya kisasa na unaweza kuvuna asali bila kuua nyuki ama nyuki kuhama, lakini pia unaweza kuwatumia nyuki kuzuia wanyama kama tembo kuvamia shamba lako," alisema.

John Masunga, mkazi wa Meatu Kijiji cha Makao, alieleza kuwa tangu wameanza kutumia mizinga hiyo, wamekuwa wakivuna asali, lakini pia wanadhibiti tembo, kutokana na kuweka mizinga pembezoni mwa mashamba yao.

# Wanufaika wa Tasaf wenye nguvu watakiwa kufanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, amewataka wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambao wana nguvu za kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo wafanye hivyo, ili waweze kujiingizia kipato badala ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini kupitia Tasaf.

Dk. Mwanjelwa alitoa maagizo hayo alipokuwa akizungumza na wananchi na walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini katika vijiji vya Lukindo na Burugo, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera.

Alisema utawekwa utaratibu maalum ambao kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi ambaye yuko kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini afanye hivyo na kulipwa ujira kutokana na kazi atakayoifanya.

"Ni wajibu wa walengwa wote wenye uwezo wa kufanya kazi ambao wako kwenye mpango huu, wafanye kazi badala ya kutegemea ruzuku ili nguvu kazi yao isipotee bure," Dk. Mwanjelwa alisisitiza.

Ameongeza kuwa, kufanya kazi kwa wanufaika hao ni sehemu ya kuwasaidia katika kuboresha maisha yao na kusisitiza kuwa ruzuku itabaki tu kwa wananchi wasioweza kufanya kazi ambao wengi wao ni wazee na watoto.

Aidha, Naibu Waziri huyo aliwataka wataalamu wa halmashauri za wilaya nchini kote kuhakikisha kuwa wanafanya ufuatiliaji wa karibu kwa wanufaika ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na tija kubwa.

Dk. Mwanjelwa anaendelea na ziara ya kikazi mkoani Kagera kukagua utekelezaji wa shughuli za Tasaf na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma katika halmashauri zote za mkoa huo ambapo tayari ameshatembelea Manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Bukoba Vijijini.

# Vyombo vya usafiri Ziwa Victoria vyakosa maboya

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

VYOMBO vya usafiri wa majini katika Ziwa Victoria vinakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na maboya, huku vilivyonavyo vikiwa katika mazingira yasiyo siyo.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, wakati akizungumza na waandishi wa habari ili kubainisha matokeo ya kile walichokibaini katika vyombo vinavyofanya shughuli za usafirishaji abiria na mizigo katika Ziwa Victoria wakati wa ziara iliyoanza Julai 29 mwaka huu mkoani Mwanza.

"Mimi na menejimenti yangu tupo Mwanza kwa ziara, tumetembelea vivuko vya Busisi, Luchelele na Kaunda ambapo tumegundua changamoto nyingi ikiwamo la vyombo vingi vya usafiri wa majini kutokuwa na maboya, huku viliyopo haviko katika mazingira rafiki na rahisi kufikika pale inapotokea hali ya hatari," alisema Ndomba.

Ndomba alisema, moja ya jukumu la TASAC ni kuhakikisha usalama wa vyombo vya usafiri majini vikiwa salama pamoja na kuwa na vifaa vya uokoaji inapotokea hali ya hatari yakiwamo maboya.

**Uelewa wa watu juu ya usalama wa vyombo vya usafiri pamoja na vifaa vya uokoaji ni mdogo kwani wengi wao hawajui namna ya kuvitumia, ikizingatiwa kuwa vyombo vingi havina maboya.**

"Uelewa wa watu juu ya usalama wa vyombo vya usafiri pamoja na vifaa vya uokoaji ni mdogo kwani wengi wao hawajui namna ya kuvitumia, ikizingatiwa kuwa vyombo vingi havina maboya," alisema Ndomba.

Ndomba alisema changamoto nyingine ni uwapo wa watu wanaofanya shughuli katika njia za vivuko na vyombo vya usafiri majini, ikiwamo wavuvi kutega nyavu zao, jambo ambalo ni hatari na linasababisha uharibifu, ajali na kinyume cha sheria.

"Pamoja na uwepo wa shughuli za wananchi kama vile wavuvi kutega nyavu zao katika njia zinazopita vivuko na matokeo yake zana hizo kujisokota na kuharibu, wakati serikali itumia fedha nyingi kutengeneza huku sheria ikielekeza kuwa ndani ya mita 100 pande zote hakupaswi kufanyika shughuli yoyote," alisema Ndomba.

Mwenyekiti wa Bodi ya TASAC, Prof. Thadeo Satta, akizungumza kwa niaba ya wajumbe wa bodi hiyo baada ya kutembelea na kukagua vivuko vya MV. Mwanza na MV. Misungwi vinavyotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Kigongo, wilayani Misungwi na Busisi, Sengerema, aliiagiza Temesa kwa kushirikiana na uongozi wa TASAC na vyombo vya usalama waunde kamati itakayoshughulikia utatuzi wa changamoto ya shughuli za uvuvi zinazofanyika kwenye njia za vivuko.

Pia kuielimisha jamii madhara yanayoweza kuathiri vyombo vya usafiri wa majini.

Awali Kaimu Meneja wa Temesa Mkoa wa Mwanza, Abdallah Atiki, alisema wanakabiliwa na changamoto ya watu binafsi kusafirisha abiria kwa kutumia mitumbwi na injini isiyo salama katika baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na vivuko vya Temesa, na pia wavuvi kuendesha shughuli zao (kutega nyavu) kwenye njia za vivuko.



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (kulia), akikabidhi sehemu ya mifuko 100 kwa Nyakiriga Kabende ambaye ni mwenyekiti wa kikundi cha kusimamia ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika vijiji vya Kigera Etuma na Kakisheri, mkoani humo juzi. **NA MPIGA PICHA WETU**

## Rukwa ina ziada ya chakula tani 470,794

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKOA wa Rukwa umesema una ziada ya chakula tani 470,793.6, baada ya msimu wa mavuno wa mwaka 2019, 2020, ambapo umefanikiwa kuvuna tani 884,368.8 ikiwa ni sawa na asilimia 69 ya mavuno yote.

Mkuu wa Mkoa huo, Joachim Wangabo, jana alibainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake wakati akiwatoa hofu wananchi wa mkoa huo kuhusiana na kuwapo kwa tishio la upungufu wa chakula katika baadhi ya mikoa nchini.

Alisema mkoa wa Rukwa unatarajia kutumia tani 413,575 kwa mwaka 2019, 2020 na kubakiwa na ziada hiyo, hivyo mkoa huo una chakula cha kutosha na hakuna hofu yoyote katika hilo.

Wangabo alisema hata hivyo, uzalishaji umeshuka kwani mkoa ulitarajia kupata chakula tani 1,677,474.8, lakini ulipata tani 1,164,242.42. Hata hivyo, pamoja na kutofikia lengo la uzalishaji kwa asilimia 100, lakini bado kuna ziada hiyo ya chakula.

Alisema serikali kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) imetoa fedha kwa ajili ya kununua tani 18,000 za chakula ambapo mkoa wa Rukwa utanunua tani 13,000 na katika mkoa wa Katavi utanunua tani 5,000 kwa ajili ya kuhifadhi.

Richard Luah, Ofisa Ugavi wa NFRA Mkoa wa Rukwa, alisema mwaka huu serikali itanunua kilo moja kwa Sh. 500, ambapo gunia la kilo 100 litanunulia kwa Sh. 50,000 bei ambayo itakuwa nzuri tofauti na walanguzi ambao wamekuwa wakiwalalia wakulima na kununua gunia hilo hadi shilingi 18,000.

Aliwaomba wakulima kuhakikisha wanazingatia ubora wa mazao hayo kwa kuwasafisha na kuyakausha vizuri sambamba na kuacha tabia ya kuchanganya na uchafu mwingine ili yawe mazito kwani wanaweza wasifanikiwe kuyauza hususani mahindi kutokana na kushindwa kukidhi ubora.

## Sababu kuendelea uvamizi, uharibifu wa tembo yatajwa

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, amesema uvamizi wa tembo katika mashamba ya wananchi utaongezeka katika kipindi hiki kutokana na serikali kuweka nguvu zaidi katika uhifadhi na ulinzi wa maliasili.

Kigwangalla alisema kuwa jitihada hizo za serikali zimesababisha kuongezeka kwa wanyama wakali na waharibifu kama tembo, viboko, pamoja na mamba huku maeneo yao yakiwa yamevamiwa na wananchi.

Waziri huyo alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu katika Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kitaifa baada ya kutembelea maonyesho hayo. Alisema kuwa katika miezi ya hivi karibuni wanyama wengi zaidi wanategemea kuvamia maeneo hayo na kuharibu mashamba ya watu pamoja na nyumba kutokana na kuongezeka kwa kiwango kikubwa hasa tembo.

Aidha, Dk. Kigwangala alisema uvamizi utaendelea kuwapo kutoka na wananchi kuvamia maeneo ya kingo za hifadhi, mazalia ya wanyama, shoroba, na kuendesha shughuli za kilimo, malisho pamoja na makazi.

"Wewe ukiweka shamba kwenye njia ya tembo yeye atapita tu, ukiweka makazi tembo atapita tu maana ni njia yake ya kila siku, kwa kweli tuna changamoto hiyo ndani ya serikali, na kwa miezi hii ya karibuni uvamizi utaongezeka," alisema Dk. Kigwangalla.

Alisema changamoto hiyo inaendelea kuisumbua wizara yake jinsi ya kupamba nayo, ambapo jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuweza kupambana na nayo.

"Hivi karibuni Rais alitoa maagizo juu ya kufanyika kwa tathmini ya maeneo ambayo wananchi waliyavamia na yalikuwa ya hifadhi mbalimbali na mapori ya akiba, bado tunasubiria maamuzi yake ambayo yanaweza kuwa suluhisho ya changamoto hii," alisema Kigwangalla.

Akizungumzia maonyesho hayo Waziri Kigwangalla aliupongeza mkoa wa Simiyu, Mara na Shinyanga kwa maandalizi mazuri na makubwa, huku akiwataka wananchi wa mikoa hiyo kujiletea maendeleo.

## RC ataka wakulima vijijini kupewa elimu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewataka wataalamu katika sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo, kuiga mfano kutoka katika Taasisi Pass kwa kuwafikia wakulima vijijini na kutoa elimu, mafunzo na utaalamu kwa wakulima kulima kilimo cha kisasa ili kuongeza wigo wa uzalishaji wa mazao.

Hayo aliyasema jana wakati wa uzinduzi wa Maonyesho ya 26 ya Nanenane Kanda ya Kaskazini, yaliyofanyika katika viwanja vya Themi, jijini Arusha.

Mghwira, alieleza kwamba Taasisi ya Pass imekuwa ikiwatembelea wakulima vijijini na kusikiliza changamoto zinazowakabili katika sekta hiyo, uvuvi na ufugaji na wamekuwa wakizitatua kwa wakati kuwapatia mikopo yenye riba nafuu, pembejeo za kilimo, vitendea kazi pamoja na kutoa elimu ya kulima kilimo chenye tija.

"Katika ziara zangu vijijini nimekuwa nikikutana na wataalamu wa Pass huko vijijini wakifanya kazi kweli wanastahili pongezi kwa mchango mkubwa wanaotoa katika sekta ya kilimo, biashara, uvuvi na umwagiliaji," alisema Mghwira.

Alisema, taasisi hiyo imekuwa ya mfano kwa kuwa inatoa mikopo yenye riba nafuu, pembejeo za kilimo na vitendea kazi vya kilimo pamoja na elimu kwa lengo la kuikuza sekta ya kilimo hapa nchini.

Vile vile, alisema changamoto inayoikabili serikali katika maonyesho ni maofisa ugani kuandaa maonyesho kwa mfumo wa kimaonyesho ambayo hayaendani na uhalisia wa mazao yanayozalishwa na wakulima vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Pass, Nicomed Bohay, alisema taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 2000 chini ya programu ya kusaidia sekta ya kilimo kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha na kibiashara kwa wajasiriamali wa bidhaa na huduma katika sekta ya kilimo.

Pia alisema hadi sasa watu wanaohudumiwa na taasisi hiyo ni wajasiriamali binafsi wa biashara za kilimo, vyama vya ushirika, makundi ya wakulima wadogo wadogo na kampuni zinazojihusisha na sekta ya kilimo.

Alisema hadi sasa wameshafanya kazi na benki 15 nchini na wamefanikiwa kuwafikia wajasiriamali wa kilimo 929,172 na kufaidika na mikopo iliyodhaminiwa na shirika hilo.

# TPRI kuelimisha wakulima umuhimu mbegu za asili

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KAIMU Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Chelestino Mofuga, ameishauri Taasisi ya Utafiti ya TPRI kujikita katika utoaji elimu kwa wakulima kuhusu kuboresha mbegu za asili ili kukwepa kemikali zinazosababishwa na mbegu za kisasa kwa kisingizio kuwa tunahitaji mavuno mengi.

Chelestino ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipowaongoza wakuu wa wilaya wenzake kutembelea mabanda ya wakulima, taasisi mbalimbali za umma na mashirika kwenye maonyesho ya bidhaa zinazozalishwa na teknolojia tofauti.

Alisema kwa sasa kwenye maduka mengi ya mbegu kuna mbegu za kisasa na hivyo kuzifanya mbegu za asili kupotea au kuzikuta kwenye mabanda ya maonyesho pekee na wananchi kuzisahau, wakati ni muhimu kuzifahamu ili waendelee kuzitumia.

**Kwa sasa mbegu nyingi zinazoonekana kwenye maduka ya mbegu ni za kisasa ambazo ni za nje na hivyo huenda mbegu za asili zikapotea kama wataalamu watashindwa kuzihifadhi.**

Vile vile, aliwataka TPRI kwa kutumia wataalamu wake kushuka ngazi za chini kuwafundisha matumizi ya mbegu za asili ambazo zinamanufaa makubwa kiafya tofauti na mbegu za kisasa ambazo zinaongeza kemikali nyingi kwenye miili ya watu na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani.

"Mimi ninaona kitengo cha mbegu za asili kiimarishwe na ikiwezekana ifanyike demonstrations farms (kilimo cha mfano) kwa wakulima huko chini kukusanya mbegu za asili katika maeneo mbalimbali na kuzihifadhi ili wakulima wapewe elimu kwa wingi namna gani zinafaa kutumiwa tofauti na hapo tutabaki kuzikusanya mbegu hizi kwenye majumba ya maonyesho kumbe na wakulima hawazijuwi tena namna ya kuzitumia," alisema Mofuga.

Alisema kwa sasa mbegu nyingi zinazoonekana kwenye maduka ya mbegu ni za kisasa ambazo ni za nje na hivyo huenda mbegu za asili zikapotea kama wataalamu watashindwa kuzihifadhi.

"Teknolojia ya matumizi ya kemikali inapoongezeka maisha ya kuishi yanapungua, kama tulikuwa tunaweza kuishi miaka 80 au 70 sasa inaendelea kushuka mtu ana uwezo wa kuishi miaka sasa 45 au miaka 50 badala ya kuishi miaka 80, we fikiria mfano mtaalamu tunamsomesha kwa gharama kubwa hadi awe profesa halafu taifa lije kumpoteza kwa sababu ya matumizi ya kemikali," alieleza.

Alisema kama wataalamu wa kudhibiti viuatilifu wa TPRI hawatachukua hatua za makusudi kuboresha mbegu za asili na kudhibiti matumizi makubwa ya kemikali, ambazo zinaongeza wagonjwa wa kansa, wataendelea kuwapoteza Watanzania na kiuchumi itakuwa ni hasara kubwa.

Alitoa mfano mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya kuwa wamekwishajisahau na kutumia viuatilifu vya kuulia magugu na kuacha kupalilia wenyewe huku akisema mkulima anaweza kuwa ekari 4,000, lakini zote anatumia sumu kupalilia, kitu ambacho anaona siyo kizuri kwa uhifadhi wa ardhi na kwa afya za wakulima na watumiaji wa mazao yatakayotokana na mbegu zilizopandwa hapo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula, aliwashauri wataalamu wa TPRI kuchukua hatua mapema za kudhibiti magonjwa mbalimbali hata kama hayajatokea nchini ilimradi wamepata taarifa yametokea katika Bara la Afrika.

Ofisa Utafiti wa TPRI, Dk. Mujuni Sospeter, alisema kuna changamoto za uingizwaji wa mbegu za chotara ambazo wakulima wengi wanazikimbilia, kutokana na uzalishaji wake kuwa mwingi na wakulima wakiulizwa wanasema ladha ya mbegu za asili bado haipo kwenye mbegu chotara hivyo mbegu za asili bado inahitajika.

Katika kuhakikisha mbegu hizo zinahifadhiwa alisema wana sampuli 6,000 za mbegu za asili, ambazo zipo kwenye benki ya kuhifadhi mbegu za asili kwa ajili ya kuziendeleza kwa manufaa ya watumiaji mbalimbali.




Mkuu wa kitengo cha unyunyuziaji wa viuatilifu vya kuulia wadudu kutoka Taasisi ya Utafiti na Udhibiti wa Viuatilifu ukanda wa Kitropiki (TPRI), Julius Mkenda, akitoa elimu kwa wakulima waliotembelea banda lao, katika maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya Themi Njiro, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mbunge apania kumaliza changamoto shuleni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MBUNGE wa Jimbo la Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, ameahidi kushiriki ujenzi wa jiko na bwalo la chakula la Shule ya Sekondari Leguruki, ambayo ni pekee inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha.


Mbunge huyo ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya Juma la Jumuiya ya Wazazi mkoa huo, ambayo yalifanyika jana kwenye viwanja vya shule hiyo, wilayani Arumeru, alisema anatambua changamoto inayoikabili shule hiyo ambayo ni jiko na bwalo la chakula hivyo anajipanga kuitatua.

Alisema atashirikiana na uongozi wa shule pamoja na wazazi wa watoto wa shule hiyo kuhakikisha majengo hayo yanakamilika ndani ya muda mfupi na kuwezesha wanafunzi kupata huduma stahiki ili kuongeza ufaulu kwenye masomo yao.

Dk. Pallangyo ambaye pia ni Mwenyekiti mstaafu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, aliwataka wanafunzi na walimu wa shule hiyo, kuongeza bidii ili yapatikane matokeo mazuri na kuifanya shule hiyo iwe miongoni mwa shule bora nchini zenye matokeo mazuri ya kidato cha nne na sita.

Alisema kuanzia mwaka huu hataki kusikia shule hiyo inakuwa na matokeo mabovu, bali iwe ni miongoni mwa shule zinazoongoza kwa kuwa walimu wapo, wanafunzi wapo na vifaa vyote vipo, hivyo haoni kwa nini isiwe na matokeo mazuri. Aliwataka wanafunzi hao kutambua kuwa wameenda shuleni kusoma na sio kucheza disko na wakifanya vizuri wataipatia soko shule hiyo.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Hezron Mbise, alisema kwenye maadhimisho hayo, ambayo yalizinduliwa wilayani Monduli wiki iliyokwisha, wamepokea mizinga 50 ya nyuki, kutoka makao makuu ya Jumuiya hiyo, pamoja na wadau ambayo itagawanywa kwa wilaya zote saba za mkoa huo, kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kiuchumi .





# Semakafu azipa mbinu shule 24 za sekondari

**Na Godfrey Mushi,** HAI

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu, amezitaka shule 24 za sekondari nchini zinazoshiriki programu za mabadilishano ya wanafunzi, kukubaliana kwanza na wabia wanaotekeleza mpango huo kwa kuzitambua changamoto zinazojitokeza na kuzitatua.

Amezitaka shule hizo kabla ya kushiriki katika programu hiyo, kila shule kufanya makubaliano na mbia ambaye atashiriki naye kwenye mpango huo na kuweka malengo ambayo yanalenga kujifunza, lakini pia kuongeza ujuzi kwa wanafunzi.

Dk. Semakafu aliyasema hayo jana katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wakati akifungua kambi maalum ya shule za sekondari zinazoshiriki katika programu za mabadilishano ya wanafunzi chini ya Shirika la Tanzania Youth Coalition (TYC).

**Napenda nisisitize mwendelee kufuata sheria na taratibu mbalimbali zilizopo ili programu hizi ziwe na manufaa kwa wanafunzi kwani lengo la serikali ni kuhakikisha na kusimamia elimu bora.**

Dk. Semakafu aliwakilishwa na Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Nkwama.

"Napenda nisisitize mwendelee kufuata sheria na taratibu mbalimbali zilizopo ili programu hizi ziwe na manufaa kwa wanafunzi kwani lengo la serikali ni kuhakikisha na kusimamia elimu bora kwa kila mwanafunzi," alieleza Naibu Katibu Mkuu huyo.

Awali akizungumza kabla ya kufunguliwa kambi hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Youth Coalition, Lenin Kazoba, alisema mkutano huo unafanyika baada ya TYC mwaka jana kufanya zoezi la kuzitambua na kuainisha shule zote nchini zinazofanya programu ya mabadilishano ya wanafunzi.

Kwa mujibu wa Kazoba, katika zoezi hilo TYC iligundua kwamba hakuna utaratibu wala mwongozo mzuri wa mabadilishano, lakini pia kuna tatizo la ukosefu wa mtandao wa pamoja wa shule hizo na zile za nchini Ujerumani.

"Lengo la mkutano huu ni kuhamasisha shule tofauti kutoka ndani ya nchi na Afrika Mashariki ambazo zinafanya programu za mabadilishano na nchi ya Ujerumani kuweza kukutana na kuunda mtandao wa pamoja. Lakini pia mkutano huu utatoa fursa kwa shule ambazo zinatekeleza programu hii kujifunza na kubadilishana uzoefu juu ya changamoto na mafanikio ambayo wanayapitia kwenye utekelezaji wa mpango huu," alieleza Kazoba.

TYC ni muungano wa mashirika 120 yasiyo ya kiserikali na vikundi 149 vya uzalishaji mali vinavyofanya kazi na vijana nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Elizabeth Kitundu, akitoa maelekezo ya serikali kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Babati jana. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi wa mji huo, Fortunatus Fwema. **PICHA: GIFT THADEY**

# X-ray sasa yawaweka pamoja CCM na Chadema

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UKOSEFU wa mashine ya mionzi kidigitali yenye uwezo wa kupiga picha na kutoa majibu ndani ya dakika moja (X Ray) katika Kituo cha Afya cha Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, umeviweka pamoja Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), baada ya kujikuta vyote vikipaza sauti, vikiitaka serikali kugharamia ununuzi wa mtambo huo.

Meya wa Manispaa hiyo, Raymond Mboya (Chadema) na Diwani wa Kata ya Bomambuzi (CCM), Juma Raibu, kwa nyakati tofauti jana walikuwa wakiipigia chapuo kwa Wizara ya Afya, kukipatia kituo hicho mashine hiyo.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika eneo la Pasua Sokoni, Meya huyo aliiomba wizara hiyo kuangalia uwezekano wa kukisaidia kituo hicho cha afya kwa kuwa ndio kituo pekee ambacho kinahudumia idadi kubwa ya wagonjwa katika kata zaidi ya nne.

Mbali ya wagonjwa wa kawaida, kituo hicho kinahudumia zaidi ya wajawazito 100 wanaokwenda kujifungua kila mwezi.

Pia kituo hicho kinahudumia kata nyingine tofauti zikiwamo Kaloleni, Bomambuzi, Arusha Chini na maeneo ya ukanda wa tambarare wa Kiwanda cha Sukari cha TPC.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Bomambuzi, Juma Raibu, aliiomba serikali kujitosa kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo la ukosefu wa mashine ya X-ray, kwa kuwa wanaamini kama ikipatikana itapunguza muda wa wagonjwa kukaa muda mrefu hospitali za rufani za Mawenzi na KCMC kutafuta huduma.

Tayari kituo hicho kimepatiwa na serikali zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kupanua kituo hicho kiweze kutoa huduma ya upasuaji, jengo la kinamama la kijifungulia, na maabara ya kisasa.

# Watakaohamishwa kupisha reli wapewa neno la faraja

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

DIWANI wa Kata ya Bomambuzi (CCM) katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, ametoa kauli ya 'faraja' kwa wananchi wa kata hiyo, zaidi ya 200 waliokuwa katika hatari ya kuhamishwa katika makazi yao kupisha ujenzi wa reli ya kaskazini kwamba serikali imesitisha mpango huo.

Raibu aliwatoa wasiwasi wananchi hao jana, wakati alipopewa nafasi ya kuzungumza katika mkutano wa hadhara wa kuzungumza na wananchi ulioandaliwa na Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini (Chadema), Jaffary Michael.

Akiwa katika mkutano huo diwani huyo aliwaeleza wananchi wa mtaa wa relini kwamba serikali imesitisha mpango wa kubomoa nyumba zao zilizojengwa karibu na miundombinu ya reli.

"Uamuzi huo wa serikali umefikiwa, baada ya kufanya makubaliano na wananchi hao na kuridhia kuondoa kesi iliyokuwa mahakamani ya kupinga nyumba zao kubolewa ndani ya mwezi mmoja ili kupisha ujenzi wa reli ya kaskazini (Tanga, Kilimanjaro na Arusha)," alisema.

Alisema serikali imekubali itatafuta eneo jingine kwa ajili ya ujenzi wa reli na kuwaachia wakazi hao waendelee kuishi katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Mbunge Michael aliiomba serikali na hasa Wizara ya Fedha na Mipango kuisaidia Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kupata kibali cha kukopa zaidi ya Sh. bilioni 19 kutoka Benki ya Uwekezaji nchini (TIB) ili kukamilisha ujenzi wa kituo cha kimataifa cha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi cha Ngangamfumuni.

Alisema tayari Rais John Magufuli ameshatoa zaidi ya Sh. bilioni 9.2 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho na kwamba hadi kukamilika kinahitaji zaidi ya Sh. bilioni 28.

"Tunamwomba Rais Magufuli atupatie kibali cha kukopa ama atusaidia kiasi cha fedha kilichobaki ili tuweze kuendelea na ujenzi na usijefikia mkandarasi akaondoka ama kusimamisha ujenzi kutokana na kukosa fedha," alisema Japhary.

Alisema ujenzi wa kituo hicho cha kisasa ujenzi wake utakuwa ghorofa kuanzia chini ambapo kitakuwa na uwezo wa kuingiza gari kubwa zaidi ya 120 kwa wakati mmoja, maeneo maalumu ya kufanya biashara na hivyo kutoa ajira kwa wakazi wa Moshi.

"Huu mradi ni wa pekee endapo utakamilika kwani jinsi ulivyo unaweza kujiendesha na kulipa mkopo na kutoa faida kubwa kwa wakazi wa Moshi na halmashauri na serikali kuu," alisema Japhary, huku akiisisitiza serikali kufanya jitihada za makusudi kufanikisha mradi huo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 6, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 19



## Teknolojia inavyon'garisha utendaji Shirika la Posta

JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Mwanafunzi aliyefariki Madagascar kwa 'kufungua mlango wa ndege '



# SHERIA NDOGO NDOGO ZINAVYOTATUA UKATILI KWENYE MASOKO SHINYANGA

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# FAHAMU SHERIA YA MAKOSA YA MITANDAO




IGP Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

TEKNOLOJIA ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imekuja na mabadiliko katika maisha ya wanadamu.

Mawasiliano ya mtu na mtu, nchi na nchi, pamoja na nchi na watu yalikuwa yakifanyika zaidi kwa kutumia barua na njia kubwa ya kuwasilisha ilikuwa Posta.

Kwa mabadiliko haya ya TEHAMA yameathiri maisha ya mwanadamu moja kwa moja katika maeneo mbalimbali kama vile; mawasiliano, biashara, elimu, jamii na hata sheria kwa kutaja machache.

Idara ya sheria imeathiriwa na TEHAMA katika maeneo mawili ambayo ni Sheria zinazotoa tafsiri ya Makosa na adhabu pamoja na haki na eneo la pili ni Sheria zinazoelezea utaratibu wa kushughulikia makosa na adhabu pamoja na haki za kijinai.

Kabla ya mwaka 2015 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikuwa na sheria ya makosa ya mitandao inayozungumzia pande zote mbili za makosa na taratibu za kushughulikia.

Sehemu ya VI ya sheria ya kielektroniki na Posta Na: 03 ya 2010 imeelezea baadhi ya matendo ambayo yakitendeka yatakuwa ni makosa ya kimtandao pia kuna baadhi ya vifungu ambavyo vinatafsiri makosa katika sura na maeneo mbalimbali.

Kimsingi sheria hii imejikita sana katika kutoa leseni kwenye maeneo mbalimbali kama vile vifaa, watoa huduma za mawasiliano na maeneo mengine muhimu ikiwamo, radio, televisheni na posta.

Hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kuwa na Sheria Kamili ya Makosa ya Mitandao ambayo ilipewa jina la Sheria ya Makosa ya Mitandao Na: 14 ya 2015.

Sheria hii ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Aprili, 2015 na baadaye kusainiwa kuwa sheria na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya nne Dk. Jakaya Mrisho Kikwete Aprili 25, mwaka 2015 na sheria hii hatimaye ilianza kutumika rasmi Septemba Mosi 2015.

Sheria hii ya Makosa ya Mitandao Na: 14 ya 2015 imelenga kutumika Tanzania Bara na Zanzibar, isipokuwa kwa Kifungu cha 50 ambacho kinazungumzia kufifilisha kosa, kifungu hicho kinasema;

"Bila ya kuathiri sheria nyingine inayotumika Tanzania Bara, Mkurugenzi wa Mashtaka, anaweza, muda wowote kabla ya mwenendo wa Mahakama kuanza na kwa kuzingatia tamko la kukiri kosa kwa hiari la mshtakiwa anaweza kufifilisha kosa na kuamuru mtu huyo alipe kiasi cha pesa atakachokitaja ambacho hakitazidi kiasi cha faini kwa kosa lolote hilo."

Malengo ya sheria hii kama yalivyoainishwa na sheria yenyewe ni; kuainisha makosa yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kuainisha utaratibu wa upelelezi, ukusanyaji na matumizi ya ushahidi wa kielektroniki na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha, sheria hii imegawanyika katika maeneo sita (06) ambayo ni; Kifungu cha 1-3 ni masharti ya Utangulizi, kifungu cha 4-29 Makosa na adhabu, kifungu cha 30 Mamlaka ya Mahakama, kifungu cha 31-38 kanuni za upekuzi na ukamataji, kifungu cha 39-46 wajibu wa watoa huduma, kifungu cha 47-51 Masharti ya jumla.

Hata hivyo, katika sheria hii kifungu cha 52-59 vinazungumzia mabadiliko ya sheria mbalimbali ambazo ni Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki Na: 03 ya 2010, Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Sheria ya Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 na Sheria ya Kurudisha Watuhumiwa, Sura ya 368.

**Imetolewa :-**
**Ofisi ya Uhusiano**
**Makao Makuu ya Polisi**
**Dar es Salaam.**



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Visawe, vitawe na vitate ni nini?

VISAWE ni maneno yenye maana zinazokaribiana. Kwa mfano, 'mtoto' na 'mwana' humaanisha kitu kimoja. Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21 (Uk. wa 577), visawe hutumika ili kuwasilisha dhana ileile iliyokusudiwa bila kubadilisha maana. Hivyo Visawe hupamba lugha ama katika mazungumzo au katika uandishi wa aina mbalimbali.

Mifano ya visawe: Afya: siha, zihi, rai, nguvu, uzima. Aibu: haya, tahayuri, soni. Alama: doa, ishara, dalili, taashira. Anza: takadamu, amiri, tangulia. Apiza: laani, duia. Arbuni: kishanzu, advansi. Athari: dosari, doa, kasoro.

Bahili: mchoyo. Baradhuli: zuzu, zuge, bwege, juha, jura, jinga. Baraste: barabara, tariki. Busara: hekima, akili, tabasuri. Chelewa: kawia, limatia, faitika, taahari, ahirika. Cheo: mamlaka, dhima, madaraka, wadhifa. Daawa: kesi, mashtaka. Daktari: tabibu, mhazigi, mganga. Duni: dhalili, hafifu, nyonge.

Fadhili: wema, hisani, ukarimu. Fikiri: waza, dhani, tafakari. Fuvu: bufuu, fuu. Kapera: mseja, mhuni. Kasoro: hitilafu, walakini, doa, taksiri. Kera: udhi, kirihi. Kibahaluli: kibatari, koroboi. Kimetameta: kimulimuli. Kuwadi: kijumbe, gambera, mtalaleshi, kibirikizi.

Laghai: danganya, nyenga, ongopa. Matata: chachawizo, ghasia, fujo, sokomoko, ugomvi, kimondo. Mauzauza: kiinimacho, mizungu, mazingaombwe. Mnadi: dalali. Mnyama: hayawani. Mpagazi: hamali, mchukuzi. Mpelelezi: jasusi, kachero, mdadisi. Msichana: banati, binti, mwari. Mtu: mja, adinasi, mwanadamu, mahuluki. Mvulana: ghulamu, janadume, barobaro. Mwizi: pwagu, pwaguzi, mdokozi. Nasa: kamata, nata, gwia. Ndoa: nikahi, harusi. Rafiki: sahibu, somo. Rika: umri, hirimu, umri unaolingana. Shabihi: fanana, landana. Shamba: konde, mgunda. Simanzi: majonzi, jitimai, ukiwa, huzuni. Stadi: bingwa, farsi, mweledi, gwiji, mtaalamu. Taabika: sumbuka, hangaika, dhikika. Taadhima: heshima, adabu, tasfida.

Uchawi: juju, sihiri, ulozi. Ugali: sima. Ugonjwa: maradhi, uwele. Ukuta: kiambaza. Uliza: saili, hoji. Wajihi: sura, uso. Weweseka: hohosa, babaika, kiakia, hangaika, riaria. Wia: dai, kitendo cha kutoka mahali fulani, kitendo cha jambo kuwa zito kutokea: imeniwia vigumu kuja. Wia radhi: kitendo cha mtu kuomba msamaha; alimwambia amwie radhi, akamsamehe.

Maneno yaliyo kwenye vitawe na vitate yataelezwa kwenye matoleo yajayo. Hapana shaka ufafanuzi wa maneno haya yatawasaidia sana waandishi na wasomaji wanaotumia maneno ya vijiweni/mitaani yaliyo kinyume cha ufasaha wa lugha ya Kiswahili kama ilivyo hapa chini:

"Stars, Harambee hainaga" ni kichwa cha habari ya gazeti la michezo. Kichwa hicho kina makosa mawili: Kiswahili hakina neno 'hainaga' ingawa siku hizi neno hilo hutumiwa sana mitaani. Kichwa cha habari yenyewe hakikukamilika! Hakielezi Stars, Harambee 'hazina' kitu gani!

Neno '...ga' limezoeleka sana mkoani Mwanza: 'nakwendaga' badala ya huenda, hula, hulala, huimba, husema (mara kwa mara) badala ya nakwendaga, nakulaga, nalalaga, naimbaga, nasemaga maneno ambayo si Kiswahili sahihi. Hali ilivyo sasa nadhani kuna wakati tutasema 'fyombo fyangu' (Wanyakyusa) badala ya vyombo vyangu; 'ndisi mbifu,' 'ukali' (Wachaga) badala ya ndizi mbivu, ugali.

Aidha kuna maneno yanayotumiwa tofauti na maana yake halisi. Kwa mfano siku hizi pilipilimboga zaitwa 'hoho' au 'pilipilihoho!' Pilipilimboga ni pilipili kubwa yenye rangi ya kijani, manjano au nyekundu isiyowasha, aghalabu hutumika kwenye kachumbari au kiungo kwenye upishi. 'Hoho' au 'pilipilihoho' ni ndogo nyembamba, nyekundu inapoiva na huwasha sana. Kwa ukali wake, huitwa pilipili kichaa. Husaidia kutibu kideri, ugonjwa wa kuku wa kuhara na kukohoa.

"Stars, Congo kwa viatu hatari" ni kichwa cha habari kwenye moja ya magazeti yetu ya michezo. 'Kiatu' ni kitu kinachovaliwa miguuni ambacho hutengenezwa kwa ngozi, plastiki n.k. na wingi wake ni 'viatu.'

Hapa "Stars, Congo kwa viatu hatari" haieleweki ila mpaka usome habari yenyewe ndio utagundua kuwa timu za Taifa Stars (Tanzania) na DR Congo ndizo zilizocheza rafu nyingi kuliko timu zingine zilizoshiriki michuano ya AFCON 2019. Kichwa kingine kwenye gazeti hilohilo: "Couple matata inayopiga pesa." Neno 'couple' si Kiswahili bali ni Kiingereza na maana yake ni vitu au watu wawili wanaohusiana kama vile mtu na mkewe, wachumba au maharusi. 'Matata' ni hali ya kugombana inayozuka miongoni mwa watu; ukorofi, mtu mwenye tabia ya ugomvi.

'Piga' ni kitendo cha kuadhibu kwa kugonga mwili kwa kitu kinachoumiza; kitendo cha kugonga kitu kwa kitu kingine kwa makusudi. 'Pesa' ni fedha. Sasa tusome kichwa kilichoandikwa: "Couple matata inayopiga pesa." Ni wasomaji wangapi waungwana wanaoelewa?

Magazeti yetu ya michezo huandika mambo ya ajabu ajabu sana. "Diamond amkana Tanasha buana!" Yaelekea neno la mwisho 'limepasishwa' kuwa badala ya neno halisi (bwana) huku wengine wakiandika 'bana!'

Mshangao mwingine kwenye gazeti hilo ni baada ya kusoma kichwa cha habari husika yenye paragrafu 8 na mwisho wa habari hiyo kukiwa na picha ya Guardiola, kocha wa mabingwa wa Uingereza kwa mara ya pili mfululizo. Kichwa cha habari kimeandikwa kwa herufi kubwa: "GUARDIOLA ASEMA ANARUDI BARCELONA"

Ingawa kichwa cha habari hiyo kimemtaja Guardiola kusema anarudi Barcelona na picha yake kuwekwa mwisho wa habari hiyo akiwa kajikunyata, hakuna paragrafu yoyote kati ya 8 iliyoandikwa Guardiola anarudi Barcelona!

***Methali: Werevu mwingi mbele kiza.***

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

NA JOSEPH MUHOZI

# Mfumo wa PSGP waimarisha upatikanaji taarifa za walengwa

- Unatambua, kutunza taarifa za mienendo ya wafanyakazi kampuni binafsi za ulinzi
- Ni teknolojia inayofichua tabia na sifa za mlinzi

KABLA haijasikika nyundo ya Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Moshi, maelezo ya awali ya mwenendo wa kesi kufikia uamuzi yalizidi kuunyong'onyeza moyo wa mama aliyekuwa ndani ya ukumbi wa chombo hicho cha kutoa haki.

Macho yake yalimkazia mtu aliyesimama kizimbani, asiamini jinsi alivyobadilika kutoka kuwa mlinzi wa mwanaye hadi kuwa muuaji katili wa mwanaye kipenzi, Humprey Makundi.

Lakini yote yakahitimishwa na sauti ya Jaji Firmin Matogolo iliyotaja adhabu ya kunyongwa hadi kufa kwa Hamisi Chacha, aliyekuwa mlinzi wa shule ya sekondari ya Scolastica ambaye sasa anatajwa kuwa muuaji wa aliyepaswa kumlinda.

Tukio hili ni king'ora (alarm) cha kutuamsha wote usingizini kuwa wapo baadhi ya walinzi binafsi tunaowapa kazi ya kutulinda sisi na mali zetu lakini si walinzi wema, bali ni hatari!

Katika jimbo la Florida nchini Marekani, kuna taarifa iliripotiwa kuwa mlinzi binafsi alimpiga risasi mtoto wa bosi wake aliyelazimisha kutoka nje ya eneo la nyumba yao kinyume na maelekezo ya baba yake!

Unapompa mtu kazi ya kuwakagua wote wanaoingia kwenye himaya yako, unapomsogeza mtu mwenye silaha iwe ya jadi au ya moto karibu na familia yako na wapendwa wako. Je, unamwamini kiasi gani? Je, unafahamu historia yake, tabia yake na utimamu wake!?

Kuna changamoto kubwa katika kumtambua mlinzi huyu ikiwa ni pamoja na kujua kama amewahi kuhusika kwenye uhalifu, hali yake ya kisaikolojia, hali yake kiafya kwa ujumla, mafunzo aliyofuzu na taarifa nyingine mtambuka.

Sekta ya ulinzi binafsi inapaswa kuangaliwa kwa jicho la umakini kwa sababu inagusa watu wengi zaidi duniani.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na gazeti la The Guardian la Uingereza na kuchapishwa Mei 2017, katika nchi nyingi, idadi ya walinzi binafsi ni kubwa zaidi ya idadi ya askari wa jeshi la polisi.

Inakadiriwa kuwa kuna walinzi takribani milioni 20 wa kampuni binafsi duniani kote; yaani zaidi ya idadi ya watu nchini Chile, Rwanda au Uholanzi.

Kwa mfano, nchini Marekani, inakadiriwa kuwa kuna walinzi zaidi ya Milioni moja wa kampuni binafsi, huku kukiwa na askari wa jeshi la polisi takribani 700,000 tu.

Hata hivyo, tofauti na askari wa jeshi la polisi, mlinzi wa kampuni binafsi ana uwezo wa kuhama kampuni moja na kujiunga na kampuni nyingine, au aliyeachishwa kazi katika jeshi la polisi kwa sababu mbalimbali kujiunga na sekta hiyo.

Kwakuwa ni vigumu kutambua historia ya mlinzi husika na kubaini mienendo yake, baadhi yao hata baada ya kufukuzwa kazi kwa kujihusisha na uhalifu, hujiunga na kampuni nyingine bila kubainika kirahisi.

Hii ni tofauti na ilivyo kwa jeshi la polisi ambapo kila askari ana namba moja inayomtambulisha, amefanyiwa usaili wa kina (vetting), amefuzu mafunzo husika na taratibu nyingine.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni akiwa jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa Chama Cha Sekta ya Ulinzi Binafsi Tanzania (TSIA), alisema kuwa kuna silaha zilizotumika kwenye uhalifu na kukamatwa na Jeshi la Polisi ambazo vibali vyake vilitolewa kwa kampuni binafsi za ulinzi.

Je, ni jinsi gani tunaweza kuwatambua na kutunza taarifa za mienendo ya wafanyakazi wa kampuni binafsi za ulinzi ili kuboresha sekta hii muhimu inayoongeza nguvu ya ulinzi wa raia na mali zao?

Teknolojia imerahisisha upatikanaji wa suluhisho la changamoto hii na nyingine zinazoikabili sekta hii.

Taarifa za mfanyakazi sasa zinaweza kuwekwa mara moja mikononi mwako hata kupitia 'simu yako.'



Mlinzi toka kampuni binafsi ya ulinzi akiwa tayari kwa kazi. **PICHA: MTANDAO**

**MFUMO WA KIELEKTRONIKI**

Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoanza kuchukua hatua kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa kusajili na kutambua kampuni na wafanyakazi wote katika sekta ya ulinzi binafsi, uliopewa jina la Mradi wa Uboreshaji wa Sekta ya Ulinzi Binafsi nchini kwa njia ya kielektroniki (PSGP).

Katika Mkutano Mkuu wa TSIA, Masauni alitoa alama kwa uanzishwaji wa mradi huo wa PSGP ambao unasimamiwa na Jeshi la Polisi akieleza kuwa utasaidia kutatua changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo.

PSGP imetayarishwa na Kampuni ya Kitanzania ya DataVision International ambayo imeshinda Tuzo ya 'East Africa Brand Leadership 2019' kama Kampuni Bora Zaidi katika utoaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utafiti pamoja na utengenezaji wa mifumo ya malipo ya kielektroniki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MRATIBU**

Macmillan George, Mratibu wa PSGP anaeleza kuwa kila mfanyakazi katika sekta ya ulinzi analazimika kusajiliwa kwenye mfumo ambapo atapatiwa namba maalum ya utambuzi kutoka Jeshi la Polisi. Namba hiyo itamtambulisha kama mfanyakazi katika sekta hii.

Kitambulisho cha mfanyakazi wa sekta ya ulinzi binafsi, kinakuwa na QR Code na namba hiyo maalum inayomtambulisha.

Hivyo, popote anapoki-scan hata kwa simu, taarifa zote za utambulisho wake na taarifa za historia yake zitaonekana mara moja. Aidha, PSGP pia ni ustawi kwa wafanyakazi wa sekta hiyo ikilenga kuwakwamua kiuchumi.

Walinzi waliokamilisha usajili na kupewa kitambulisho wanapata fursa ya mikopo kwa kutumia kitambulisho hicho ikiwa ni pamoja na kukopa sehemu ya mshahara kabla ya mwisho wa mwezi.

Kwa mantiki ya utambuzi huu, ni dhahiri Serikali itapata uhakika wa kukusanya kodi kwa kila mlinzi kielektroniki, ukizingatia maelfu kama sio makumi elfu ya wafanyakazi wa kampuni binafsi wanaoifanya sekta kuwa sehemu muhimu ya ajira rasmi na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Sekta hii ni moja kati ya sekta zenye thamani kubwa inayoweza kubeba sehemu ya uchumi wa dunia.

Kwa mfano, Agosti 2017, Jarida la Forbes lilieleza kuwa sekta ya ulinzi wa kampuni binafsi inakadiriwa kuwa na thamani ya dola bilioni 180 za Marekani, na kwamba inatarajiwa kufika dola bilioni 240 mwaka 2020.

Unaweza kuona ni jinsi gani sekta hii inaweza kuwa sehemu ya kuchagiza Tanzania kufikia uchumi wa kati endapo itasimamiwa kwa ufanisi.

Zaidi, kwa kuhakikisha kila mfanyakazi wa kampuni binafsi ya ulinzi anakuwa mlinzi salama, unajenga msingi imara wa kuwavutia zaidi wawekezaji wa nje.

Kumbuka, asilimia kubwa kama sio zote za kampuni hulindwa na kampuni binafsi ya ulinzi. Hivyo, PSPG inaweza kuhuisha ukuaji wa uchumi kwa kasi zaidi kwani wawekezaji wataendelea kumiminika wakiwa na uhakika wa usalama wao na mitaji yao katika kila ngazi.

Ni dhahiri, katika dunia ya sasa, tunaitegemea sana sekta hii. Mchango wake ni wa kipekee kwani walinzi hawa hujiweka mstari wa mbele kuzuia wahalifu, wakati mwingine baadhi hupoteza maisha.

Ni vyema kuweka chujio mahsusi la utambuzi wa kielektroniki ili kuwaondoa wale wanaochafua sekta na kuwanufaisha wanaofanya kazi zao kwa uaminifu. Tunatambua kuwa Serikali inaendelea kukamilisha mpango wa kuandaa na kuwasilisha bungeni sheria itakayoongoza sekta ya ulinzi binafsi, lakini usajili wa kielektroniki wa wafanyakazi wote katika sekta ya ulinzi binafsi unapaswa kupewa kipaumbele ili kuhakikisha tunakuwa na walinzi salama.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Sheria ndogo ndogo zinavyotatua ukatili kwenye masoko Shinyanga

- Mhalifu akibainika faini kati ya Sh. 5,000 hadi 15,000
- Samia ataka usawa uzingatiwe kwa jinsia zote

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia hasa kwa wafanyabiashara wanawake kwenye masoko mbalimbali nchini yamekuwa ni kero kwa jamii na Tanzania inapoelekea kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025.

Hayo ni pamoja na kuwavua nguo wanawake kwa maana ya kutukanwa matusi ya nguoni, kutakwa kimapenzi kwa nguvu, vipigo, kushikwashikwa maumbile yao bila ridhaa na hata kudhulumiwa fedha nyakati zingine.

April 26, 2019 gazeti la Nipashe lilichapisha makala inayopinga matukio hayo ya ukatili wa kijinsia kwenye masoko ya Shinyanga mjini katika chapisho lililokuwa na kichwa cha habari kisemacho: "Mtihani wa kinamama kufikia '50 kwa 50' katika ujasiriamali...

Makala hiyo ilielezea namna udhalilishaji mkubwa wanaofanyiwa wafanyabiashara wanawake sokoni ambapo ililenga kupinga vitendo hivyo katika dhima ya kuwawezesha wanawake kufanya biashara zao kwa amani na kuongeza vipato kwenye familia zao, hivyo kuondokana na dhana ya utegemezi kutoka kwa waume zao.

Mwandishi wa makala haya alitembelea masoko yote ya Shinyanga Mjini ambayo yamekuwa kinara cha ukatili wa kijinsia kwa wafanyabiashara wanawake.

Masoko hayo ni pamoja na Soko Kuu, Nguzo Nane, Ibinzamata, Kambarage, Majengo Mapya, Ngokolo Mitumbani, na Ndembezi.

Baada ya kufika kwenye masoko hayo alizungumza na wafanyabiashara wanawake, wakiwamo waathirika wa matukio hayo ya ukatili wa kijinsia, viongozi wa masoko pamoja na wafanyabiashara wa kiume ambao ndio watuhumiwa wa matukio hayo.

**SHIJA**

Merysiana Shija ni mfanyabiashara Mwanamke katika Soko la Ndembezi Shinyanga Mjini ambaye ni miongoni mwa waathirika wa matukio hayo ya ukatili wa kijinsia.

Anasema wanakumbana na lugha chafu za matusi kutoka kwa wafanyabiashara wenzao wanaume, lakini hata baadhi ya wateja, hasa wale wanaowahudumia chakula.

Anasema kabla ya kuacha biashara yake ya umamalishe na kuhamia kwenye biashara nyingine ya kuuza mboga, alikuwa akitoa huduma ya chakula kwa tenda kwa vibarua waliokuwa wakitengeneza barabara mjini humo.



Zuhura Athumani, mfanyabiashara wa mboga katika Soko la Ngokolo Mitumbani Shinyanga Mjini, akielezea namna ukatili wa kijinsia unavyofanyika sokoni hapo.

Merysiana anabainisha kwamba mara baada ya kumaliza ujenzi huo, wateja wake hao waligoma kumlipa na mbaya zaidi akiambulia matusi ya nguoni.

"Kwa kweli wafanyabiashara wanawake tunanyanyasika kwenye Masoko... tunatukanwa matusi ya nguoni kwa kutajwa nyeti zetu, vipigo, kushikwa shikwa maumbile bila ridha, kudhulumiwa fedha na hata kushuka kiuchumi sababu ya kuonekana sisi ni viumbe dhaifu," anasema na kuongeza:

"Mfano kwenye biashara yangu ya awali ya umamalishe niliachana nayo mara baada ya mtaji kukatika... nilikuwa nikilisha wajenzi wa barabara kwa tenda, lakini baada ya kazi yao kwisha waligoma kunilipa na nikaambulia matusi juu...sikuwa na namna zaidi ya kuanza biashara nyingine."

> "Kwa kweli wafanyabiashara wanawake tunanyanyasika kwenye Masoko... tunatukanwa matusi ya nguoni kwa kutajwa nyeti zetu, vipigo, kushikwa shikwa maumbile bila ridha...

**GILIGILI**

Muathirika mwingine wa matukio hayo ni Agnes Giligili, mfanyabiashara wa Soko la Ngokolo Mitumbani.

Anasema mwaka jana alikumbana na mkasa wa kutukanwa matusi ya nguoni kutoka kwa mfanyabiashara mwezake wa kiume anayeuza matunda.

"Nilikuwa nadai pesa yangu, hatua iliyonifanya nifunge biashara kwa muda kwa sababu ya kudhalilishwa... watu walijazana, nikaona aibu hivyo ikabidi nirudi nyumbani kupumzika," anasema na kuongeza:

"Hata hivyo, baada ya siku chache kijana huyo alinifuata nyumbani na kuniomba msamaha, kwa kitendo alichonifanyia cha kunidhalilisha, ndipo moyo wangu ukasawazika."

Agness anasema ukatili wa kijinsia kwenye masoko dhidi ya wanawake unapaswa kupigwa vita kwa sababu ya madhara yake yakiwemo ya kushusha utu wa mtu na uchumi wakati mwingine.

"Kwa mfano nilipofunga biashara yangu nilirudi nyuma kimaendeleo,"anasema.

**ATHONY SABUNI**

Huyu ni mfanyabiashara wa kiume kwenye Soko la Ngokolo Mitumbani.

Anakiri wanawake wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, sababu ikiwa ni ukosefu wa elimu ya ukatili, hali inayosababisha wengine kufanyiwa ukatili bila ya kujua. "Unajua wafanyabiashara wote wa kiume si kwamba wanafahamu nini maana ya ukatili wa kijinsia... mfano lugha hizi za matusi ya nguoni na kushikashika wanawake maumbile yao, kwenye masoko vinaonekana kama tu ni jambo la kawaida, lakini kumbe huo ni ukatili tena mkubwa sana," anasema na kuongeza:

"Ili kutokomeza ukatili huu kwenye Masoko yote ya Shinyanga Mjini, inapaswa elimu ya kupinga vitendo hivyo iendelee kutolewa, ikiainisha matendo yapi ni ukatili, ili watu wapate kufahamu."

**MWENYEKITI WA SOKO**

Mwenyekiti wa Soko la Ngokolo Mitumbani, Trasy Leonard, anasema mara baada ya kuona matukio ya ukatili wa kijinsia yakizidi sokoni hapo, waliita kikao na viongozi wenzake na kuamua kutunga sheria ndogo ambayo itatokomeza vitendo hivyo.

Leonard anasema walitunga Sheria kuwa mtu akitukana mwezake, awe mwanamke au mwanamume atapigwa faini ya Sh. 5,000, kufungiwa biashara yake kwa wiki mbili ama vyote kwa pamoja kwa lengo la kutoa fundisho kwa wanaoendeleza vitendo hivyo.

"Tumekuwa tukipambana na kupinga matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wafanyabiashara wanawake, ambao ndio waathirika wakubwa wa lugha za matusi, kushikwa maumbile yao, na hata kudhulumiwa fedha zao," anasema na kuongeza:

"Aidha, tumepiga marufuku wanawake kuvaa nguo fupi (vimini) zinazosababisha kwa namna moja ama nyingine ukatili wa kushikwa maumbile yao, hata kutakwa kimapenzi kwa nguvu."

**MWENYEKITI SOKO KUU SHINYANGA**

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Soko Kuu la Shinyanga Mjini, Alex Stephen, anabainisha kwamba baada ya kukithiri kwa vitendo hivyo katika soko lao nao walitunga Sheria ndogo.

Kwamba mtu akifanya kosa hilo atatozwa faini ya Shi. 15,000 na kutofanya biashara kwa wiki mbili.

Anasema Sheria hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia Sokoni hapo.

"Hata hivyo, bado kuna baadhi ya wanaume ambao wameendelea kuwafanyia

Inaendelea Uk. 18

JIELIMISHE

## KIJANA ANG'OLEWA MENO 526 INDIA



MTOTO wa miaka saba ambaye alikuwa akilalamika kuumwa na taya lake, amekutwa na meno 526 ndani ya mdomo, kwa mujibu wa hospitali moja nchini India alikokuwa akifanyiwa matibabu.

Mtoto huyo alilazwa mwezi uliopita katika mji wa Kusini wa Chennai kutokana na uvimbe na maumivu karibu na meno yake ya nyuma katika taya lake la chini kulia.

Kulingana na mtandao wa Zee News, wakati madaktari walipomfanyia ukaguzi katika kinywa chake waligundua kijifuko katika taya lake la chini kilichojaa meno yasio ya kawaida.

Kwa mujibu wa Ofisa Mkuu wa Masuala ya Vinywa wa Hospitali ya Meno na Taasisi ya Mafunzo ya Seveetha, wakati upasuaji wa kutoa meno hayo ukifanyika mwezi uliopita, madaktari walihitaji muda ili kuchunguza kila jino kabla ya kuthibitisha matokeo yao.

"Kijifuko hicho kilikuwa na uzito wa gramu 200, tulikitoa polepole,"anasema.

Mtandao huo unasema kwamba wazazi wake waligundua uvimbe huo wakati alipokuwa na umri wa miaka mitatu, lakini hawakujali sana kwa kuwa uvimbe huo haukuwa mkubwa.

"Hata hivyo baada ya uvimbe huo kuanza kuongezeka baadaye, wazazi hao walimleta mvulana huyo hospitalini kwetu," anasema Profesa P. Senthilnathan wa idara ya masuala ya vinywa na upasuaji.

Anasema picha iliyopigwa kwa kutumia miale ya X-ray ilibaini meno mengi yaliyowafanya madaktari kumfanyia upasuaji.

Ijapokuwa kulikuwa na vipande vidogovidogo, madaktari wanasema kuwa vilikuwa na ishara ya meno.

Ilichukua takriban saa tano kwa madaktari kutoa meno hayo madogo kutoka katika kifuko hicho.

"Kijana huyo alirudi katika hali yake ya kawaida siku tatu baada ya upasuaji," anasema Pratibha Ramani, Profesa na kiongozi wa idara ya vinywa katika hospitali hiyo.

Dk. Ramani ambaye alihusika katika upasuaji huo, aliiambia gazeti la Times nchini India kwamba, meno hayo yalikuwa na ukubwa tofauti.

Kulingana na madaktari hao hicho ndicho kisa cha kwanza duniani, kwa mtu mmoja kukutwa na meno mengi madogo.

Kwa mujibu wa Dk. Senthilnathan, ugunduzi huo unaonyesha kwamba kuna umuhimu wa kufanyiwa ukaguzi wa kinywa mapema iwezekanavyo.

Alisema ijapokuwa hamasa ya magonjwa ya vinywa inaimarika nchini humo, sehemu za mashambani bado kuna tatizo.

"Zamani masuala kama ukosefu wa madaktari wa meno, ukosefu wa elimu, ufukara ulimaanisha kwamba hakuna hamasa ya kutosha...lakini matatizo haya bado yapo," anasema na kuongeza:

"Unaweza kuona watu mijini wana hamasa ya kutosha lakini wanaoishi katika maeneo ya mashambani, hawana elimu ama hata uwezo wa kuwa na afya nzuri ya vinywa vyao."

Kulikuwa na kisa kama hicho mjini Mumbai mwaka 2014 ambapo meno 232 yalitolewa kutoka kwenye mdomo wa kijana mmoja.

**BBC**

# Sheria ndogo ndogo zinavyotatua

Inatoka Uk. 17

vitendo hivyo wanawake hasa Mama Lishe, pindi wanapokwenda kudai fedha za chakula.

**OFISA MAENDELEO JAMII**

Naye Ofisa Maendeleo Jamii wa Manispaa ya Shinyanga, Bestina Gunje, anawaasa wafanyabiashara wanawake kwenye masoko, kutobaki kimya pale wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, bali watoe taarifa kwa viongozi, ili wapate haki zao.

"Mfano wanapodhulumiwa malipo ya fedha zao, watoe taarifa mapema kwa viongozi wa Soko, waje katika ofisi zetu za manispaa au waende katika dawati la jinsia la Polisi, ili wahusika wakumbane na mkono wa sheria," anasema na kuongeza:

"Nimesikitika kusikia Mamalishe aliyedhulumiwa fedha zake na vibarua waliokuwa wakitengeneza barabara, akakaa kimya hatimaye mtaji wake ukakatika na kuanza biashara nyingine... angefika kwetu tungeweza kumsaidia kupata haki yake."

**MWANASHERIA**

Mwanasheria wa kujitegemea Matha Masalu kutoka Kampuni ya Masalu Law Attorneys Mkoani Shinyanga, anasema kumfanyia mwanamke ukatili wa aina yoyote ni kosa kisheria.

"Kuna vifungu vinapinga kumtolea lugha chafu mwanamke, pamoja na kumshikashika maumbile bila ya ridhaa yake," anasema.

**AGAPE**

Mustapha Isabuda ni Ofisa miradi kutoka Shirika la Agape mkoani Shinyanga, linalotetea haki za watoto na wanawake.

Shirika hili limeamua kuchukua jukumu la kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wafanyabiashara wanawake kwenye Masoko ya Shinyanga mjini, kwa kutoa elimu ya kupinga vitendo hivyo.

**MAKAMU WA RAIS**

## JE, WAJUA?



Watoto walioachiwa na makundi yenye silaha nchini Sudan Kusini. **PICHA: MTANDAO**

## Mwanafunzi aliyefariki Madagascar kwa 'kufungua mlango wa ndege '

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Cambridge ameanguka na kufa nchini Madagascar baada ya kufungua mlango wa ndege ndogo ikiwa angani, wanasema polisi.

Alana Cutland, mwenye umri wa miaka 19, kutoka Milton Keynes - Buckinghamshire, nchini Uingereza alifariki dunia wiki iliyopita, kulingana na taarifa iliyothibitishwa na wizara ya mambo ya kigeni ya Uingereza.

Polisi katika kisiwa hicho cha Afrika wamesema haijabainika wazi ni kwanini alifungua mlango wa ndege hiyo ndogo ilipokuwa angani.

Dhana moja ambayo inachunguzwa ni kwamba huenda alipata athari mbaya za dawa za kutibu ugonjwa wa malaria.

Familia yake inasema imesikitishwa sana na kifo cha binti yao ambaye walimuita kama "msichana mwenye akili, na huru."

Jafisambatra Ravoavy, ambaye ana cheo cha kanali katika Jeshi la polisi ya Madagascal, amemthibitishia mwandishi wa BBC kuwa Cutland alifungua mlango wa ndege baada ya ndege hiyo kupaa angani kutoka kwenye eneo la uwanja lisiloweza kufikiwa kwa urahisi, Kaskazini mwa Madagascar, Julai 25.

Alikuwa akisomea masomo ya sayansi ya mazingira katika chuo cha Robinson College na alikuwa kisiwani humo kupata uzoefu wa kazi.

Chanzo cha kifo chake bado hakijathibitishwa na mamlaka za Uingereza. Polisi wanatumia helikopta na barabara kuusaka mwili wake.

Katika taarifa, familia yake ilisema kuwa alikuwa ni msichana mwenye kipaji cha kucheza, akiwa ni mtu anayependa kujifunza mambo mapya "ambaye alitoa nuru kwa kila chumba alichoingia na kuwafanya watu watabasamu kwa kuwapo kwake tu.

"Alikuwa mkarimu kila wakati na mtu aliyeisaidia familia na marafiki zake, jambo ambalo lilimfanya ajenge urafiki na watu wa aina mbalimbali maishani mwake, ambao tunafahamu fika watamkosa sana," walisema.

Dk. David Woodman, kutoka Chuo cha Robinson College, anasema kuwa "Walishitushwa sana na taarifa ya kifo cha Alana" na wanatuma salamu zao za rambirambi kwa familia yake.

"Katika kipindi cha miaka yake miwili hapa shuleni, alitoa mchango mkubwa sana katika mambo mbalimbali ya kimaisha katika chuo hiki...tutamkosa sana sote," anasema.

Madagascar ni kisiwa kilichopo kwenye mwambao wa Kusini Mashariki mwa Afrika, ambacho ni maarufu kwa mbuga za kipekee za wanyamapori.

***BBC***

# UTAFITI

## RIPOTI: IDADI KUBWA YA WATOTO WALIUAWA, KUKATWA VIUNGO 2018

MWAKA 2018 umeongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya watoto waliouawa au waliokatwa viungo kwenye maeneo ya mizozo tangu Umoja wa Mataifa (UN), uanze kufuatilia na kuripoti uhalifu mkubwa kwenye vita.

Hiyo ni kwa mujibu wa Ripoti ya Katibu Mkuu wa UN, kuhusu watoto kwenye mizozo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kulikuwa na visa 24,000 vya ukatili ambavyo vimethibitishwa mwaka 2018 katika maeneo 20 yanayoshuhudia mizozo katika ajenda ya watoto kwenye mizozo.

Ripoti inasema, wakati idadi ya vitendo vya ukiukaji vya aina nyingine vikipungua au kusalia katika viwango vya awali, watoto zaidi ya 12,000 waliuawa au kujeruhiwa mara nyingi na matukio na ufyatulianaji risasi.

Pia mabomu ya kutegwa, vilipuzi vya mabaki ya vita, mabomu ya kutegwa ardhini na vitendo vya kijeshi kutoka kwa vikosi vya taifa, visivyo vya taifa na vya kimataifa.

Akizungumzia ripoti hiyo wakati akiiwasilisha mbele ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa UN kwa ajili ya watoto na migogoro ya silaha, Virginia Gamba anasema:

"Inasikitisha kwamba watoto wanaendelea kuathirika vibaya na uhalifu wa silaha, huku tukiwaona wakiuawa au kuachwa na ulemavu kutokana na uhasama."

Anaongeza: "Ni muhimu basi pande husika katika mizozo kutoa kipaumbele katika ulinzi wa watoto...hili haliwezi kusubiri, ni lazima zichukue wajibu wa kulinda watoto na kuweka mikakati ya kuhakikisha uhalifu huu hautokei."

Ripoti imetanabaisha baadhi ya vitendo vya uhalifu dhidi ya watoto huku watoto takriban 7,000 wakitumikishwa jeshini na Somalia ikisalia kuwa nchi yenye idadi kubwa ya watoto waliotumikishwa jeshini, ikifuatiwa na Nigeria na Syria.

Kwa mujibu wa ripoti, kumeripotiwa visa 933 vya ukatili wa kingono dhidi ya wavulana na wasichana.

Idadi hii inakadiriwa kuwa ndogo kuliko idadi kamili kutokana na kutofikika kwa baadhi ya maeneo, hofu dhidi ya unyanyapaa na kushambuliwa.

**MASHAMBULIZI MENGINE**

Kwa upande mwingine, mashambulizi dhidi ya shule na hospitali yamepungua kwa ujumla lakini yameimarika katika baadhi ya maeneo hususan Afghanistan na Syria ambako kuna mashambulizi hayo tangu kuanza kwa mizozo katika nchi hizo.

Nchi ya Mali ni mfano wa matukio ya watoto kunyimwa haki ya kupata elimu na kutumikishwa jeshini, huku shule 827 zilifungwa nchini humo kufikia mwisho wa mwezi Desemba mwaka 2018, na kuwanyima watoto 244,000 fursa ya kupata elimu.

**KUSHIKILIWA**

Ripoti inasema badala ya watoto kuchukuliwa kama wahanga wa utumikishwaji, maelfu ya watoto walizuiliwa maeneo tofauti kwa uhusiano wao au madai ya kuhusiana na vikundi vilivyojihami mwaka 2018. Katika muktadha huo ripoti imetoa wito kwa mataifa kufanya kazi na UN kuwatafuta watoto na wanawake wanaodaiwa kuhusika na makundi ya waasi, huku msingi ukiwa ni mahitaji ya watoto kupewa kipaumbele.

Idadi ya watoto walionufaika na msaada wa kujumuishwa katika jamii imeongezeka mwaka 2018 hadi 13,600 kutoka 12,000 mwaka 2017, ambapo ripoti imependekeza kuimarishwa kwa ufadhili ili kukabiliana na mahitaji yanayoongezeka wakati watoto wengi wakitenganishwa na makundi hayo.

SAINI

# ukatili kwenye masoko Shinyanga

Julai 30, 2019, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassani, akiwa Jijini Dodoma alizindua mradi wa kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto kwenye maeneo ya masoko, ambao utatekelezwa katika mkoa wa Dodoma na Shinyanga.

Mradi huo unatekelezwa na Jumuiya ya Tawala na Serikali za Mitaa (Alat) kwa ufadhili wa Shirika la UN-Women.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi huo, Samia ameonya tabia ya wanaume kuwadhalilisha wafanyabiashara wanawake sokoni kwa kuwashika maumbile yao, kuwatolea lugha chafu za matusi ya nguoni, na kutaka taarifa zitolewe ili wahusika wa vitendo hivyo wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Anasema wanaume na wanawake wanalindwa na Katiba, na wana fursa sawa za kushiriki shughuli za kiuchumi.

Kwamba wote wana haki ya kufanyabiashara kwenye masoko.

"Wanaume na wanawake wana haki ya kufanyabiashara kwenye masoko, lakini waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji ni wafanyabiashara wanawake, ambapo wamekuwa wakishikwa maumbile yao, kutolewa lugha chafu za matusi, na kudhulumiwa fedha zao," anasema na kuongeza:

"Masuala haya yanavunja heshima ya wanawake kwa sababu yanawafanya wajisikie vibaya na kuathirika pia kisaikolojia, sababu kutwa nzima anavurumishiwa matusi ya viungo vya mwili, pamoja na kushikwa matiti na hata akirejea nyumbani kwake anakuwa hana raha kabisa."



**Na Maneno Selanyika**

# Teknolojia inavyon'garisha utendaji Shirika la Posta



Makamu wa Rais, Samia Hassan (wa pili kulia), akimkabidhi tuzo Mkuu wa Banda la Shirika la Posta, John Tinga (kushoto mwenye kofia), katika maonyesho ya kimataifa ya 43 ya biashara maarufu kama Sabasaba mwaka huu Julai 2019. **PICHA: MANENO SELANYIKA**

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC) linamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Tanzania. Lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 19 ya mwaka 1993 na lilianza rasmi kutoa huduma Januari Mosi, 1994.

Lengo la Serikali kuanzisha shirika hilo ni kulipa jukumu kutoa huduma za kiposta ndani na nje ya nchi.

Shirika hilo lipo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo ndiyo ina jukumu la kulisimamia, kutunga sera na kutoa miongozo mbalimbali ya kuliendesha kupitia Bodi ya Shirika.

Uongozi wa shirika hilo unaeleza kuwa katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli, limefanya mabadiliko makubwa katika maeneo mbalimbali ya huduma kwa wateja.

Unabainisha kuwa mabadiliko hayo yamefanyika katika utoaji wa elimu, kasi na usalama wa mali za wateja na kuhakikisha linatoa huduma kwa bei nafuu.

Posta Masta Mkuu wa TPC, Hassan Mwang'ombe, anasema shughuli zinazofanywa na shirika hilo mbali na huduma za barua, vifurushi na vipeto, ni kutoa huduma nyinginezo zikiwamo za umiliki wa masanduku ya barua, huduma ya EMS, huduma za kulipa gawio la hisa, pensheni kwa wastaafu au mishahara kwa kampuni na taasisi mbalimbali.

Anasema huduma asili za shirika ni barua na vifurushi, akibainisha kuwa soko lina ushindani mkubwa wakiwa na zaidi ya kampuni 50 zinazoshindana.

"Shirika katika juhudi zake za kuhakikisha linatoa mchango wake kikamilifu katika kuchangia kujenga uchumi wa nchi yetu, limeingia mikataba na wizara na idara mbalimbali za serikali.

"Pia wateja wakubwa kama vile kampuni za simu, benki na NGO's kwa ajili ya kurahisisha zaidi kusafirisha barua, nyaraka na vifurushi vyao," Mwang'ombe anasema.

Anaongeza kuwa katika kipindi cha miaka minne iliyopita, shirika limeboresha huduma zake katika eneo la teknolojia na Tehama, akibainisha kuwa kwa sasa, shirika linatumia mifumo ya kisasa ya mawasiliano katika uendeshaji wa huduma ya EMS.

TEKNOLOJIA

Posta Masta Mkuu huyo anasema TPC inatumia teknolojia mbalimbali kama Netsmart na mfumo wa International Postal System (IPS) ambao unawezesha ufuatiliaji (Track na Trace) wa barua, nyaraka, vifurushi na vipeto vinavyosafirishwa kupitia nchi mbalimbali duniani na nchini kwa njia ya EMS.

Anasema teknolojia hiyo inamwezesha mteja kupitia kompyuta yake au simu ya mkononi kujua mzigo wake katika safari yake umefika wapi bila kulazimika kwenda Ofisi za EMS.

Anasema mifumo ya mawasiliano ya kisasa imewekwa katika ofisi ya kumjali mteja ambayo inashughulikia kwa haraka malalamiko, matatizo na hata kupokea maoni ya wateja.

Anaongeza kuwa mfumo mpya wa anwani za makazi na postikodi (Physical Addressing and Postcode System), utaiwezesha EMS kuboresha zaidi huduma zake hasa kwa makazi binafsi.

Anasema changamoto kubwa ilikuwa kujua mitaa na nyumba ya mteja, hivyo Postikodi itasaidia kuzitambua na kuiwezesha EMS kuwafikia wateja wake kirahisi zaidi ikiwa ni pamoja na huduma ya PCUM inayohusika na kukusanya na kusambaza nyaraka kwa haraka zaidi.

HUDUMA MPYA

Mwang'ombe anasema shirika mara kwa mara linabuni huduma mpya ili kukidhi mahitaji ya wateja wao.

Anabainisha kuwa katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa awamu ya tano, shirika limeanzisha huduma mpya na kuimarisha zilizokuwapo.

Anasema huduma zilizoimarishwa ni maduka ya kubadilisha fedha (Bureau de Change), akieleza kwamba kumekuwa na ongezeko la vituo vya kubadilisha fedha ndani ya Jiji la Dar es Salaam na katika mji mingine nchini, hususani kwenye maeneo yenye shughuli nyingi za kitalii na kibiashara.

"Mpaka sasa vituo zaidi ya 10 vya kubadilishia fedha jijini Dar es Salaam vimefunguliwa kikiwemo kile cha Kariakoo, Mtaa wa Libya, Oysterbay, Kijitonyama, City Drive, Posta Mpya na maeneo mengine katika mikoa kama Tanga, Arusha na visiwa vya Zanzibar," anasema.

Anabainisha kwamba shirika linatarajia kufungua vituo vipya kama vile Posta Kuu za Mbeya, Karatu, Namanga na Meru jijini Arusha na Posta Kuu Mwanza, Dodoma, Moshi na Viwanja vya ndege vya Zanzibar na Dar es Salaam.

"Pia tunatazamia kufungua vituo zaidi hasa sehemu zinazoonekana kuwa na wageni wengi katika mikoa mbalimbali nchini," anasema.

Anaongeza kuwa shirika limeanzisha maduka mawili ya kimtandao, moja likiwa kwa ajili ya ununuzi wa stempu na la pili la kuagiza bidhaa kwa njia ya mtandao kisha kufanya malipo kwa njia hiyohiyo.

"Kuanzishwa kwa duka la kuuza na kununua bidhaa kwa njia ya mtandao (e-shop) ni matokeo ya utekelezaji wa mikakati iliyopitishwa na taasisi zinazoendesha huduma za posta duniani," anasema na kuongeza:

"Pia, shirika limeendelea kuimarisha huduma zake za usafirishaji wa barua na vifurushi kwa kuimarisha huduma zake baada ya kuongeza magari yake ya kusafirisha mizigo mikubwa kupitia huduma yake ya Post Pargo."

Anabainisha kuwa huduma ya Post Bus, ambayo ilikuwapo miaka ya 2000, kwa sasa imerejeshwa na wameanza kusafirisha abiria kwenye barabara za Makambako-Songea na Masasi-Mtwara.

"Nyingine ni ya Virtual Box, hii ni huduma ya mteja analipia sanduku la barua kupitia namba maalum ambapo popote alipo ana uwezo wa kulipia sanduku lake la barua kupitia njia za kibenki ama kwa simu ya mkononi, pia ana uwezo wa kutuma ujumbe kuomba kifurushi ama

barua yake afikishiwe mpaka alipo popote pale," anasema.

Mwang'ombe anafafanua kuwa TPC imeendelea kuimarisha huduma ya Posta mlangoni katika sehemu ambazo miundombinu ya anwani za makazi zimekamilika na kwamba litaendelea kupanua huduma hizo kwa wananchi kwa kadri ya miundombinu hiyo itakavyoimarika.



# WADAU SABATO KASIKA

**NI kipindi cha udahili kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha sita ili kujiunga na vyuo mbalimbali vya elimu ya juu. Hata hivyo, huwa kuna changamoto ya baadhi ya waombaji kuomba kozi zenye ushindani mkubwa kulingana na ufaulu wao. Wadau wanasemaje?**



**VENANCE GILBERT (MHITIMU, SHAHADA YA AWALI YA ELIMU KATIKA LUGHA NA MENEJIMENTI (BED-LM) CHUO KIKUU MZUMBE)**

KUMEKUWAPO na manung'uniko miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu, ambayo hutokana na kozi wanazosoma chuoni. Kuna sababu kadhaa za kufanya hayo. Hata hivyo, kuna mambo kadhaa mwanafunzi anaweza kuyazingatia katika suala zima la kuchagua kozi ya kusoma, ambayo ni kama yafuatayo: Ujuzi alionao ingawa kuna baadhi ya kozi hazihitaji ujuzi sana vyuoni, lakini atambue kuwa suala la ujuzi ni la muhimu katika kipi usomee. Kwa mfano ujuzi katika lugha, hesabu au kuwa na uwezo wa kuhifadhi kumbukumbu. Zipo kozi zinazohitaji uwezo wa kukumbuka, kwa mfano sheria japo kozi zote huhitaji kumbukumbu lakini nyingine huhitaji zaidi. Ujuzi alinao mwanafunzi utamsaidia kusoma vyema kozi yake na hivyo kila siku masomo yatamwendea vizuri. Lingine ni kutambua nini anapenda. Hivyo baada ya kugundua ujuzi au uwezo ulio nao, suala linalofuata ni kufahamu unapenda kufanya nini. Lengo lake linatakiwa liwe kufanya jambo ambalo unalipenda, hii itamsaidia katika kuridhika na masomo yako, utasoma kwa furaha sana na utakuwa umeridhika. Haya yote yatawezekana kama sababu tajwa hapo juu hazitaingilia anachopenda kusoma. Pia mwanafunzi anapaswa kutafuta kitabu cha chuo kinachoelezea kwa kina kuhusu hali ya chuo yaani 'University Prospectus', kisha apitie kozi anazotaka. Prospectus ni kitabu kinachoelezea mambo ya kiutawala na kitaaluma kuhusu chuo. Pia kinaelezea vizuri kuhusu kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo husika ikijumuisha kozi ndogondogo, ambazo hufundishwa kwa muda wote wa masomo.




**MAGESA NATHANAEL (MSOMI WA SHERIA, MKAZI WA BAGAMOYO PWANI)**

CHANGAMOTO imekuwa ikisababisha baadhi ya wanafunzi kukimbia kozi. Binafsi niliwashuhudia kwenye kozi yetu ya sheria. Wakati mwingine hiyo inatokana na uchaguzi wa kozi gani, ambayo anataka kusoma chuo kikuu na zipo sababu mbalimbali zinazochangia hayo hasa kuanzia kwenye uchaguzi wa kozi kwa kufuata mkumbo wa marafiki, kushawishiwa na hata wakati mwingine kuchaguliwa kozi na wazazi. Wengine wanaweza kuwaona rafiki au ndugu zao ambao walisoma kozi fulani na kufanikiwa, wakatamani kusoma kozi hiyo bila kujali kwamba bahati ya mwingine hawawezi kuilalia mlango wazi. Mtindo huo husababisha wengine kukimbia kozi au kuhitimu wakiwa hawana sifa kwenye ushindani wa soko la ajira. Kwa hiyo wanaojiandaa kujiunga na elimu ya juu watambue kuwa wanatakiwa kuzingatia ufaulu wao katika kuchagua kozi ili hatimaye waweze kuingia katika soko la ajira. Kwa kuzingatia hayo, mwanafunzi anaweza kufanya vizuri katika masomo yake ya juu bila kuwapo kwa changamoto, ambazo zimekuwa zikiwakumba baadhi yao wanapofanya udahili. Kila mwanafunzi awe makini katika kuchagua kozi lakini pia ni muhimu kuchagua chuo kulingana na ufaulu badala ya kukimbilia vyuo ambavyo anajikuta hana sifa ya kujiunga navyo eti kwa sababu tu ya ushawishi kutoka kwa watu wa karibu.



**ANNA ELIAS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SUALA hili ni la kujadili kwa umakini ili kusaidia wanafunzi ambao wanatarajia kuingia vyuo vikuu mwaka huu, kwani kila mwaka kumekuwa kukijitokeza changamoto kwa baadhi yao kuchagua kozi bila kuzingatia ufaulu wao. Hali hiyo inasababisha wengine kujikuta wakikosa nafasi za masomo kwa mwaka husika. Chanzo kikubwa kikiwa ni wanafunzi wenyewe kung'ang'ania baadhi ya vyuo kwa sababu vina hadhi. Hapa jambo la msingi ni wenyewe kuhakikisha ufaulu wao unakidhi vigezo vya ushindani wa kozi na vyuo wanavyochagua, vinginevyo watapoteza muda kurudia mchakato wa uchaguzi wa kozi. Kwa maana hiyo ni vyema kila mwanafunzi anayejiunga na chuo kikuu atambue kuwa ufaulu wake ndiyo ushindani wake. Iwapo mwanafunzi hakuchaguliwa katika chuo na kozi fulani, basi anatakiwa kuhakikisha ana mbadala mwingine wa chuo, aache kung'ang'ania chaguo la kozi ambalo hakuchaguliwa. Ikumbukwe kuwa kwa utaratibu wa siku hizi ni kwamba iwapo mwanafunzi hakuchaguliwa kozi fulani huwa anapewa na sababu, na anapaswa kuzizingatia. Lakini akipuuza, matokeo yake ni kutoa malalamiko yasiyo na msingi kwa kudhani ameonewa na kumbe mwenye ndiye amechangia kuharibu au kushindwa kufuata taratibu za kumwezesha kufikia malengo ambayo amejiwekea katika masomo ya elimu ya juu. Kimsingi ni kila upande utimize wajibu wake katika udahili.



**AGNESS JULIUS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWENYE mchakato wa kuchagua kozi, mtu anaweza kutafsiri vyovyote anavyoona. Lakini kwangu mimi ni kwamba kuna jambo la msingi la kuzingatia pale mwanafunzi anapochaguliwa kuingia chuo kikuu, hasa la kuorodhesha kozi anazotaka kusoma kulingana na jinsi anavyopendelea. Pia akumbuke kuwa pamoja na kuorodhesha kozi nyingi, mwisho wa siku ni moja tu ambayo atatakiwa kusoma au kwa kupangiwa na chuo kutokana na jinsi alivyochagua ama kubadili mwenyewe. Vipo baadhi ya vyuo huwa vinaruhusu kubadili kozi mwanzoni mwa muhula wa kwanza na pia vipo vingine haviruhusu utaratibu huo. Hivyo kama mwanafunzi atakuwa hajaipenda zaidi kozi husika, anaweza kuahirisha mwaka wa masomo au kuhama chuo. Sambamba na hilo wanafunzi wanaotarajia kujiunga na masomo ya elimu ya juu hawatakiwi kuwa wavivu wa kusoma maelekezo kabla ya kuanza kujiunga au kuchagua kozi katika vyuo. Wanafunzi wanatakiwa kuzingatia sifa zinazohitajika katika kujiunga na kozi na kuangalia ufaulu wao kabla ya kuanza kujaza fomu, kwa kutambua kuwa serikali haina utaratibu wa kumpangia mwanafunzi programu ya kusoma, isipokuwa anachagua mwenyewe kutokana na sifa alizonazo kwenye kozi husika.



**JUSTINA MASANJA (MKAZI WA JIJINI MWANZA)**

BAADHI ya wanafunzi wanapokuwa katika sekondari na hasa kuanzia kidato cha tano na sita, huwa na ndoto zao ambazo zinaweza kuwa hazizingatii ni wapi uwezo wao ulipo. Wapo ambao hufikia hata kubagua kozi za kusoma kwa kufuata mkumbo bila kuangalia uwezo wao. Wakati mwingine hata wazazi na walezi huhusika katika tatizo hili la kuchagulia watoto wao kozi ya kusoma, kwamba mtoto asomee kozi fulani. Wakati mwingine wanafanya hivyo bila kujua uwezo wa mtoto wao darasani ukoje, na wanakwenda na mawazo hayo hadi vyuo vikuu. Sasa matokeo yake ndio hayo ya changamoto wanazokutana nazo kwenye uchaguzi wa kozi. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imewahi kusema kuwa ufaulu wa wanafunzi wanaoomba kujiunga na vyuo ndio imekuwa changamoto katika kuchagua vyuo na kozi za kwenda kusomea. Kwamba tume inakutana nazo kwa waombaji kwa kutozingatia ufaulu wao na kozi husika sambamba na chuo wanachoomba. Tume inasema kuwa mwanafunzi anaweza kuwa ana daraja la kwanza, lakini ana 'C' tatu mwingine ana daraja hilohilo lakini ana 'A' tatu, sasa mkiomba kozi moja na inahitaji watu kumi. Hivyo siyo rahisi mwenye 'C' kuchaguliwa na kuachwa mwenye 'A' tatu. Tatizo kubwa linaelezwa kuwa ni waombaji kushindwa kuzingatia ufaulu wao na idadi ya watu wanaohitajika kwenye kozi katika chuo wanachoomba. Kwa hiyo ni muhimu wanafunzi kuzingatia vigezo ili kumaliza changamoto inayoweza kuwakumba.



# Maambukizi ya VVU Mbeya, Songwe tishio

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SHIRIKA la World Vision Tanzania limezindua mradi maalumu wa kupambana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) katika mikoa ya Mbeya na Songwe, huku taarifa zikionyesha kuwa kiwango cha maambukizi katika mikoa hiyo kimegoma kushuka.

Mradi huo una malengo makuu mawili ambayo ni kuwatambua watu wanaoishi na VVU, kuwaunganisha na huduma za matibabu na kuhakikisha wanaendelea kutumia dawa pamoja na kutekeleza mbinu mbalimbali za kuzuia ukatili wa kingono kwa watoto wenye umri kati ya miaka tisa na 14.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi wa World Vision Tanzania, Dk. Kasilima Yosh, alisema mradi huo unazihusisha taasisi za dini, viongozi wa mila, taasisi za umma na baadhi ya viongozi wa serikali.

Alisema mradi huo ni wa miezi 15 na unafadhiliwa na Shirika la PEPFAR kupitia Shirika la Henry Jackson Foundation (HJF) na unatekelezwa kupitia Shirika la Caritas pamoja na Hospitali ya Igogwe, iliyopo wilayani Rungwe.

**Endapo mradi huo utafanikiwa, kuna uwezekano mkubwa wa kufikia sifuri tatu ifikapo mwaka 2030 na sifuri ya kwanza ni kutokuwapo kwa vifo vitokanavyo na Ukimwi, sifuri ya pili ni kutokuwapo kwa maambukizi mapya.**

Dk. Yosh alisema mradi huo unatekelezwa katika halmashauri tatu ambazo ni Ileje na Mbozi kwa Mkoa wa Songwe na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa Mkoa wa Mbeya.

Alisema wameamua kuzishirikisha taasisi za dini kutokana na mipango mingi ya kupambana na Ukimwi kutekelezwa kupitia vituo vya afya na hivyo wananchi kutoshirikishwa vizuri.

"Mpango huu unalenga kufikia malengo ya 95 ifikapo mwaka 2023 kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe ambayo ni asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU wawe wanajua hali yao, asilimia 95 ya pili ya watu wote wenye VVU wawe wameanzishiwa dawa na asilimia 95 ya tatu wote wanaotumia dawa wawe wamefubaza virusi," alisema Dk. Yosh.

Alisema endapo mradi huo utafanikiwa, kuna uwezekano mkubwa wa kufikia sifuri tatu ifikapo mwaka 2030 na sifuri ya kwanza ni kutokuwapo kwa vifo vitokanavyo na Ukimwi, sifuri ya pili ni kutokuwapo kwa maambukizi mapya.

Kwa upande wake Mratibu wa Tume ya Kupambana na Ukimwi (Tacaids) Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Petro, aliwaomba viongozi wa dini kuwa mabalozi wazuri wa mradi huo kwa kuwahamasisha waumini wao kupima afya zao.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa mikoa hiyo, lakini endapo watajitokeza wapotoshaji bila kukemewa unaweza ukashindwa kuleta matokeo chanya.

"Kuna baadhi ya wahubiri na viongozi wa dini wamekuwa wakiwapotosha wananchi, unasikia kiongozi wa dini anasema amemwombea mgonjwa wa Ukimwi amepona na anamshawishi aache kutumia dawa, tafadhali tunaomba mtusaidie kukemea watu wa aina hiyo," alisema Petro.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Donald Bombo, aliushukuru uongozi wa World Vision na wadau wake kwa kuleta mradi huo katika mikoa ya Mbeya na Songwe na kueleza kuwa ni mara ya kwanza kwa shirika hilo kupeleka miradi katika mikoa hiyo.

Alisema katika mikoa hiyo maambukizi yamegoma kabisa kushuka kwa kuwa mpaka sasa katika mikoa hiyo maambukizi bado ni asilimia 9.3 na kwa Mkoa wa Songwe ambao ni mpya maambukizi ni asilimia 5.8.

Aliwataka wadau wote kushiriki katika kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa asilimia 100 ili ulete matokeo chanya kwa mikoa husika.

## Wapewa somo kilimo cha mkataba

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WADAU wa zao la alizeti katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi, wamepewa somo kuhusu kilimo cha mkataba cha zao hilo ili kuongeza uzalishaji na kupunguza kiwango cha uagizaji wa mafuta ya kupikia kutoka nje ya nchi.

Meneja wa Mradi wa kuboresha mifumo ya masoko ya maziwa na alizeti (Tam), unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la nchini Uholanzi (SNV) chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Uingereza (Ukaid), Tom Ole Sikar, alitoa elimu hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao maalumu cha wadau wa alizeti kilichofanyika jijini hapa.

Alisema wakulima wengi wa mikoa hiyo wana elimu ndogo kuhusu kilimo cha mkataba na kwamba ndio maana shirika hilo limeamua kuanza mradi wa kuwaelimisha ili waachane na kilimo cha mazoea na kuzalisha kwa tija.

Ole Sikar alisema uzalishaji wa alizeti katika mikoa hiyo ni mdogo kuliko uhalisia wa taarifa za kiutafiti na kuwa wakulima wengi wamejikita katika uzalishaji wa mazao mengine yakiwamo ya nafaka na mikunde.

"Tumebaini kuwa wakulima wa mikoa hii hawajui kuwa kilimo cha alizeti ni kilimo cha biashara ambacho kinaweza kuwatajirisha, wengi wamejikita katika uzalishaji wa mahindi na wanaishia kupanda alizeti kuzunguka mashamba hayo ya mahindi, tunataka wabadilike," alisema Ole Sikar.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya kuna wakulima wawili pekee wakubwa wa alizeti ambao mmoja analima ekari 100 na mwingine ekari 80 na kuwa mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji.

Vilevile alisema asilimia 66 ya mafuta yanayotumika nchini yanaagizwa kutoka nje ya nchi na kusisitiza wakulima kuongeza uzalishaji wa alizeti ili kuuza bidhaa nje ya nchi.

Naye Ofisa Mshauri wa Sera wa Shirika la SNV, Renatus Mbamilo, alisema wadau wa zao hilo wanakabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinasababisha zao hilo kutokuwa na tija kama ilivyo kwenye mikoa ya Singida na Dodoma.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na wakulima kutokuwa na elimu ya kilimo bora ikiwamo matumizi ya mbolea, mbegu zisizokuwa na ubora pamoja na changamoto za kisera.

Alisema baadhi ya wadau wakiwamo wanunuzi wa alizeti na wasafirishaji wamekuwa wakikabiliwa na tozo mbalimbali wanaposafirisha mbegu kutoka katika maeneo ya wakulima kwenda kwenye viwanda hali ambayo alidai inawakwamisha.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, akiangalia mpunga uliotokana na mbegu aina ya Supa BC iliyoboreshwa kwa teknolojia ya nyuklia kwa kutumia mionzi ya Gamma, iliyotumika kumulika mbegu za zamani aina ya Supa. Mradi ulifadhiliwa na Shirika la Nguvu za Atomiki la Kimataifa (IAEA) na kuratibiwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Taasisi ya Kilimo Zanzibar (ZARI). Kwa sasa wananchi wa visiwani Zanzibar wanatumia mchele uliotokana na mbegu hiyo tangu mwaka 2011. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Sumatra yawaonya madereva wa Bajaj

Na Nebart Msokwa, MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (Sumatra) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imetoa onyo kali kwa madereva wa pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la 'bajaji' kuacha kuingilia njia za magari ya abiria 'daladala'.

Wametakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za usafirishaji ambazo zinawaongoza ikiwa ni pamoja na kutumia njia za pembezoni zilizoainishwa.

Meneja wa Sumatra Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daudi, alisema kundi hilo ni miongoni mwa makundi yanayoongoza kwa kuvunja sheria za usafirishaji kwa kuingilia njia za daladala na kuchukua abiria kwenye vituo vya daladala.

Alisema kwa sasa wanajipanga kuanza operesheni maalumu ya kuwadhibiti madereva hao ili kuondoa changamoto zinazojitokeza ikiwamo migogoro na wadau wengine wa usafirishaji ndani ya Jiji la Mbeya.

Daudi alisema kwa mujibu wa sheria, usafiri wa bajaji unapaswa kukodiwa na si kuchukua abiria katika vituo vya daladala kama wanavyofanya baadhi yao na kusisitiza kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Mwanzoni mwa mwaka huu kulitokea mgomo wa daladala ndani ya Jiji letu la Mbeya na sababu kubwa ilikuwa ni kuingiliwa njia zao na bajaji, tulilazimika kukaa mezani, tukajadiliana na kufikia uamuzi ambao ulileta mafanikio, lakini sasa hawa waendesha bajaji wameanza tena kukiuka," alisema Daudi.

Alisema kwa sasa yawezekana wasikae tena vikao na badala yake kinachofuata ni usimamizi wa sheria na wametoa elimu vya kutosha na sasa ni utekelezaji.

Mwenyekiti wa Bajaji Jiji la Mbeya, Idd Ramadhani, alisema kutokana na changamoto hiyo wamelazimika kukaa kwenye vituo vya daladala kufanya operesheni ya kuwakamata madereva wanaokiuka sheria za usafirishaji.





# Jiji kuandaa utaratibu mpya wamachinga

Na Peter Mkwavila, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inakusudia kuandaa utaratibu kwa wafanyabiashara ndogondogo (machinga) utakaowawezesha kufanya biashara kwenye vyombo vinavyohamishika kama matoroli.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara zao kando kando mwa barabara zilizopo jijini hapa.

Alisema hivi karibuni kumekuwa na wimbi la wafanyabiashara hao kupanga na kuweka meza katika maeneo ya barabara hizo.

Alisema wanaandaa utaratibu ambao utawafanya wauze bidhaa zao kwenye matoroli badala ya kuweka kwenye meza na fremu ambazo zimekuwa zikiwekwa kwenye maeneo ya barabarani na yasiyo rasmi.

**Bado kuna changamoto kwa baadhi yao kufanya biashara zao kwa kukiuka sheria hizo.**

Pia Yuna alisema jiji hilo linatoa elimu hiyo ili kuhakikisha wafanyabiashara ndogondogo wanafanya biashara zao bila bugudha kwenye maeneo yao ambayo yametengwa rasmi.

"Halmashauri ya Jiji kwenye masoko yake yote bado yana nafasi kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo hatuoni sababu ya kufanya biashara zao kwenye maeneo yanayohatarisha maisha yao," alisema.

Alisema elimu waliyoitoa imeweza kusaidia kufanya biashara hizo kwa kufuata kanuni, sheria na utaratibu kwa mujibu wa halmashari ya jiji hilo tofauti na hapo awali walipokuwa wakivamia maeneo yasiyo rasmi kwa kufanya biashara hizo.

Katibu wa wafanyabiashara eneo la CCM makao makuu Happy Dickson, alisema hivi sasa wameondolewa kwenye eneo hilo baada ya kupatiwa elimu ya kutosha kutokana na madhara yanayoweza kutokea kwa kufanya biashara eneo lisilo rasmi.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi yao kufanya biashara zao kwa kukiuka sheria hizo.

"Pamoja na Rais wetu ikiwamo Halmashauri ya Jiji kutujali na kuturuhusu kufanya biashara zetu kwa uhuru, pia tunatakiwa kuzingatia usalama wetu na mali zetu kwa kutofanya biashara hizo kwenye maeneo yasiyo rasmi na hii itatusaidia kuondokana na migogoro isiyo rasmi kwa upande wetu sisi wamachinga," alisema.



Mwanafunzi Braiton Nanda wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi El Shadai ya jijini Dodoma, akielezea jinsi alivyofundishwa kuhusu rangi za Bendera ya Taifa kwenye mahafali ya sita ya darasa la saba yaliyofanyika shuleni hapo, eneo la Ihumwa, mwisho wa wiki. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Jafo ataka maonyesho kuwa endelevu

Na Renatha Msungu, DODOMA

HALMASHAURI za mikoa ya Dodoma na Singida zimetakiwa kuhakikisha mabanda yaliyopo viwanja vya Nanenane yanatumika kutoa elimu kwa wananchi mbinu za kisasa kwenye sekta ya kilimo na mifugo kipindi chote badala ya kusubiri msimu wa maonyesho pekee.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akifungua maonyesho ya wakulima na wafugaji kanda ya kati, katika viwanja vya Nanenane Nzuguni, jijini hapa.

Alisema wananchi wanatakiwa kuendelea kupata elimu ya jinsi ya kulima na kufuga kisasa kipindi chote bila kusubiri Nanenane.

"Uwepo wa mabanda haya utawezesha wananchi kujifunza masuala mbalimbali ya kilimo kwa mwaka mzima bila kusubiri kipindi cha Nanenane, mwaka 2016 niliagiza ifanyike hivi sio msubiri Nanenane kupata per diem (posho)," alisema.

Jafo pia aliwaagiza wakuu wa mikoa ya Dodoma na Singida kuhimiza taasisi na watu binafsi kuweka mfumo wa uvunaji maji ya mvua ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara.

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na uharibifu wa miundombinu ya barabara inayosababishwa na maji yanayotiririka barabarani msimu wa mvua.

"Ni vema kuzihimiza taasisi zote wakiwamo watu binafsi kuweka mfumo wa uvunaji maji ambao utazuia madhara hayo ikiwamo kuwapa faida, wao wataweza kuyatumia maji hayo kwenye shughuli mbalimbali za kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Alipongeza mikoa hiyo kwa kuongezeka kwa pato la mtu mmoja kutoka asilimia 1.39 ya mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 1.52 kwa mwaka 2018.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema maonyesho hayo yamekuwa chachu kwa wananchi kujifunza mbinu mbalimbali za kisasa kwenye kilimo na ufugaji.

# Aagiza mabaraza ya ardhi kero yavunjwe

Na Mwandishi Wetu, KONGWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Kongwa kuvunja mabaraza ya ardhi na usuluhishi yanayolalamikiwa na wananchi kutokana na kutotenda haki kwenye mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi.

Dk. Mahenge alitoa agizo hilo katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza na kutatua kero za wananchi, wilayani humo.

Alisema mabaraza hayo yamekuwa wakiwakandamiza wananchi kisheria.

"Mkuu wa Wilaya, Mwanasheria na Mkurugenzi pitieni vizuri mabaraza ya kata yote ili mjiridhishe na kama kuna malalamiko vunja baraza, wachaguliwe wapya na wafanyiwe uchunguzi," aliagiza.

Vile vile, alisema mabaraza mengi yanalalamikiwa kila sehemu na suala hilo linaweza kumalizwa na uongozi kwa kuwachagua watu watakaotenda haki kwa wananchi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratus Ndejembi, aliwataka wananchi kutumia viongozi kwenye maeneo yao kuwasilisha malalamiko hayo ili yaweze kutatuliwa.

Akiwasilisha kero zao kuhusu mabaraza kwa mkuu huyo, wananchi hao walisema watu wasio na uwezo ndio wamekuwa wakionewa kwenye mabaraza hayo.

Walisema katika hukumu kuna watu wanaoshindwa na kushindwa, lakini kuna malalamiko namna kesi zinavyoamuliwa licha ya kulalamikiwa kwenye ngazi mbalimbali.

**Mkuu wa Wilaya, Mwanasheria na Mkurugenzi pitieni vizuri mabaraza ya kata yote ili mjiridhishe na kama kuna malalamiko vunja baraza, wachaguliwe wapya na wafanyiwe uchunguzi.**



## CCM yahamasisha wanawake nafasi uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, amewataka wanawake mkoani huko kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi nyakati za uchaguzi wa viongozi nchini.

Alitoa rai hiyo wakati akifunguwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake (UWT) Mkoa wa Kaskazini Unguja, akiamini kwa kufanya hivyo kutaleta mabadiliko katika uongozi.

Alisema CCM imetoa fursa kwa makundi mbalimbali kuwania nafasi za uongozi bila ya ubaguzi wa jinsia.

Alisema wanawake wameundiwa jumuiya yao (UWT) ambayo ni taasisi inayojishughulisha na kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake kugombea uongozi.

"Chama Cha Mapinduzi hakina ubaguzi wa jinsia, kimetoa nafasi kwa makundi mbalimbali ikiwamo wanawake na wanaume kugombea nafasi za uongozi kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya uongozi na kuleta maendeleo," alisema.

Ame aliwapongeza wanawake wa UWT kwa kufanya kazi kwa ari katika kujenga uhai wa chama na kuona kinapiga hatua kubwa ya kushika hatamu ya uongozi.

Alisema UWT siku zote imekuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi.

"Mkoa wetu unayo imani kubwa na umoja wa wanawake katika kukitetea chama na kuona kinashika hatamu ya kuongoza dola katika kipindi cha uchaguzi mkuu," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mariyamu Muharami Shomari, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanawake wanajitokeza kuwania nafasi mbalimbali za juu za uongozi katika mkoa huo wakati ukifika.

Aliwataka wanawake kuacha tabia ya kuwatafuta wagombea sehemu nyingine na kuwaleta katika mkoa huo ambao.

Alisema kitendo hicho kwa kiasi kikubwa kimekuwa kikisababisha majungu na malumbano ambayo hutishia ustawi wa chama.

"Nachukuwa nafasi hii kukemea baadhi ya tabia za viongozi kuwatafuta wagombea wengine sehemu nyingine na kuwaleta hapa, kitendo hicho husababisha mgawanyiko wa chama na kuleta uhasama," alisema.

**Nachukuwa nafasi hii kukemea baadhi ya tabia za viongozi kuwatafuta wagombea wengine sehemu nyingine na kuwaleta hapa, kitendo hicho husababisha mgawanyiko wa chama na kuleta uhasama.**

# Kinamama waona fursa ushonaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KINAMAMA katika Kijiji cha Kijini Mbuyu Tende, Mkoa wa Kaskazini Unguja wameanza kujiajiri kupitia kazi za ushonaji baada ya kupatiwa mafunzo ya Mradi wa Huduma za Jamii wa Best of Zanzibar.

Mwenyekiti wa Kituo cha Ushonaji cha Kinamama, Mboje Khamis Shauri, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya kituo hicho, mradi huo umelenga kutumia soko na sekta ya utalii kujiingiza kipato.

Alisema kinamama hao pia wameona fursa katika kuwahudumia wahitaji wa sare za wafanyakazi na wanafunzi katika shule za msingi na sekondari za Kijini na Matemwe Mbuyu Tende.

"Lengo letu kubwa kutumia soko la sekta ya utalii na kuwaondoshea usumbufu wananchi, badala ya kununua sare za wanafunzi mjini, wanunue hapahapa kijini kuwapunguzia gharama," alisema.

Alisema changamoto kubwa kwa sasa kwa kinamama hao ni mtaji na upatikanaji wa vifaa.

Ofisa Elimu wa Mradi wa Best Of Zanzibar, Ali Suleiman Hamad, alisema wameamua kuanzisha kituo cha ushonaji kwa lengo la kuwawezesha kinamama kujiajiri baada ya kuona hoteli za kitalii zinaendelea kuongezeka katika ufukwe wa Matemwe Mbuyu Tende.

Alibainisha kuwa kituo hicho sasa kina mafundi wanane waliopata mafunzo Kurasini jijini Dar es Salaam kabla na wao kuanza kutoa mafunzo kwa wanawake wenzao.

Ali alisema vijiji vya Kijini na Matemwe Mbuyu Tende vinakabiliwa na umaskini huku ardhi yake ikiwa haifai kwa kilimo kutokana na kuwa na mawe.

**Changamoto kubwa kwa sasa kwa kinamama hao ni mtaji na upatikanaji wa vifaa.**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mpinduzi Zanzibar, Mohamed Aboud (kushoto), akitoa cheti kwa mshiriki wa kozi fupi ya saba ya viongozi mbalimbali wa kitaifa (NDC) 2019, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Laurean Bwanakunu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waziri aonya uzembe watumishi hospitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, amewaagiza viongozi na wafanyakazi wa Hospitali ya Kivunge kuingia kazini kwa zamu kama ilivyo katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja ili wananchi wapate huduma muda wote wanapozihitaji.

Alisema agizo hilo linapaswa kutekelezwa kuanzia kesho ili kuhakikisha afya za wananchi zinaimarishwa kwa kupatiwa matibabu kwa wakati.

Aliyasema hayo katika Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A Unguja baada ya kupokea malalamiko ya wananchi kwa kukosa huduma kwa wakati.

Alisema utaratibu wa kuingia kazini kwa zamu utaondosha malalamiko yaliyojitokeza na kuonyesha kirahisi utendaji wa kila mfanyakazi.

"Huu ni mpango rasmi wa serikali utakaoanza wiki ijayo, tunaanza kwa Hospitali ya Kivunge, utakwenda na Makunduchi na nyingine zinafuatia," alisema.

Waziri Hamad pia aliwataka wafanyakazi wa hospitali hiyo kutumia lugha nzuri katika kuwahudumia wagonjwa, akieleza kuwa lugha nzuri huwapa faraja.

Mkurugenzi wa Utumishi wa Wizara ya Afya, Ramadhani Khamis Juma, alisema kwa upande wa utumishi, serikali imejitahidi kuwasomesha ili watoe huduma bora na kwa wakati.

Mkurugenzi wa Tiba wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Juma Salum Mbwana, aliwataka watumishi wenzake kujirekebisha na kufanya kazi kwa bidii ili kuepuka kuwajibishwa.

HABARI KITAIFA

# Wawekezaji mji wa kisasa waaswa mgogoro wa fidia

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amewataka wawekezaji wa mradi wa mji wa kisasa wa Star City mjini Morogoro kuachana na mgogoro wa kutaka fidia ili kupishe ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa itakayopitisha treni ya mwendokasi ndani ya eneo lao la uwekezaji.

Amesema kukamilika kwa reli hiyo kutaongeza tija na kurahisisha shughuli wanazokusudia kuzifanya.

Waziri Bashungwa aliyeambatana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alisema hayo baada ya kutembelea mradi wa kiuwekezaji wa mji wa kisasa wa Star City uliopo Manispaa ya Morogoro.

Viongozi hao walielezwa na mwekezaji wa ujenzi huo kuwa ujenzi wa reli hiyo umetumia eneo lao ambalo lilitengwa rasmi kwa madhumuni ya serikali kujenga bandari kavu ili kupunguza msongamano wa malori yanayokwenda Bandari ya Dar es Salaam.

**Nia ya serikali ni kujenga uchumi wa viwanda, na kuhakikisha malengo ya wawekezaji binafsi yanafanikiwa, na kwamba hata mwekezaji huyo kutokana na uwekezaji mkubwa alioufanya.**

Meneja Mkuu wa Mji huo wa kisasa wa uwekezaji, Annath Bhat, alisema kumegwa kwa eneo hilo kungekwamisha baadhi ya shughuli za ujenzi wa miundombinu ya mji huo.

Waziri Bashungwa alisisitiza wamewomba mwekezaji kukubali makubaliano kwa kuachana na fidia baada ya kuona picha kubwa ya mradi huo sambamba na kuangalia manufaa makubwa yatakayokuja mbeleni baada ya kukamilika kwa mradi huo kiuchumi.

Alisema nia ya serikali ni kujenga uchumi wa viwanda, na kuhakikisha malengo ya wawekezaji binafsi yanafanikiwa, na kwamba hata mwekezaji huyo kutokana na uwekezaji mkubwa alioufanya, atahitaji miundombinu hiyo ya reli na ndio maana akataka kuwapo maridhiano kati ya serikali na mwekezaji huyo kwani bado mradi wa reli ya kisasa utakuwa na manufaa makubwa kwa taifa.

Naye Naibu Waziri Nditiye alikiri iwapo wanataka kupitisha mradi wowote, ni lazima sheria huwataka walipe fidia kwa watu au taasisi binafsi, lakini kama watakuta ni mali ya serikali kinacholipwa huwa ni mali iliyopo na sio ardhi, na kwamba ujio wao katika mji huo wa kisasa ni kuhakikisha wanaondoa vikwazo vyovyote vinavyojitokeza katika sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji (EPZA), Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, alibainisha changamoto hizo zilivyochelewesha kuanza kwa uwekezaji huo mkubwa, na kuwa kupita kwa treni ya mwendokasi katika eneo la mradi kutasaidia sana uwekezaji na viwanda.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Steven Kebwe, alifafanua miradi hiyo yote ina faida kubwa sana kwa mkoa wa Morogoro.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Ofisa Biashara wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Gulila Mapuli (kulia), alipotembelea banda la benki hiyo, katika viwanja vya maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane, Nzuguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Veta yabuni mashine udhibiti upotevu mazao

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

WAKATI serikali kupitia Wizara ya Kilimo, ikianza mkakati maalumu wa udhibiti wa upotevu wa mazao ya chakula baada ya kuvunwa ili kukabiliana na mahitaji ya chakula kutokana na tishio la upungufu wa chakula, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imebuni mashine rahisi ya kuzuia upotevu wa mazao ya chakula baada ya kuvuna.

Akizungumza katika banda la maonesho ya kilimo yanayofanyika katika Viwanja Nanenane Kitaifa Kanda ya Ziwa mkoani Simiyu, mgunduzi wa mashine hiyo ambaye pia ni mwalimu wa utengenezaji zana za kilimo kutoka VETA, Gema Ngoo, alisema mashine hiyo ina uwezo wa kuzuia upotevu wa mazao ya mpunga, ngano, mtama na uwele wakati wa umenyaji baada ya mavuno.

Ngoo, alisema mashine hiyo iliyotengenezwa mahususi kwa ajili ya kumsaidia mkulima imewekwa injini ndogo yenye uwezo wa kutumia lita tatu ya mafuta ya petroli na kumenya gunia kumi kwa siku na kuzuia upotevu wa mazao hayo, hivyo kuwa na uhakika na usalama wa chakula baada ya kuvuna.

Mwalimu huyo alisema lengo la kuamua kutengeneza mashine hiyo rahisi limekuja baada ya kuona wakulima wengi nchini wamekuwa wakipoteza chakula kwa kiwango kikubwa wakati wa mavuno, kutokana na kutumia teknolojia duni ikiwamo ya kupiga mpunga wakiwa mashambani kwa kutumia miche ya vinu ambayo imekuwa ikipoteza chakula kwa kiwango kikubwa.

Alisema mashine hiyo inayowezwa kukokotwa na wanyamakazi kama punda, ng'ombe na wengine pia inaweza kuvutwa na trekta ndogo itaweza kusaidia mpango wa serikali wa kusaidia wakulima katika upotevu wa chakula wakati wa mavuno na kuwataka wakulima kufika katika banda la maonesho hayo ya Nanenane kujionea na kujifunza kuhusu teknolojia ya mashine hiyo ambayo inauzwa kwa bei ya chini.

# Watumishi wa umma watakiwa kutimiza wajibu

**Na Restuta Damian,** MULEBA

WAAJIRI katika sekta ya umma wametakiwa kutimiza wajibu ambao wamepewa ili kuondoa ucheleweshwaji wa taarifa za watumishi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, wakati akizungumza na viongozi wa Wilaya ya Muleba baada ya kupokea taarifa za utumishi na utawala kwenye wilaya hiyo.

Alisema waajiri katika halmashauri wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea kwani wakuu wa idara ndiyo wenye jukumu la kutuma taarifa katika ofisi husika, ili kurahisisha utoaji wa maamuzi kwa kuzingatia sifa na taratibu.

"Tatizo jingine watumishi wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea na kusahau majukumu yao, wakuu wa idara na waajiri ndiyo wenye kuandaa taarifa za watumishi wengine, lakini imekuwa ni ucheleweshaji tunabaki kulaumiana," alisema Mwanjelwa.

Aidha, alisema lengo la kufanya haraka kwenye kupata ufumbuzi wake katika mkoa wa Kagera kuna changamoto hiyo, hivyo lazima waajiri wawajibike isavyo katika kuandaa taarifa kamilifu na zinazotakiwa. Katika hatua nyingine, Dk. Mwanjelwa alisema kuwa mtumishi wa umma lazima kuibua ubunifu, uadilifu wa kinidhamu katka kazi kwa kutofautisha watumishi wa sekta binafsi na umma.

"Kinachotakiwa sasa ni ubunifu, wafanyakazi fanyeni ubunifu wakati sisi tutaona kile unachokifanya msifanye mazoea, ubunifu wa mambo mbalimbali kazini ndiyo utumishi huo," alisema Mwanjelwa.

Hata hivyo alisema kuwa tayari madaraja 193,000 yamesharuhusiwa kupandishwa watumishi wa umma kwa nchi nzima.

Aliongeza kuwa ushirikiano kati ya wakurugenzi na kamati ya ulinzi na usalama katika kuweka wazi shughuli zote za halmashauri hiyo ndiyo sehemu ya utawala bora na kuwa njia moja ya kuijenga serikali.

Awali akitoa taarifa ya utumishi na utawala wilayani Muleba, Mkuu wa Wilaya hiyo, Richard Ruyango, alisema katika wilaya hiyo kuna uhitaji wa watumishi 5,837 wakati waliopo ni 3,701.

Alisema wamepokea kibali cha kupandisha vyeo watumishi 1,128, walimu wakiwa 1,002 na 126 ni waliokuwa wakitumikia idara mbalimbali.

## HABARI KIMATAIFA

# India yaifuta Kashmir kuwa jimbo

**NEW DELHI,** India

INDIA imetangaza kuifuta hadhi maalum ya Jimbo la Kashmir pamoja na kufanya mabadiliko ya utawala wa jimbo hilo katika moja ya hatua kubwa kuwahi kuchukuliwa katika eneo hilo lenye utawala wa ndani.

Uamuzi huo umetangazwa na Waziri wa Mambo ya Ndani wa India, Amit Shah, wakati maelfu ya wanajeshi wakiwasili kwenye jimbo la Kashmir ambalo linapinga kutawaliwa na India.

Tamko hilo limefuta ibara ya 370 ya katiba ya India ambayo inatoa ruhusa kwa Jimbo la Kashmir kuwa na katiba yake yenyewe pamoja na haki ya kufanya maamuzi kuhusu masuala yote isipokuwa ulinzi, mawasiliano na mambo ya kigeni.

Ibara hiyo ya katiba ambayo itafutwa inawazuia raia wa India walio nje ya jimbo la Kashmir kununua ardhi, kufanya kazi katika serikali za mitaa, kupata nafasi za ufadhili wa masomo zinazotolewa kwa ajili ya jimbo hilo, pamoja na kuishi jimboni humo moja kwa moja.

**Kwa miongo kadhaa waasi katika eneo la Kashmir lililo chini ya utawala wa India wameongoza mapambano ya kupinga kuwa chini ya India.**

Wakosoaji wa serikali ya India inayoongozwa na jamii ya walio wengi ya wahindu wameitaja hatua hiyo kuwa jaribio la kulazimisha jimbo la Kashmir kuwa chini ya mamlaka kamili ya India na kuruhusu jamii ya wahindu kuchanganyika na wakazi wa jimbo hilo ambalo wakazi wake wengi ni waislamu.

Vyombo vya habari vya India vimeripoti kuwa serikali ya India imeamuru Jimbo la Kashmir ligawanywe katika maeneo mawili yenye uongozi tofauti ambayo ni Jammu Kashmir na Ladakh.

Hatua hiyo imekuja baada ya siku kadhaa za kukosekana utulivu na kuwasili kwa vikosi vya jeshi kwenye jimbo la Kashmir pamoja na kukamatwa kwa wanasiasa mashuhuri wa jimbo hilo ikiwamo mawaziri viongozi wa zamani, Mehbooba Mufti na Omar Abdullah.

Kwa miongo kadhaa waasi katika eneo la Kashmir lililo chini ya utawala wa India wameongoza mapambano ya kupinga kuwa chini ya India.

Wakazi wengi wa jimbo hilo wanaunga mkono madai ya waasi yanayotaka jimbo hilo liunganishwe chini ya utawala wa Pakistan au liwe nchi huru na wamekuwa wakishiriki maandamano kupinga utawala wa India.

Uamuzi huo wa India unatarajiwa kuwa utazusha machafuko na kuzidisha mvutano na Pakistan.

India na Pakistan zinadhibiti maeneo tofauti ya Jimbo la Kashmir lakini nchi zote mbili zinadai umiliki kamili wa eneo zima na zimepigana vita mbili kuwania eneo hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Pakistan, Shah Mahmood Qureshi, alikieleza kituo kimoja cha televisheni nchini Pakistan kuwa India imefanya kosa kubwa kwa kuiondolea Kashmir hadhi yake maalum na kwamba Pakistan itaongeza juhudi za kidiplomasia kukabiliana na kile alichokiita matendo yanayokiuka sheria.

Kwenye Mji Mkuu wa Pakistan, Islamabad, maelfu ya wanaharakati wanaounga mkono uhuru wa jimbo la Kashmir wameandamana karibu na ubalozi wa India muda mfupi baada ya India kutangaza uamuzi huo. **DW**

## Trump atangaza siku tano za maombolezo kitaifa

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, juzi ameamrisha bendera zote za taifa zipandishwe nusu mlingoti katika ofisi zote za serikali katika kipindi cha siku tano.

Lengo kuu ni kutoa heshima kwa wahanga wa mashambulizi la risasi yaliyotokea mwishoni mwa juma mjini El Paso katika majimbo ya Texas na Dayton, watu wapatao 29 walifariki.

Rais Trump ametaja mashambulizi hayo kuwa yanatokana na matatizo ya maradhi ya akili na amesema atatoa taarifa rasmi muda wowote kuhusu mashambulizi hayo.



Rais Trump aliwaambia waandishi wa habari kuwa chuki haina nafasi nchini Marekani na kwamba juhudi zinafanyika ili kuzuia mashambulizi mengine yasitokee siku za usoni.

Viongozi wa Jimbo la Texas wameeleza kuwa shambulizi la El Paso ni ugaidi wa ndani, na kwamba waendesha mashitaka wanapanga kuomba adhabu ya kifo dhidi ya mshukiwa wa shambulizi hilo.

Wagombea wengi wa kiti cha urais katika chama cha Democratic wamemshtumu Rais Trump kwa kile wanachosema matamshi yake ya chuki dhidi ya wahamiaji ndio yamechochea shambulizi lililotokea Mji wa El Paso.

Rais wa Mexico, Manuel Lopez Obrador, amethibitisha kuwa raia sita wa Mexico ni miongoni mwa watu waliouawa katika shambulizi lililofanyika ndani ya duka la Walmart katika mji huo wa El Paso ambao unapakana na Mexico.

Mashambulizi ya El Paso na Dayton ni ya 21 na 22 kufanyika tangu mwaka 2019 ulipoanza. **VOA**




Kiongozi wa Chama cha PDP cha Kashmir, Fayaz Ahmed, akizungumza na waandishi wa habari kulaani hatua ya India kuifuta hadhi maalum ya Jimbo la Kashmir. **PICHA: ALLIANCE**

## Msomi mwenye degree 6 afariki bila ajira

**NAIROBI,** Kenya

MSOMI na mwanasiasa kutoka Kenya, Dk. Reuben Savai (70), ambaye aliwahi kuwania kiti cha urais mwaka 1997 na 2002 na kushindwa amefariki.

Mtoto wa kiume wa mwanasiasa huyo, Daniel Lihanda amethibitisha kifo cha baba yake.

Licha ya kuwa na shahada sita na cheti cha diploma, mwanasiasa huyo mwenye utata hakuwahi kupata kazi nchini Kenya.

Dk. Savai ambaye alikuwa ni Kiongozi wa chama cha Kenya Republican Reformation Party ambaye alisomea shahada sita nchini Ugiriki na diploma kutoka Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda, juhudi za kupata kazi Kenya ziligonga mwamba.

Baadhi ya vitu alivyosomea ni pamoja na Diploma ya Thiolojia, Shahada moja ya sheria, shahada mbili za elimu na nyingine moja ya Sayansi.

Familia yake imesema alizuiliwa kufanya kazi ya sheria nchini Kenya kwa sababu hakufuzu katika chuo cha mafunzo ya sheria nchini humo.

Dk. Savai, ambaye alitaka kuwampinga marais wastaafu wa Kenya Daniel Arap Moi na Mwai Kibaki, alizuiliwa kuwania kiti cha urais kwa kukosa stakabadhi zilizohitajika kuidhinishwa kushiriki chaguzi hizo

Miaka ya 1990, alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa chama cha Forum of Restoration and Democracy (Ford), Kenya iliporejea kwenye mfumo wa siasa ya vyama vingi.

Mwaka 1997, Dk. Savai aliwania kiti cha ubunge lakini alishindwa na Raila Odinga, ambaye wakati huo alikuwa kiongozi wa chama cha National Development Party (NDP).

Lihanda aliliambia gazeti la Nation kuwa baba yake alikutwa amefariki nyumbani kwao katika kile kinachoshukiwa kuwa kupooza.

Lihanda alisema baba yake hakuwahi kuajiriwa nchini Kenya licha ya elimu kubwa aliyokuwa nayo na kujihusisha kwake katika siasa za nchi hiyo.

"Alisomea ulaya na kupata shahada sita na cheti cha Diploma. Aliporudi Kenya hakuwahi kupata kazi akaamua kujitosa katika siasa" alisema Lihanda.

Aliongeza kuwa baba yake alikuwa akisumbuliwa na tatizo la shinikizo la damu licha ya kukabiliwa na hali ngumu ya maisha.

Familia ya mwanasiasa huyo imetoa wito kwa wahisani kuisaidia kuchangisha kiasi cha dola 1,274 kugharamia mazishi yake.

Mwili wake umepelekwa katika chumba cha kuhifadhi maiti mjini Kaimosi Magharibi mwa Kenya. **BBC**

# Mwenyekiti wa CCM kortini tuhuma rushwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, imemfikisha mahakamani Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Likongowele, Mohamedi Ndope (Kifuku), akituhumiwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 300,000.

Ndope alifikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Liwale, Erasto Phili, na kusomewa shtaka linalomkabiri na Mwanasheria wa Takukuru, Osborn Paossi.

Paossi alidai mshtakiwa alikamatwa na taasisi hiyo eneo la Nangando, Liwale Mjini, Julai 28, mwaka huu, majira ya usiku akipokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mlalamikaji, ambaye ni mtumishi wa Idara ya Afya Kijiji cha Likongowele.

"Mshtakiwa alikamatwa baada ya watumishi wa taasisi kuweka mtego, uliofanikiwa kumkamata akiwa anapokea kiasi hicho cha fedha," alidai Paossi.

Paossi alidai kuwa, mtuhumiwa aliomba rushwa hiyo kutoka kwa mtumishi huyo, kwa kile kilichoelezwa kutaka kumsaidia asichukuliwe hatua za kinidhamu kufuatia uwapo wa malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi.

Mwanasheria huyo wa Takukuru Mkoa wa Lindi, alidai kutokana na kitendo hicho, mshtakiwa akiwa ni kiongozi wa chama cha siasa ambacho kinapinga rushwa, amefanya kosa kwa mujibu wa kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kosa hilo na yupo nje kwa dhamana, huku kesi yake imepangwa kusikilizwa tena Agosti 15, mwaka huu.




Wakazi wa Bariadi mkoani Simiyu, wakipatiwa huduma mbalimbali kwenye banda la Vodacom katika viwanja vya Nanenane Nyakabindi. Kampuni ya Vodacom imewaandalia wateja wao huduma za kidigitali ikiwamo vifaa vya intaneti na simu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vijiji 1,300 vyapatiwa umeme wa REA

**Na Happy Severine,** SIMIYU

JUMLA ya vijiji 1,310 kati ya vijiji 3,559 Tanzania Bara zimepatiwa umeme wa uhakika kupitia mradi wa umeme vijijini (REA) awamu ya tatu mzunguko wa kwanza ambao unagharimu takribani kiasi cha Sh. trilioni 1.2.

Kupitia mradi huo ambao unatarajia kukamilika Juni mwakani, REA imesema kuwa wanatarajia kuwapata wateja 200,000 tangu mradi ulipoanza utekelezaji wake Julai, 2018.

Hayo yalielezwa jana na Kaimu na Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Masoko na Teknolojia wa REA, Mhandisi Advera Mwijage, alipokuwa anazungumza na Nipashe katika maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Mhandisi Mwijage alisema kuwa vijiji hivyo ambavyo vimefikiwa na mradi tayari wameshawasha umeme na makandarasi wote wapo na wanaendelea na kazi ya kuhakikisha mradi huo unakamilika mwaka 2020.

Aliongeza kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuvifikia vijiji vyote 12,268 Tanzania Bara ifikapo mwaka 2021, na kuviwekea umeme, huku katika mkoa wa Simiyu mradi huo ukifikia asilimia 66 ya utekelezaji wake.

Alisema katika mkoa wa Simiyu wanatarajia kufikia takribani vijiji 152 kupitia mradi huo na wateja 7,000 kwa gharama ya Sh. bilioni 34.2.

"Mradi huu mbali na kuwafikia wananchi wengi sasa hivi, umefanikisha kuanzishwa kwa viwanda vya nguzo za umeme kutoka vitatu hadi tisa, mita za umeme kutoka 0 hadi 4, transfoma moja hadi nne, na waya kutoka moja hadi tano," alisema Mhandisi Mwijage.

"Viwanda hivi vimeanzishwa baada ya agizo la serikali ya awamu ya tano la kutaka vifaa vinavyotumika kwenye mradi huu vitoke kwenye viwanda vya ndani na siyo nje ya nchi na vimeanzishwa ndani ya miaka miwili tu," aliongeza Mhandisi Mwijage.

Naye Meneja uzalishaji wa kiwanda cha nguzo Qwihaya Co.Ltd kilichopo mkoani Iringa, Fredy Ngwega, alisema kupitia mradi huo wa umeme vijijini, wamefanikiwa kuongeza uzalishaji wa nguzo kutoka 300 kwa siku hadi 1,800.

"Kama kiwanda tumepata mafanikio makubwa kupitia mradi huu na agizo la serikali, wafanyakazi wameongezeka kutoka 50 hadi 300, na mafanikio haya yamepatikana ndani ya miaka miwili toka mradi umeanza utekelezaji wake," alisema.

Naye Issaya Hezron, msimamizi wa uzalishaji kutoka kiwanda cha Baobab Energy System kilichopo mkoani Pwani kinachozalisha mita za umeme, alisema wana uwezo wa kuzalisha mita 1,000 kwa siku.

## Waziri afunda wanaushirika

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, amewataka wanaushirika nchini kufanyakazi kwa bidii ili kuongeza wigo wa ajira zinazoweza kuzalishwa na vyama vya ushirika nchini.

Aidha, alitaka ajira zinazoweza kuzalishwa kuwa ni ufundi, biashara na viwanda kwa wakati ambao serikali ya awamu ya tano imejipambanua kuelekea kwenye uchumi wa viwanda 2025.

Manyanya aliyasema hayo jana alipotembelea eneo linapofanyika mafunzo ya ushirika yanayofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika viwanja vya Nanenane vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Mafunzo yanayoendeshwa katika "Kijiji cha Ushirika" ambacho kinaundwa na mabanda ya tume, vyama vya ushirika pamoja na wadau wa ushirika.

Tume hiyo inatoa elimu kwa wajumbe wa Bodi za Mazao ya Kilimo, na watendaji wa vyama vya ushirika ili kuwawezesha kuendesha vyama kwa weledi na viwango bora.

"Elimu hii ikalete mabadiliko chanya katika ushirika, isiishie kwa viongozi bali ifike kwa wanachama ili kuleta mabadiliko chanya," alisema Mhandisi Manyanya.

Awali Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Charles Malunde, alisema tume inatumia fursa ya maonyesho ya Nanenane kutoa mafunzo kwa watendaji na viongozi wa vyama vya ushirika kutoka maeneo mbalimbali.

"Mafunzo haya yanatoa fursa ya kuwajengea uwezo watendaji na viongozi wa vyama kwa kuwakutanisha vyama vya ushirika, taasisi na wadau wa ushirika kama vile Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) pamoja na Shirikisho la vyama ya Ushirika (TFC)," alisema Malunde.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Zavery Mkingule, alisema ni muhimu vyama vya ushirika kufanyiwa ukaguzi na kupata hati ya ukaguzi.

"Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayotoa picha juu ya taarifa za fedha alizokagua kama zinaonyesha hali halisi au sivyo," alisema na kuongeza:

"Kuonyesha hali halisi maana yake ni kwamba taarifa za fedha zimeandaliwa kulingana na viwango vya uhasibu vilivyokubalika na pia taarifa hizo hazina makosa yoyote makubwa au ubadhirifu na hivyo kutopotosha picha halisi," alisema Mkingule.

Mambo yaliyojadiliwa ni utawala bora, uandishi wa taarifa za fedha, majukumu ya bodi, haki na wajibu wa mwanachama na kusisitiza kuwa ni muhimu wanachama kufuatilia vyama vyao kwa kuwa maamuzi ya chama ni ya wanachama wenyewe.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo ambaye ni Mjumbe wa Bodi kutoka chama cha Jojababi Shinyanga, Amina Malale, alisema kuwa mafunzo hayo yamemwongezea maarifa hususan katika masuala ya utendaji na uongozi katika chama cha ushirika.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAHITAJIKA MHASIBU SIFA:** MWANAMKE ELIMU: DIPLOMA MAWASILIANO: 0715 885533 / 0752 610700.

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA

### KUPOTEA KWA KADI


**Honorary Consulate** of the Republic of Sierra Leone anatangaza kupotea kwa kadi yenye usajili wa namba T.310 CC3 ya gari aina ya TOYOTA HILUX, yenye chasis namba **PN133JV2508500540.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/OST/RB/187368/2019**

115361202

### KUPOTEA KWA CHETI




**Ulrick Mdendemi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.157/28** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1985 katika shule ya Sekondari Hanga Seminary.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: SO/RB/5456/2018**

115361102

### KUPOTEA KWA CHETI



**Ayubu Joel Mlugu** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0964/0019 kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2002 katika shule ya Sekondari Hombolo.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi taarifa: KJN/RB/186/015**

115361902

### KUPOTEA KWA CHETI



**Benitha Benjamin Rwaiyama** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha nne na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4104/0013 kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Lord Baden Powell Sekondari.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/KIG/RB/186950/2019**

115361802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Sara Barankena Sospeter** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenyen **index namba S.1642-0033** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Heri.

**Yeyote atakekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/BUG/RB/182680/2019**

115361702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA ARDHI RUFAA NA. 17/2017**
**SUED AMANI LEMA ............................................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SAMSON NGUJI CHOMOLA NA WENZAKE .........WAJIBU RUFAA**

KWA:
1. SEMISTATUS HUSSEIN MASHAMBA
2. JALALA MUSTAFA YSUFU
3. GODFEY ROBERT SIMON
4. ISACK JOEL KUDEL
5. SALUM AWADH AL-GUHUM
6. MAPINDUZI ANDREA KIKASA
7. EMMANUEL LUSIANA DAFAY
8. SHAURI QAMANA
9. MWANZI YOHANES MBILINYI
10. ANNA LAWRANCE NGOWI
11. EDWARD ELIAS BUGANDA & ANNE ISDORY MSIKE
12. LILIAN JONARD KIMARO
13. IDDY SAI MAMBINA
14. PASCAL CHARLES MAGANDULA
15. RAPHAEL MAGALAMILE JOSHUA
16. ALPHA CHOLOBI

POPOTE PALE WALIPO

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI RUFAA NA. 17/2017 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

MNAFAHAMISHWA KWAMBA; shauri tajwa hapo juu linatajwa Mahakama kuu ya Tanzania,kanda ya Dodoma,mbele ya MHE.JAJI L.MANSOOR,wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00)kamili asubuhi siku ya ijumaa tarehe 23/8/2019.

HIVYO; Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; Hamkufika nyinyi wenyewe au Mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyinyi au Mawakili wenu kuwepo

IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 29/07/2019.

215361402

**AFFIDAVIT FOR CONFIRMATION OF OWNERSHIP OF LAND AND CONFIRMATION OF LOSS OF LETTER OF OFFER OF RIGHT OF OCCUPANCY**

**PLOT NO.597 BLOCK 'P' MABAWA AREA, TANGA CITY**

**I BARAKAELI ELIBAHATI MUNGURE,** a Christian male adult P.O Box 178 Tanga do swear and state as follows:-

1. That I am the rightful owner of the above mentioned property and in that respect I was issued with a Letter of Offer of right of Occupancy **Ref No. TAD/20511/6/KAM** dated 11th February, 1999 (hereinafter referred to as the "the Letter of Offer").
2. That sometime in July, 2019 I lost the said Letter of Offer and diligently reported the same at Police station in Tanga **TAN/RB/180015/2019.**
3. I hereby verily declare and confirm that I am the rightful and registered owner of the property with the above reference.

**VERIFICATION I**, the said **BARAKAELI ELIBAHATI MUNGURE** hereby verify that what is stated hereinabove is all true, by virtue of the Oaths and Statutory Declaration Act, Cap.34, R.E. 2018.

215361602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 11/2018.**
**SAMWELI STEPHANO ...............MRUFANI**
**DHIDI YA**
**PHILIMON ATHUMANI ............MRUFANIWA.**
**KWA: PHILIMON ATHUMANI**
**(POPOTE PALE ULIPO )**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na. 11/2018 yamepangwa kutajwa tarehe 12.08.2019 mbele ya mwenyekiti wa Baraza E. MOGASA saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe /mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa .Usipohudhuria Baraza litasikiliaza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 08/07/2019

215361502

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA**
**AT MWANZA**
**(WITH EXTENDED JURISDICTION)**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 02/OF 2019**
**IN THE MATTER OF THE PROBATE AND ADMINISTRATION OF ESTATE ACT**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RAJNIKANT KHIMJI PATEL**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR APPOINTMENT OF EXECUTOR OF THE ESTATE OF RAJNIKANT KHIMJI PATEL BY AVINASH KHIMJI PATEL**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**


All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of August 2019.

The Will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.
Dated at Mwanza this 02nd day of August, 2019.

215361302

### KUPOTEA KWA CHETI



**William Paul** anatangaza kupotelewa na cheti cha cha Ualimu Daraja A chenye **index namba E.510/437** kilichotolewa na chuo cha Ualimu Tabora(TCC) mwaka 1997.

**Yeyoteatakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi taarifa: KIGL/RB/6000/016**

115360602

### KUPOTEA KWA VYETI



**David Maluila** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.395/40** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1988 katika shule ya Sekondari Boza, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.147/657** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1991 katika shule ya Sekondari Pugu.

Yeyote atakaviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MLA/RB/1240/2009**

115360502

### KUPOTEA KWA VYETI



**Coletha Thomas Lyimo** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.222/27** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1977 katika shule ya Sekondari Zanaki, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.218/507** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1979 katika shule ya Sekondari Rugambwa.

**Yeyote atakaviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: MOSH/RB/7340/16**

115360302

### KUPOTEA KWA CHETI



**Judith Abel Mafuta** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba **S.4841/0035** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Chanji.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .
Polisi Taarifa: **BUG/RB/388/2018**

115361002

### KUPOTEA KWA KADI

Kiluwa Steel Group Company Ltd anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T857 DDE aina ya MERCEDES BENZ yenye chasis namba WDC1648222A357803.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi .

Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/153855/2019**

115360702

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# EVERTON YAMSAJILI KEAN WA JUVENTUS




**LONDON,** England

EVERTON imemsajili fowadi wa Juventus, Moise Kean kwa ada ya uhamisho ya awali ya euro milioni 27.5 kwa mkataba wa miaka mitano.

Kean mwenye umri wa miaka 19, aliingia kwenye kikosi cha kwanza cha Juventus msimu uliopita akifunga mabao sita katika mechi 13 za ligi Kuu, akiisaidia klabu hiyo kutwaa taji la nane mfululizo la Serie A.

Pia alikuwa mchezaji kijana zaidi kuifungia Italia wakati ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Finland katika mchezo wa kufuzu michuano ya Euro 2020.

"Najisikia fahari kubwa kupewa heshima ya kuvaa jezi ya Everton. Nitajitahidi kwa hali na mali kuisaidia timu hii," amesema Kean.

"Nilishawishiwa kusajili kwa sababu Everton ni klabu kuwa yenye matarajio makubwa. Naujua ukubwa wa klabu. Nataka kufanya kazi na klabu hii, nitajitahidi kwa hali na mali.

"Nataka kuwa sehemu ya timu yenye mafanikio na nataka kushinda kitu nikiwa na timu hii." Kean amekuwa ni mchezaji wa tano kusajiliwa na Everton kipindi hiki cha majira ya joto baada ya viungo Andre Gomes, Fabian Delph na Jean-Philippe Gbamin pamoja na golikipa, Jonas Lossl.

"Mshambuliaji ilikuwa ni moja ya vipaumbele vyetu vya kusajili kipindi hiki cha majira ya joto," alisema kocha wa Everton, Marco Silva.

## *Malcom akumbana na ubaguzi*

**MOSCOW,** Urusi

WINGA wa Brazil, Malcon ambaye alijiunga na Zenit anaweza kuondoka klabuni hapo baada ya kukumbana na ubaguzi wa rangi.

Mchezaji huyo ambaye alijiunga na Zenit akitokea Barcelona kwa ada ya awali ya pauni milioni 41 wiki iliyopita, alizomewa na mashabiki wa timu hiyo katika mchezo wake wa kwanza Jumamosi, huku wakionyesha mabango ya kuwa hawataki mchezaji mweusi.

Zenit ilikuwa inacheza na Krasnodar na mashabiki hao walizomea kwa ubaguzi wa rangi Malcom.

Kwa mujibu wa Daily Mail zomea hiyo ilidumu kwa dakika 10 na kufanya uwanja huo kuzizima.

Taarifa za gazeti la AS zinasema kwamba, klabu hiyo sasa inafikiria kumuuza mchezaji huyo wakati wa dirisha dogo la usajili Januari ili kumuepusha na ubaguzi wa rangi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye alijiunga na Barcelona msimu uliopita kutoka Bordeaux ya Ufaransa, amecheza mehi 24 chini ya kocha ya Ernesto Valverde.



## Alli kukosa mwanzo wa EPL



**LONDON,** England

DELE Alli anaweza kukosa mwanzoni mwa msimu huu baada ya kuumia misuli ya nyama za paja na kuongeza pigo kwa kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino.

Spurs walifungwa kwa mikwaju ya penalti na Inter Milan Jumapili kwenye mchezo wao wa mwisho wa kujipima nguvu kabla ya kuanza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa.

"Siamini kama atakuwa fiti kwa ajili ya mwanzo wa msimu huu," amesema Pochettino. "Ameumia na nafikiri anaweza kuwa nje ya uwanja kwa muda kidogo.

"Bado ni kijana, ndio kwanza ana umri wa miaka 23, na amekuwa akiumia mara nyingi mno misuli ya nyama za paja kwa miaka michache iliyopita.

"Anatakiwa kutulia na kuangalia mwili wake unakuwaje, lakini tupo hapa kwa ajili ya kujaribu kuhakikisha kwamba anapona haraka.

"Tunafikiri kwamba atakuwa hajaumia kwa kiwango kikubwa, lakini zimebaki siku chache kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi na anaweza kurudi kundini baada ya wiki chache."

Pochettino anakabiliwa na majeruhi wengine ambapo Ben Davies anajiuguza kutoka kufanyiwa operesheni, huku Serge Aurier amefanyiwa operesheni ya mkono.

# Klopp amuonya Guardiola, Man City

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amemuonya Pep Guardiola na Manchester City kwamba Liverpool bado wako imara na watatoa ushindani mkubwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, licha ya kufungwa kwenye mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii juzi Jumapili.

City ilitwaa taji lake la kwanza kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu England baada ya kuibuka na ushindi kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 kwenye uwanja wa Wembley Jumapili baada ya kutoka sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90.

Mara baada ya mchezo huo, Klopp alisema ameridhishwa na kiwango cha timu yake hasa walivyocheza kipindi cha pili na anaamini watatoa changamoto kubwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2019-20.

"Kwa hakika walicheza kwa kiwango kizuri, hasa katika kipindi cha pili," alisema akiiambia BT Sport.

"Timu zote zilikuwa na msimu wa maandalizi unaofanana. Angalau tulistahili kusawazisha na niliridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji.

"Kiwango kilikuwa muhimu zaidi kuliko ushindi. Tunajua kwamba bado tuko fiti; tunaweza kutoa changamoto kubwa.

"Katika kipindi cha kwanza tungeweza kucheza vizuri, lakini tulikuwa na nafasi nzuri. Katika kipindi cha pili, tulibadilisha vitu vichache, tulitaka kupata matokeo, lakini tulishindwa, hongera kwao Man City."





# MAN UTD WAACHANA RASMI NA DYBALA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imesitisha rasmi mazungumzo na Paulo Dybala kwa ajili ya kumsajili baada ya kushindwa kufikia mahitaji ya mshahara anaotaka mshambuliaji huyo wa Juventus.

United ilianza mazungumzo kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 25, katika mpango ambao ungemhusisha Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 26 kwenda nchini Italia.

Hata hivyo, kiwango cha mshahara ambacho alikuwa akikihitaji Dybala kimeshindwa kufikiwa na Man United.

Ole Gunnar Solskjaer alikuwa akimhitaji zaidi mchezaji huyo kijana, lakini mahitaji ya maslahi yake binafsi ya Dybala yamewafanya maofisa wa Man United kuamua kuachana nae.

Dybala alijiunga na Juventus akitokea Palermo mwaka 2015 na alifunga mabao 10 kwa miamba hao wa Italia msimu uliopita, likiwemo bao pekee kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya mabingwa Ulaya hatua ya makundi dhidi ya United pale Old Trafford Oktoba mwaka jana.

Bado sasa majaliwa ya Lukaku ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji hayajulikana.

Lukaku ambaye alijiunga na mashetani wekundu hao akitokea Everton kwa ada ya awali ya pauni milioni 75 Julai mwaka 2017 na alifunga mabao 12 msimu uliopita, anataka kuondoka klabuni hapo.

Mwezi uliopita United ilikataa pauni milioni 60 iliyotolewa na wapizani wa Juventus kwenye Serie A, Inter Milan kwa ajili ya mshambuliaji huyo.

# *Lacazette hatihati kuikosa Newcastle*



**LONDON,** England

ALEXANDRE Alexandre Lacazette anakabiliwa na changamoto ya kupona haraka kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa Arsenal wa Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle, baada ya kuukosa mchezo wa mwisho wa maandalizi ya msimu dhidi ya Barcelona.

Mfaransa huyo aliumia kifundo cha mguu Ijumaa iliyopita wakati akicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Lyon, huku kocha Unai Emery akiwa bado hajafanya maamuzi ya kumjumuisha au la.

"Matumaini yangu atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo dhidi ya Newcastle na madaktari watatoa tathmini yake, lakini kwa sasa bado haijulikani," alisema Emery.

"Kama atakuwa tayari kwa ajili ya mchezo ujao, hili ni suala la madaktari."

Akiwa ameukosa mchezo wa Jumatato wa ushindi dhidi ya Angers, Lacazette pia aliukosa mchezo wa kichpo cha mabao 2-1 Jumapili pale Nou Camp, wakati Luis Suarez akifunga bao la ushindi dakika ya mwisho baada ya Ainsley Maitland-Niles kusawazisha kwa kujifunga baada ya Pierre-Emerick Aubameyang kuanza kufunga.

# DONDOO OKA MAGAZETI Y AYA



# BARCA: HATUMTAKI NEYMAR KWA SASA

**Hatujazungumza nao, ila leo, kwa wakati huu suala hilo sasa limewekwa kando...**

**BARCELONA,** Hispania

MAKAMU wa Rais wa Barcelona, Jordi Cardoner amesema mpango wa kwenda kumsajili Neymar kutoka Paris Saint-Germain unaweza kuwekwa kando kwa wakati huu.

**Sky Sports News inatambua mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Brazil ameiambia PSG anataka kuondoka majira haya ya joto.**

Lakini pia inaeleweka mabingwa hao wa Ufaransa watakubali kumuuza endapo tu wataweza kupata pauni milioni 200 ilizotumia kumnunua Neymar kutoka klabu hiyo ya Hispania mwaka 2017 ama kama mpango huo utahusisha kupewa na baadhi ya wachezaji.

Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo amesisitiza kumekuwa "hakuna ofa nono" iliyowafikia hadi sasa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.

Wakati alipoulizwa kuhusu kuwapo kwa mpango huo kwa Neymar, Cardoner alikiambia kituo cha televisheni cha TV3: "Kama ilivyo leo, hakuna suala la Neymar, kama rais alivyosema, na kuna utata.

"Sisi ni watendaji tu. Tunajua hana furaha Paris na ni hali ambayo inahitaji kutatuliwa Paris.

"Hatujazungumza nao. Kuna heshima nyingi kati ya klabu hizi na kama kuna suala la Neymar siku moja, tutazungumza.

"Leo, kwa wakati huu, limewekwa kando."

Mchambuzi wa soka la Ufaransa Jonathan Johnson, amesema Philippe Coutinho ni "ufunguo" kwa mpango wowote muhimu ambao unaweza kushuhudia Neymar akijiunga tena na Barcelona akitokea PSG.

"Kuna wachezaji fulani PSG wanajua wasingependa," Johnson aliiambia Sky Sports News.

"Hawatakuwa tayari kabisa kwa Umtiti kwa sababu ya historia yake ya kuwa majeruhi. Mimi pia huongozwa kuamini Umtiti hataki kujiunga na PSG ama hata kwa upande wa Rakitic.

"Mchezaji ambaye anaweza kuwa pamoja katika mpango kama huu kwa sasa ni Coutinho. Anaweza kuwa ufunguo muhimu kwa mpango huu.

"Mchezaji mwingine ambaye anaweza kuhitajika PSG, na pengine nafasi wanaoitazama kuiimarisha tangu Dani Alves alipoondoka akiwa mchezaji huru, ni Semedo upande wa beki ya kulia.

"Hivyo PSG pengine inaweza kututumai kwamba Barcelona wangeweza kuwa tayari kujitoa sadaka ili kufanikisha mpango huo."

## ZISIKUPITE

### MANDZUKIC KUTUA UNITED

MANCHESTER United imekubali mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Mario Mandzukic, 33, kwa pauni milioni 6.2. Nyota huyo wa kimataifa wa Croatia anaweza kuigharimu pauni milioni 15 ama kwa kujumuishwa na mapngo wa kubadilishana kwa straika wa United, Mbelgiji Romelu Lukaku, 26. ***(Mail)***

### REAL YAGOMEWA KWA POGBA

MANCHESTER United imekataa ofa kutoka Real Madrid kwa kiungo wao wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, ambayo inamjumuisha mshambuliaji Mcolombia James Rodriguez, 28, kama sehemu ya kubadilishana. ***(Sun)***

### ICARDI APIGWA MKWALA INTER

INTER Milan imemwambia straika Muargentina Mauro Icardi, 26, hatacheza kwa miaka miwili kama ataendelea kusisitiza kukaa hadi atakapomaliza mkataba wake klabuni hapo. ***(Gazzetta Dello Sport - in Italian)***

### BARCA YAAHIDI MAJEMBE ZAIDI

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amependekeza kuwa mabingwa hao wa Hispania watasajili 'jembe' jipya baada ya kuthibitisha kutua kwa beki wa kushoto wa Hispania U-21, Junior Firpo, 22, kutoka Real Betis. ***(Sport)***

### YAMGEUKIA VAN DE BEEK

REAL Madrid imeamua kuinasa saini ya kiungo wa Ajax, Mholanzi Donny van de Beek, 22, kuliko kumgeukia Paul Pogba wa Manchester United. ***(Marca)***

### AKE KUMRITHI MAGUIRE

LEICESTER City inazingatia kupata huduma ya ama beki wa beki wa Burnley, Muingereza James Tarkowski, 26, ama beki wa kati wa wa Bournemouth, Mholanzi Nathan Ake, 24, kama mbadala wa nyota wa kimataifa wa England, Harry Maguire, 26. ***(Sky Sports)***

### CANCELO KUPISHANA DANILO

MANCHESTER City inajiandaa kuingia vitani kuwania saini ya beki wa Juventus na Ureno, Joao Cancelo, 25, kwa pauni milioni 32, huku beki wa kulia Mbrazil Danilo, 28, akielekea upande wa pili. ***(Mail)***

### KUMPOTEZEA CARROLL

NEWCASTLE United hataenda kumsajili straika wao wa zamani Andy Carroll, 30, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka West Ham United. ***(Mirror)***

### CHAMBO YA SESSEGNON

TOTTENHAM inajiandaa kumjumuisha kiungo Muingereza Josh Onomah, 22, katika mpango wao wa pauni milioni 30 wa kumsajili beki wa Fulham na England U-21, Ryan Sessegnon, 19. ***(Mail)***

### MIGNOLET ATAFUTIWA MBADALA

LIVERPOOL inaitaka saini ya kipa wa Southampton, Muingereza Alex McCarthy, 29, na kipa wa zamani wa West Ham, Mhispania Adrian, 32, kama mbadala wa Mbelgiji Simon Mignolet, 31. ***(Liverpool Echo)***

### WAIKATALIA EVERTON

WATFORD imekataa kutoa ofa ya pauni milioni 32 kwa kiungo wa Everton, Mfaransa Abdoulaye Doucoure, 26. ***(RMC, via Express)***

# Yanga haipoi, yaifuata Mlandege Zanzibar

**Na Shufaa Lyimo**

YANGA haitaki 'kupoa' kuelekea dhamira yao ya kufanya vizuri kwenye mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana utakaopigwa Uwanja wa Taifa Jumamosi, kwani leo inaelekea Zanzibar kutafuta kasi zaidi ya mechi hiyo ya raundi ya kwanza.

Juzi katika Uwanja wa Taifa, Yanga ilihitimisha Wiki ya Mwananchi kwa kufanya tamasha kubwa ambalo walilitumia kutambulisha jezi za msimu huu, wachezaji wao wa msimu mpya ikiwa ni pamoja na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya, ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Lakini leo kikosi hicho kinatarajia kuelekea Zanzibar kujiandaa na mechi dhidi ya Township Rollers kwa kucheza mechi mbili za kirafiki visiwani humo kabla ya kurejea kwa mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa.

Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya Yanga jana, Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Frederick Mwakalebela (pichani chini), alisema timu yao leo mchana itaondoka kuelekea visiwani Zanzibar kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo wa Jumamosi.

Alisema wakiwa visiwani humo watacheza michezo miwili ya kirafiki kabla ya kurejea Ijumaa ya wiki hii tayari kuivaa Towship Rollers.

Aliongeza Kocha Mkuu Mwinyi Zahera ameahidi kukiboresha kikosi hicho na kudai ana uhakika wa kuanza kwa ushindi nyumbani.

"Jumatano usiku tutacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mlandege na Alhamisi usiku tutacheza dhidi ya Malindi, lengo la kucheza usiku ni ili kila mtu aweze kuona kikosi chake," alisema mwenyekiti huyo.

Kwa upande wake Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Dismas Ten, alisema mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa utachezwa saa 12 jioni na kuwataka mashabiki wao kujitokeza kwa wingi kama walivyofanya kwenye siku ya kilele cha Wiki ya Mwananchi.

Aidha, alitaja viingilio vya juu vya mchezo huo kuwa ni Sh. 50,000 na Sh. 15,000 wakati cha chini kitakuwa Sh 5,000.



# NDAYIRAGIJE AFUNGUKA UDHAIFU TAIFA STARS

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kuitupa nje timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars, katika mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Kocha wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragije, amesema bado kuna makosa machache anapaswa kuyafanyia kazi kabla ya kuivaa Sudan kwenye mechi ijayo.

Ikiwa ugenini katika Uwanja wa Kasarani nchini Kenya, Taifa Stars juzi iliibuka na ushindi wa penalti 4-1 baada ya dakika 90 za mchezo kumalizika kwa sare tasa kama ilivyokuwa kwenye mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam wiki moja iliyopita.

**Lakini pamoja na kufanikiwa kusonga mbele, Ndayiragiji ameliambia Nipashe kuwa amebaini makosa machache kwenye safu ya kiungo na ushambuliaji na kuahidi kuyafanyia kazi mapema.**

Akizungumza na Nipashe jana, kutoka Kenya Ndayiragije alisema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na mlinda mlango wake Juma Kaseja kwa kazi kubwa aliyoifanya.

"Tunashukuru tumefanikiwa kusonga mbele kitu ambacho tulikuwa tunakiomba kila siku, kiukweli Kaseja amefanya kazi kubwa," alisema na kuongeza:

"Vijana wamejituma, lakini kwenye safu ya umaliziaji, haina umakini nitaifanyia kazi kwa sababu bado tuna muda mrefu wa kujiandaa kabla ya kukutana na Sudan".

Aidha, aliwashukuru Watanzania kwa ushirikiano waliowaonyesha kuelekea kwenye mchezo huo, ambao ulikuwa na ushindani mkubwa.

Aliwataka wachezaji wake kuwa makini ili kufikia malengo waliyojiwekea na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (wa pili kulia) akiwasili eneo unapojengwa Uwanja wa mazoezi wa Simba, Bunju jijini Dar es Salaam tayari kwa uwekaji jiwe la msingi. Wa tatu kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Mohamed "Mo" Dewji, akiwa na viongozi wengine wa Simba na mashabiki wa timu hiyo. **PICHA: SIMBA NEWS**

# MO aitaka Simba B Daraja la Kwanza

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Mohamed "Mo" Dewji, amezidi kuwapagawisha mashabiki na wanachama wa klabu hiyo baada ya kueleza ataandika barua Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuomba Simba B iruhusiwe kucheza Ligi Daraja la Kwanza.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa uwanja wao mpya wa mazoezi Bunju jijini Dar es Salaam, Mo alisema lengo lake ni kutaka kuifanya Simba B kuwa kituo chao cha kuzalisha vipaji na kuvihamishia timu ya wakubwa.

Alisema kama TFF itamkubalia, gharama zote za kuihudumia timu hiyo itakuwa juu yake kwa sababu anataka kuona Simba ikiwa chanzo cha kuzalisha vipaji nchini.

"Mimi ni shabiki kindakindaki wa Simba, ninataka kuona tukizalisha vipaji, hivyo nitaandika barua TFF kuomba Simba B iruhusiwe kucheza Ligi Daraja la Kwanza," alisema huku akifafanua kuwa gharama zote za ujenzi wa uwanja huo hazihusiani na dau la Sh. bilioni 20 alilotangaza kuwekeza Simba.

Mgeni rasmi katika uwekaji wa jiwe hilo la msingi alikuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe.

## Jang'ombe Boys waahidi makubwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Jang'ombe Boys inayocheza Ligi Kuu Zanzibar imesema msimu huu imepanga kufanya maajabu katika ligi hiyo ili kurejesha hamasa kwa mashabiki wake walioibeza kutokana na matokeo mabaya ya msimu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa timu hiyo, Ali Othman alisema kikosi cha msimu huu kipo vizuri kutokana na kufanya usajili aliouita ni wa nguvu.

Alisema timu hiyo imesajili wachezaji 15 kutoka madaraja mbalimbali na kwamba tayari viwango vya wachezaji hao vinaendana na kasi ya timu hiyo.

Akitaja nafasi walizosajili, alisema ni makipa watatu, mabeki watano, washambuliaji watano, pamoja na viungo wa kati wawili.

Michezo
Jumanne Agosti 6, 2019
Nipashe



## Barca: Hatumtaki Neymar kwa sasa

UKURASA 30

**KIMBIZA...**



Mabeki wa Arsenal wakijaribu kumdhibiti Luis Suarez kwa kumweka 'mtu kati' katika mechi ya kujiandaa na msimu mpya iliyopigwa Uwanja wa Nou Camp juzi usiku na miamba hiyo Emirates kukubali kipigo cha mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Zahera: Huyu Sadney subirini

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya mashabiki wa soka kumponda mshambuliaji mpya wa Yanga, Mnamibia Sadney Urikhob kwa kukosa nafasi nyingi juzi katika mechi ya kirafiki dhidi ya Kariobangi Shark's, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mwinyi Zahera, amefunguka kuwa huyo ndiye aina ya straika aliyekuwa akimtaka kutokana na kasi yake uwanjani.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mchezo wao ulioisha kwa sare ya bao 1-1, Uwanja wa Taifa juzi kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi, Zahera alimsifu Sadney na kudai ni aina ya wachezaji aliokuwa anawahitaji kwa muda mrefu.

"Sadney ana mbio sana uwanjani hakuna mchezaji anayemfikia kwa sababu yuko speed hana masihara akiwa anacheza ndio maana nikamsajili na ataleta mafanikio msimu ujao wa ligi na Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Zahera. "Kikosi kilichopita kilikuwa kina wachezaji ambao wakiingia kucheza wanatembea badala ya kukimbia hali hiyo ilikuwa inaniumiza sana," alisema kocha huyo.

Aidha alidai kulikuwa kuna mapungufu makubwa katika upande wa wachezaji wa pembeni, ambayo atayafanyia kazi na kwamba kwa siku zilizobaki kabla ya kuanza mashindano zinamtosha kumaliza tatizo hilo.

Yanga leo inatarajia kuelekea Zanzibar kwa ajili ya mechi mbili za kirafiki dhidi ya Mlandege Jumatano na Malindi Alhamisi kabla ya kurejea jijini Dar es Salaam Ijumaa kwa kuivaa Township Rollers ya Botswana kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Jumamosi.

# Simba: Nchi itasimama

### Mo Dewji afunguka Sh. bilioni 20, Manara aahidi kuja kivingine leo akidai Yanga kuiga...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Uongozi wa Klabu ya Simba ukisema kuelekea kilele cha SportPesa Simba Wiki nchi leo itasimama kutokana na walivyojipanga kufanya makubwa msimu ujao na wakianza kuonyesha cheche hizo watakapoivaa Power Dynamos katika Uwanja wa Taifa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji amewapagawisha zaidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

**Simba leo itafikia kilele cha SportPesa Simba Wiki kwa kufanya tamasha kubwa katika Uwanja wa Taifa ambapo pamoja na mambo mengine itawatambulisha wachezaji wake na jezi za msimu mpya huku ikicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.**

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema wapo tayari kwa mchezo huo wa kirafiki na kwamba wataonyesha kile walichokifanya katika Kambi ya kujiandaa na msimu mpya nchini Afrika Kusini.

"Maandalizi tuliyofanya Afrika Kusini ni mazuri na tupo tayari kwa ajili ya ushindani wa kimataifa na kitaifa, hivyo tuna amini tutafanya vizuri kwani muda upo na uwezo tunao," alisema.

Kwa upade wa Mo, akizungumza katika hafla fupi ya uwekaji jiwe la msingi katika Uwanja wa mazoezi wa Simba uliopo Bunju jijini Dar es Salaam, aliwakuna mashabiki wa klabu hiyo kwa kueleza kuwa uwekezaji wake wa Sh. bilioni 20 haupo kwenye mpango wa Uwanja wa Bunju na kwamba kiasi cha fedha alichotoa amejitolea kama shabiki wa Simba.

"Mimi ni shabiki kindakindaki wa Simba, Sh. bilioni 20 nilizotangaza kuwekeza Simba hazipo katika ujenzi wa uwanja huu, lakini pia ninataka kuandika barua TFF kuomba Simba B iruhusiwe kucheza Ligi Daraja la Kwanza na nitaihudumia kwa fedha zangu ili viwe kuzalisha vipaji kwa ajili ya timu ya wakubwa," alisema na kushangiliwa na umati wa mashabiki waliohudhuria hafla hiyo ambayo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe.

"Uwanja huu unajengwa kwa bajeti inayojitegemea tofauti na ile Sh. bilioni 20 ambazo nilisema nitaweka, ninachotaka tuwe na miundombinu mizuri na tunajenga viwanja viwili ambapo kimoja ni cha nyasi bandia na kingine ni cha nyasi asilia."

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, akizungumzia kuhusu kilele cha SportPesa Simba Wiki, amesema leo lazima aje na mtindo mpya wa utambulisho baada ya ule wa awali kudai umeibwa na watani zao, Yanga kwenye utambulisho wao juzi. Yanga juzi ilihitimisha Wiki ya Mwananchi Uwanja wa Taifa kwa kutambulisha wachezaji wa msimu mpya na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Kariobangi Shark's ya Kenya katika mechi iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1.

Lakini Manara kupitia ukurasa wake wa Instagram jana alisema: "Yupo Haji Manara mmoja tu Bongo!! Uhai na Majaliwa tu ila kesho (leo) taifa hili tutalisimamisha kupisha Simba Day!!

"Wameiga style yangu ya utambulisho ila kesho nakuja vingine!! Hapa ni University kamili, hadi PhD natoa!! Ukikosa kesho (leo) umeliwa.

"Kesho ni watu elfu sitini kamili na haijalishi kwetu kama ni siku ya kazi!!Halafu hili goli la Kario***c, lilifungwa second half kabla ya tuta la hisani? Okey Simba ni next level nyie*** mliopooza kama***."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002